**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3. Thuwaibah Edington Kissasi | Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake. |
| 4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 7.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 8.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni. |
| 9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 15.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 16.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 17.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 18.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 21.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 22.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 24. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 26.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 28.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 29.Mhe. Zahra Ali Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 31.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando. |
| 32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Omar Ali Shehe | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43. Mhe. Abass Juma Muhunzi | Jimbo la Chambani. |
| 44.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 45.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 46.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |

| | |
|---|---|
| 47.Mhe. Ali Moh'd Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 48.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 49.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 50.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 53. Mhe. Asha Moh'd Hilal | Jimbo la Magogoni. |
| 54.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 59.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 61.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 63. Mhe. Juma Duni Haji | Uteuzi wa Rais |
| 64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Uteuzi wa Rais |
| 70.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 71.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 73.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 74.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 75.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 76.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 77.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |

| | |
|---|---|
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.** |

**Kikao cha Sita – Tarehe 18 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 66**

**Kamati ya Maadili ya Baraza**

**Mhe. Hija Hassan Hija** – Aliuliza:-

Kwa mujibu wa Kanuni zake Baraza la Wawakilishi lina uwezo wa kuanzisha Kamati mbali mbali zikiwemo Kamati za Kudumu *(Standing Committees)* kama linavyoona inafaa.

(a) Je, Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawkilishi ni miongoni mwa Kamati ya Kudumu *(Standing Committee)* ya Baraza hilo?

(b) Kama ndiyo, je inafanyakazi kwa mazingira na wakati gani?

(c) Wenyeviti wa Kamati nyengine za Kudumu za Baraza ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Baraza na hushiriki vikao vya Kamati ya Uongozi na kupata stahili zao. Je, vipi kuhusu Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili?

**Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi -** Alijibu:-

Mhe. Spika naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Kamati za Maadili ni miongoni mwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Kanuni ya 104(g) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2009.

(b) Kwa mujibu wa Kanuni ya 114(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Kamati hii hufanya shughuli zake endapo kutahitajika kuchunguzwa au kutolewa maamuzi juu ya masuala yote yanayohusu

kinga, fursa, mamlaka na madaraka ya Wajumbe wa Baraza pamoja na mamlaka na madaraka ya Mhe. Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza ambayo yamepelekwa mbele ya Kamati na Spika au Mjumbe yeyote wa Baraza. Aidha, Kamati hii huchunguza na kumshauri Spika kwenye Baraza juu ya lalamiko lolote kuhusu uamuzi wa Spika, Naibu Spika, au Mwenyekiti wa Baraza ambalo limepelekwa mbele ya Kamati hiyo na Mjumbe yoyote.

(c) Kama nilivyoeleza hapo awali, Kamati ya Maadili ni moja miongoni mwa kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 107(f) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza. Hata hivyo, kuna utofauti mkubwa wa kiutendaji baina ya kamati ya Maadili na kamati nyenginezo za kudumu za Baraza. Kiutaratibu, Kamati ya Maadili hufanya kazi zake pale tu linapotokea jambo maalumu kama Kanuni ya 114(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar,

Mhe. Spika, Toleo la 2009 inavyoeleza. Nathubutu kusema kuwa katika kipindi chote cha Baraza la Saba, Kamati hii imekutana mara moja tu, kinyume na Kamati nyengine za Kudumu za Baraza ambazo hukutana wiki mbili kabla ya kila Mkutano wa Baraza kama maamuzi ambayo tukafanya marekebisho ya Kanuni katika kipindi kilichopita. Mantiki kubwa ya wenyeviti wa Kamati za kudumu kuingizwa kwenye Kamati ya Uongozi ni kutoa fursa kwa wenyeviti hao kuwasilisha taarifa muhimu zinazohusu Kamati zao katika vikao vya Kamati ya Uongozi. Ni wazi kuwa Kamati ya Maadili kiasili haikuwa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu. Kamati hii ilianzishwa na ilifanywa kuwa ni miongoni mwa kamati za kudumu katika marekebisho ya Kanuni za Baraza yaliyofanyika katika mwaka 2005.

Hata hivyo, kamati hii haifanyi kazi kwa kuendelea kama zilivyo kamati nyengine bali hukutana kwa nadra pale tu inapotokezea jambo linalohitaji kushughulikiwa na kamati hii. Kwa mazoea hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili alikuwa haalikwi kuhudhuria mikutano ya Kamati ya Uongozi. Hiyo ilikuwa ni kasoro kubwa lakini sasa tayari imerekebishwa.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu yenye ufafanuzi mzuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa wamekiri kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ilikuwa haalikwi kwenye Kamati ya Uongozi, na hiyo ni kasoro kubwa ambayo Baraza ilikuwa inafanya.

(a) Je, tangu kuonekana kwa dosari hiyo ni vikao vingapi Mwenyekiti huyu amehudhuria?

(b) Nilitaka kujua wenzake wenyeviti wa Kamati nyengine hupata stahili kama wenyeviti. Je, humu muda wote alikuwa akipata stahili hizo na kama alikuwa hapati je, kuna malipo ya a*rrear* ya stahili zake?

**Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba hapo mwanzo alikuwa haalikwi katika vikao vya Kamati ya Uongozi huyu Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili.

(a) Kwa kuwa suala hilo tuliliona ni kasoro lakini sasa hivi tumelifanyia marekebisho. Kwa ghafla kuweza kumwambia kwamba tumemualika katika vikao vingapi sitoweza kumjibu kwa haraka haraka kwa sababu sina uhakika. Chombo hiki ni chombo kizito sana kila unachokizungumza unatakiwa uwe umekifanyia utafiti wa kina. Kwa kuwa hili suala lipo ndani ya shughuli zetu za Baraza basi ndani ya kikao hichi hichi nitamjibu Mheshimiwa Mujumbe kwamba amealikwa vikao vingapi.

(b) Suala la stahili haya mara nyingi yanakuwa ni maamuzi ya Kamati ya Uongozi. Hapo mwanzo kama nilivyosema mtu analipwa kwa mujibu wa zile kazi anazozifanya. Ukiangalia wenyeviti wa Kamati hizi nyengine za kudumu, kwa kweli kila baada ya miezi mitatu kamati zinafanya kazi mfululizo kwa muda wa wiki mbili. Hata huyu Mwenyekiti wa hii Kamati ya Maadili na eye ni Mjumbe katika Kamati nyengine ambazo anapata stahili vile vile kama wenzake wanavyopata. Kwa kuwa hii kamati shughuli zake ni nadra tu kwa hiyo bado sishawishi Kamati ya Uongozi lakini bado sijaona umuhimu zaidi.

Kwa sababu haya maposho tunayolipwa ni kodi za wananchi na kodi za wananchi kwa kweli tunatakiwa tuzitumie vizuri sana ili wananchi waweze kufaidika na mchango wetu kama Baraza la Wawakilishi linavyotaka. Kwa hiyo suala la stahili tutajaribu kulizungumza tena kwenye Kamati ya Uongozi. Kwa sababu katika Kamati ya Uongozi kama alivyosema wenyeviti wote wa Kamati zote wanahudhuria, kwa hivyo yale maoni na michango itakayotoka pale tutajaribu kuangalia kama tutaona iko haja na yeye tutamuangalia.

Lakini pamoja na hayo tuangalie mtu kile anacholipwa na ile kazi ambayo anaifanya. Kamati hii kama tulivyosema tokea kuanzishwa imefanya kazi mara moja tu. Sasa ukija ukimmiminia mtu marupurupu na mambo mengine kwa kazi ambayo ilifanyika mara moja tu inakuwa kidogo hatuwatendei haki wananchi wetu. Ahsante.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kwa ruhusa yako namba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza lako hili ni mihimili au kazi yao kubwa ni kuhakikisha kwamba ndio Kamati ya Uongozi ya Wajumbe wote wa Baraza hili na linalotokea lolote kwa utendaji au utekelezaji wao ndio mstari wa mbele katika kupitisha mambo mbali mbali kwa maslahi ya Baraza hili pamoja na wafanyakazi wake. Swali langu lipo hapa.

(a) Kwa kuwa Kamati ya Maadili inatokana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini na Kamati ya Uongozi ni moja katika uongozi wa kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda sawa sawa ili pasitokee tatizo kwa wajumbe wetu na Baraza zima la Wawakilishi. Hivyo Mhe. Waziri haoni kwamba ipo haja katika vikao vya Kamati ya maadili na wajumbe hao wenyeviti wakawekwa kwenye kamati hiyo; na

(b) Labda nimuulize Mhe. Waziri nani hasa mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza hili.

**Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:**

(a) Mhe. Spika, Mheshimiwa Mwakilishi ameomba kwamba Wenyeviti wa Kamati vile vile wawe ni Wajumbe wa Kamati ya Maadili. Nadhani katika Kanuni zetu za Baraza na kanuni hizo tumezitengeneza sisi wenyewe. Kwa hivyo mimi nawaomba sana Waheshimiwa kile ambacho tulichokwisha kukiamua basi tuendelee kukitekeleza. Kwa sababu sisi tunatakiwa tuwe mfano bora katika suala zima la utawala bora la kufuata sheria. Sasa kwa kuwa Kanuni yetu inaeleza vizuri basi nafikiri ufafanuzi wetu kama Kanuni yetu inavyoeleza katika Kamati ya Maadili; na

(b) Vile vile ametaka kujua nani Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili. Hili suala ni kwamba Kamati ya Maadili ni nyeti. Nitamtaja kwa sababu Baraza hili Mhe. Spika, linataka uwazi. Kwa hivyo Mwenyekiti wa kamati ya Maadili ni Mhe. Thuwaibah Edington Kissasi. (*Makofi*)

Lakini naomba waheshimiwa msianze kumchukia kwa sababu hii dhamana ambayo tumempa sisi wenyewe. Vile vile nataka nirejee kwa Mhe. Hija kwa sababu nilieleza kwamba nitamjibu Mhe. Thuwaibah kwa kuwa yeye ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili lakini vile vile sasa hivi ni Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo anaingia katika Kamati ya Uongozi kwa nyadhifa hiyo ya Mwenyekiti sasa hivi. Kwa hiyo tayari ameshaingia na hakuna namna nyengine ya kuweza kumtoa, ana vyeo viwili na vyote anavitumikia ndani ya Kamati ya Uongozi. Ahsante.

**Nam. 46**

**Hifadhi ya Msitu wa Ngezi**

**Mhe. Ali Abdulla Ali** – Aliuliza:-

Msimu wa Hifadhi ya maumbile wa Ngezi Vumawimbi ni moja kati ya maliasili ya misitu ya Asili iliyobakia kisiwani Pemba. Msitu huo wenye eneo la hekta 2900 sawa na 20 km na miti 355 tofauti ambayo baadhi yake haipatikani katika sehemu yoyote nyingine Duniani ulitangazwa rasmi kuwa msitu wa Akiba *"Forest Reserve"* tangu mwaka 1959. Hivi sasa katikati ya msitu huo imepita barabara inayokwenda kijiji cha Makangale.

(a) Mhe. Waziri, pamoja na kwamba Barabara ni sehemu muhimu ya maendeleo ya jamii, huoni kwamba kupita kwa barabara katika eneo hilo ni kukaribisha uharibifu wa msitu huo; na

(b) Kwa kuzingatia suala hilo na kwa kuwa msitu ni kitega uchumi na eneo hilo limetangazwa kiutalii, huoni haja ya kuihamishia njia hiyo eneo jingine ili kuhifadhi mali ya asili hiyo isipotee kabisa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi** – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa kuwa wazima ili kuhudhuria kikao cha Baraza.

Mhe. Spika vile vile kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo. Suala lililoulizwa linahusiana na barabara ya Msitu wa Ngezi na uharibifu wa mazingira kutokana na barabara iliyokuwepo. Mhe. Spika, ni kwamba ule msitu ni moja katika maeneo ambayo yanatembelewa na wageni mbali mbali. Sasa tunaposema kwamba tusiwe na barabara ya kufika pale sasa sijui hao wageni ambao tunaowategemea wafike pale watafikaje.

Mhe. Spika, pia msitu wa Jozani nao vile vile barabara imepita kati kati tena barabara kuu. Kwa hiyo mimi nafikiria suala hili tuliangalie vyema, lakini baada ya hapo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kupita kwa barabara katika eneo la Msitu wa Ngezi ni kukaribisha uharibifu wa msitu huo, ndio maana hadi leo wizara yangu haijaweza kujenga barabara katika eneo hilo hivyo kupelekea hadi sasa kutumika barabara ya asili na ya miaka mingi; na

(b) Kwa muda mrefu wizara yangu imekuwa ikiliangalia suala la kujenga barabara hiyo kwa kuimarisha sehemu nyengine lakini kutokana na maumbile na ukubwa wa Msitu huo ni lazima ukutane nao kabla ya kufika vijiji vya Makangale, Vumawimbi, Mkia wa Ng'ombe na vijiji vyengine. Hata hivyo wizara yangu tayari ipo tayari kupokea mawazo na maelezo kutoka kwa Waheshimiwa na wananchi wengine ili kusaidia kupatikana njia nyengine mbadala kwa sehemu hiyo.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi naomba nimuulize kama ifuatavyo:-

Anakiri kwamba Barabara hii iliyopita katika msitu wa ngezi ni muhimu kwa sababu kule upande wa pili kuna hoteli nyingi za kitalii na watalii anahitajika kwenda kule. Tatizo la pale ni tatizo la mazingira je, waliwahi kukaa na watu wa mazingira wakatafuta mawazo na njia bora ili njia hiyo ikatengenezwa bila ya kuharibu hayo mazingira ya ule msitu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa ile njia na kwamba kule nako wanaishi binaadamu na pale pana msimu muhimu kwa taifa, Wizara yangu imeshafanya vikao na watu wa Misitu na watu wa Mazingira, wao wakatwambia kwamba tujenge barabara lakini tusipitishe pale. Tukawauliza tupitishe wapi mpaka leo hawajatupa jibu.

Na ukweli kutoka pale kwenda Makangale kwa kujenga barabara usiuguse msitu ule ni jambo gumu sana sijui utapitia wapi. Unajua kutoka Konde mpaka Makangale ni kilomita 12 na kutoka Konde mpaka mnarani ni karibu kilomita 15 ni umbali ambao unahitaji barabara lakini bado tunakwazwa sisi kama Wizara ya Mawasiliano hatuwezi tukapinga maagizo ya Mazingira au watu wa misitu. Lakini bado wananchi upande mmoja wanapiga kelele hawana barabara na upande wa pili huku tunakatazwa.

Kwa hivyo sisi tupo ni watu ambao tupo tayari kushirikiana na pande zote mbili. Mhe. Mwakilishi na watu wake na upande wa pili Idara ya Kilimo na Mazingira. Kwa hivyo hali halisi iko hivyo. Uwezo wa kujenga pale tunao lakini hali bado haituruhusu.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, kwanza hapo ulipozungumza Msitu wa Hifadhi wa maumbile ya Ngezi Vumawimbi. Mimi nilitaka afanye marekebisho kidogo. Msitu wa ngezi uko mbali na Vumawimbi iko mbali, Vumawimbi iko pwani na Ngezi ndio ngezi ambao ndio upo huo msitu wenyewe.

La pili Mhe. Spika, ni kwamba barabara hii ambayo inakata katikati ya msitu ni barabara muhimu sana kwa watu wote, hatuwezi tukaiondosha barabara ile pale ilipo na tukaipeleka pahala pengine zipo sababu za msingi ambazo inashindikana barabara ile kupelekwa upande wa pili. Kwa sababu upande wa pili kuna mto mkubwa sana ambao haiwezekani upande wa pili kupitisha barabara.

Mimi namuomba Mhe. Waziri kwamba hili suala aliangalie kwa uangalifu sana kwamba hiyo hoja iliyoletwa kwamba kuna uharibifu wa msitu miye sioni uharibifu wa msitu huo. Kwa hivyo naomba hili suala aliangalie kwa vizuri. Ni maelezo tu sio swali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, mimi sina matatizo na ombi la Mhe. Suleiman. Lakini kwa utaratibu ambao upo serikalini barabara yoyote ambayo tunajenga sisi ni lazima tupate ushauri na watu wa mazingira.

Sasa huu mpira haupo kwangu, upo kwa Waziri wa Mazingira aangalie kama itawezekana hatuwalazimishi kwa sababu na wao wanajua nini kinatakiwa kifanywe katika mazingira. Kwa hivyo wakisema Ok, inaweza ikapitishwa lami, sawa. Wakisema tuweke kifusi tu, sawa. Wakisema tuiwache vile vile mashimo tu, sawa.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru ili na mimi nitoe maelezo ya ziada pale alipomalizia kaka yangu Mhe. Machano. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wawe waangalifu kidogo na suala hili la mazingira. Suala hili la kutaka kupitisha barabara katika msitu wa ngezi limekuwa likijitokeza mara kwa mara katika Baraza lako tukufu hili.
Sisi kama serikali tumekuwa tukiwasiliana na wataalamu wa mazingira na maelezo wanayotupa ni kwamba kunaweza kukatokea uharibu wa mazingira. Mhe. Suleiman hapa anasema yeye halioni tatizo, lakini mimi tatizo naliona kwa sababu vyombo ambavyo vinatumika katika kutengeneza barabara sote

tunavijua, ni vyombo ambavyo vikubwa na vizito. Sasa kuvipitisha katika msitu ule halafu mtu anasema yeye tatizo halioni mimi kidogo inanipa mushkeli.

Jana mtakumbuka wakati Mhe. Ali Haji Ali alivyokuwa akitoa mchango wake, nilivutiwa sana. Alisema anavyohisi yeye mara nyingi sisi katika serikali anavyoona yeye akasema yapo mambo ambayo tunayafanya lakini haufanyiki utafiti mkubwa sana wa kitaalamu. Akaishauri serikali akasema tuanzishe sasa kitengo maalum ambacho kiwe ni cha masuala hasa ya utafiti kwamba maamuzi yote tunayoyafanya. Lile jambo sio la kulipuuza sana mfano mzuri sasa tutekeleze hoja ile hapa Barazani. Maana hoja ile imetolewa hapa Barazani sasa sisi tuwe wa mwanzo kuzingatia mawazo ambayo wenzetu wamekuwa wakitoa.

Ushauri ule mimi umenivutia sana. Pamoja na umuhimu wa kupitisha barabara maana ni kweli barabara ni muhimu sana lakini na hili la mazingira na utunzaji wa msitu ni muhimu zaidi. Ushauri wangu nasema tuendelee kushirikiana na wataalamu. Sisi kama serikali tuendelee jambo hili kulifanyia utafiti wa kutosha. Tatizo ninaloliona tukifanya maamuzi ya haraka tukatengeneza barabara, tukapitisha vifaa vizito halafu msitu ule ukaharibika sisi tutakuwa na dhima kubwa kwa watoto na wajukuu wetu watakaokuja.

Naomba niwape ripoti tulipokuwa katika mkutano wa Dunia pale Dar-es-Salaam mwaka huu. Tulizungumza kwa undani sana masuala yanayohusu uharibifu wa mazingira na masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Jambo moja kubwa hasa katika hizi nchi zetu zinazoendelea linaathiri sana sasa hivi kumekuwa na ukataji mkubwa sana wa miti. Sasa wataalamu wanatwambia moja katika kazi kubwa sana ya miti kufyonza hewa. ya joto *carbon dioxide*. Sasa tukihatarisha hii miti na hasa kwa watu wanaoishi kwenye visiwa kama ilivyo Zanzibar wataalamu wanatwambia katika kipindi cha miaka 50 na 60 inayokuja kina cha maji kitaongezeka sana kwa sababu wenzetu walioendelea viwanda wanaendelea tu kuzalisha hewa ya *Carbon dioxide.* Njia nzuri zaidi ni kuendelea kupanda miti na kuitunza miti ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia. Sasa wakati hayo yote yanatokea duniani bado sisi tuna mawazo ya kwamba tusiendelee kuutunza msitu ule.

Mimi nasema msitu ule ni muhimu sana barabara ni muhimu sana kwa maendeleo ya watu lakini tupime katika haya mawili lipi muhimu. Mimi ukiniuliza sasa tufanyeje. Bado kuna umuhimu sisi kama serikali kuendelea kutumia kifusi na kuitengeneza vizuri. Maana tunaweza kutumia utaalamu huu huu wa kawaida tukahakikisha kwamba barabara hii ikaendelea kupitika vizuri. Na kwa kuwa hili wataalamu wamelikubali mimi nafikiri tuendelee kulifanya hili.

Tatizo ninaloliona moja ya hatari ya kutumia kifusi mara nyingi unapotumia kifusi baada ya mwaka mmoja au miezi sita ikinyesha mvua barabara ile itaharibika tena. Sasa ni jukumu letu kuhakikisha kila baada ya miezi sita au mwaka mmoja kuendelea kuiweka katika hali nzuri ili iendelee kuwahudumia wananchi. Nadhani hii litatusaidia sana katika kuendelea kudumisha msitu ule. Neema aliyotujaalia Mwenyezi Mungu. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Nam. 59**

**Maabara ya Hospitali ya Mnazi mmoja**

**Mhe. Hija Hassan Hija** – Aliuliza:-

Maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni muhimu kwani ndio Hospitali kubwa na ya Rufaa hapa Zanzibar. Maabara hii ndiyo inayotakiwa kuwa kiongozi na mshauri mkuu kwa maabara zote za vituo vya afya vya Serikali na watu binafsi.

(a) Je, Mhe. Waziri Maabara hiyo inazo sifa za kuwa maabara ya Hospitali ya rufaa?

(b) Zipo taarifa kuwa ili maabara hii iweze kufanyakazi zake kwa ufanisi huhitaji zaidi ya Tshs. 5,000,000/= kwa mwezi, lakini kwa sasa huingizwa si zaidi ya Tshs. 1,000,000/= kwa mwezi, jambo linaloifanya maabara hiyo kufanya kazi chini ya uwezo wake. Kwanini Serikali isipitishe uamuzi wa wagonjwa kuchangia huduma za maabara hiyo ili kuiwezesha kufanya kazi zake vyema?

(c) Inasemekana Maabara hiyo kwa sasa inashindwa kufanya vipimo vya "*Blood Culture*" kutokana na ukosefu wa fedha za kununulia madawa *(Reagants).* Hilo ni kweli?

(d) Katika Idara ya *Haematology and Clinical Chemistry* ya Maabara hiyo baadhi ya vifaa vyake vimeharibika kutokana na chumba hicho kuwa na joto kali kutokana na kukosekana kwa *Air Condition (AC).* Je Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja haioni kuwa huo ni udhaifu na aibu mbele ya uso wa Wafadhili na hata mbele yetu sisi wenyewe?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye vifungu (a) , (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni muhimu kwani ndio Maabara ya Hospitali ya rufaa kwa Zanzibar. Ili maabara iwe na sifa ya kuwa maabara ya Hospitali ya rufaa inatakiwa iwe na sifa zifuatazo:-

- Wafanyakazi wa kutosha wenye fani za maabara tofauti;
- Vifaa vya kisasa vyenye kufanya kazi; na
- Upatikanaji wa *reagents*.

Mhe. Spika, Maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kati ya Maabara tano za Tanzania ( Muhimbili, KCMC, Mbeya na Bugando) ambazo zimo katika mchakato wa kupatiwa utambulisho ili ziweze kutambulika kimataifa kwa mujibu wa muongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mhe. Spika, kwa sasa maabara yetu imekuwa ikipokea washauri ambao huja na kufanya kazi nasi ili kuweza kuziba yale mapungufu na hatimae tuweze kutambulika kimataifa. Kwa upande wa vifaa tunavyo vya kisasa licha ya baadhi ya wakati kutokea upungufu wa hapa na pale ambao pia hupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia maabara hiyo imeanzisha mfumo wa wagonjwa *(cost sharing)* huduma za maabara hiyo ili kuiwezesha kazi zake kwa ufanisi zaidi na pindipo ikitokea kuwa mgonjwa ameshindwa kulipia huduma hiyo Idara imeweka mfumo maalum wa kuwasamehe wale wote wasio na uwezo kwa kufuata taratibu zilizowekwa ili kupatiwa huduma.

Mhe. Spika, wizara ya Afya na Ustawi wa jamii kupitia Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, imeshaandaa mikakati ya kutoa huduma za vipimo vya *blood culture* kwa kushirikiana na wafadhili wake jambo ambalo tunalisubiria utekelezaji wake. Hata hivyo kwa sasa maabara ya Hospitali yetu inatoa huduma za "*urine* na *stool culture*.

Mhe. Spika, katika Idara ya *hematology* na *Clinical chemistry* ya maabara hiyo baadhi ya vifaa vyeke viliharibika na ilitokana na tatizo la umeme lililoikumba nchi yetu mwaka jana na kupelekea hospitali kutumia umeme wa jenereta, ambao baadhi ya wakati ulikuwa ukipanda na kushuka, hivyo kupelekea baadhi ya vifaa kuharibika pamoja na hizo *Air Condition*. Lakini kwa sasa vifaa hivyo zinafanya kazi kama kawaida baada ya mafundi wetu kuvifanyia ukarabati.
Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wafanyakazi wa hospitali ya Mnazi Mmoja na Wizara ya Afya kwa jumla kwa mashirikiano yao makubwa na kazi nzuri waliofanya wakati nchi yetu ilipokumbwa na tatizo la umeme kwani huduma zote ziliendelea kama kawaida na kuweza kudhibiti mripuko wa maradhi katika nchi yetu.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa amesemea kwamba sifa za maabara ya rufaa ni kuwa na wafanyakazi wa kutosha, vifaa vya kisasa na upatikanaji wa *reagent*, na kwa kuwa sisi kama kamati tumekwenda na tumeambiwa kwamba maabara hiyo wafanyakazi hawatoshi *reagant* hamna kwa sababu hatufanyi *blood culture*. Atakubaliana na mimi kwamba maabara ile sio ya rufaa;

b) Amesema kwamba kumeanzishwa *cost sharing* kwa wasio na uwezo. Mhe. Spika, wana vigezo gani vya kumjua huyu ana uwezo na huyu hana; na

*c)* Katika maabara hiyo tumeviona vifaa ambavyo vina gharama kubwa zaidi ya milioni 65 vimeharibika kwa sababu ya ukosefu *Air Condition. (AC).* Je, wafadhili wetu wakiona hali hii watatuelewaje.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, laiti kama angeliona mheshimiwa maabara ya Mnazi Mmoja miaka mitatu au miaka minne iliyopita angelijua kwamba kweli hii sasa ni maabara ya rufaa.

Mhe. Spika, kabla sijajibu suala hili miaka minne iliyopita nilipata ujumbe kutoka *Saudi Funds* lakini hawajatusaidia nikawapeleka kwenye maabara ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, walipoiona wakaniambia kwamba Mhe. Waziri bora ya maabara ya skuli kuliko maabara hii ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, sikuhamaki niliona kweli bora maabara ya *Lumumba Collenge* kuliko ya Mnazi Mmoja Hospitali. Lakini sasa hivi kwa ushirikiano mkubwa wa *AICAP* Shirika la Kimarekani, *Colombia University* wametusaidia kuweka vifaa vya kisasa vyenye gharama kubwa, mambo yote sasa hivi yanapatikana Mnazi Mmoja Hospitali. Mhe. Spika, hayo ni mafanikio ya Chama cha Mapinduzi, ni mafanikio ya Rais Amani Abeid Karume.

Mhe. Spika, *AICAP* waliwapa *supplier* wao wametoa fedha wakatuletea *stabilizer* yenye nguvu ndogo, lilipotokezea tatizo la umeme vifaa hivyo viliharibika, lakini hawa *AICAP* kwa sababu tunakwenda vizuri basi wametutengenezea upya vifaa vyote na vinafanya kazi katika hali ya kisasa. Mhe. Spika, ni kwamba wafanyakazi tunao, anayeongoza maabara sasa hivi ana *PhD* Dk. Marijani juzi amerudi *Nairobi University* vijana wanaona raha kufanya kazi Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, *cost sharing* kuiendesha maabara ya Mnazi Mmoja Hospitali kama alivyoambiwa ni milioni 5 kwa mwezi. Mhe. Spika, sisi hatufanyi biashara sisi huwa tunawasaidia wananchi aliyekuwa nacho anatoa, aliyekuwa hana anaambiwa bure. Mhe. Spika, gharama za *cost sharing* kwa mwezi ni asilimia 50 zinapatikana milioni 2, 500,000. Kwa hivyo, kigezo kipo wote waliokuwa hawana uwezo tunawafanyia bure na ushahidi upo na tunasema wazi kwamba yeyote aliyekuwa hana fedha kwa Mnazi Mmoja Hospitali matibabu ni bure.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, jibu la Mhe. Waziri haliridhishi, suala lililokuwa ni kwamba vitu vyote hivyo vilivyoletWa hivyo kweli serikali inashinda kuweka *air condition* ambayo ndio iliyosababisha kuharibika vifaa hivyo. Sio suala la kupigwa siasa hapa, ni suala la kujibu.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, maabara hiyo kuna AC tatu zinafanya kazi zote kilichoharibu ni ile *machine* ya upimaji damu sio AC ni umeme uliokuja ulipanda na kuteremka *stabilizer* ilikuwa na nguvu ndogo na Kamati ya Mhe. Fatma Fereji na Mhe. Said Ali Mbarouk na Mhe. Hija Hassan Hija mimi ndiye niliyewapeleka maabara ile. Mhe. Spika, tatizo sio AC, AC ziko tatu kule ukiingia chumba sasa hivi kinabaridi kuliko hiki hapa.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mengi ya mkazo ambayo Mhe. Waziri ametoa bado nasema kwamba kutokana na jibu mama ambavyo limetolewa kwamba sasa hivi maabara ya Zanzibar ni miongoni mwa maabara ambazo zinatakiwa ziwe za kitaifa na pengine kimataifa.

Mhe. Spika, ni kwamba bado tuna upungufu mkubwa wa wataalamu ni sawa wametokea wafadhili wametusaidia vifaa vipo, lakini nilikuwa napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa upande wa maabara hii ya damu tuna wataalamu wangapi na pia kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu tuliokuwa nao ni wataalamu wangapi hivi sasa wako masomoni kwa ajili ya kuja kufanya kazi hizo za maabara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, suala la wataalamu mpaka sasa hivi tunao wataalamu na wanaendelea na shughuli hizi na kama wako wangapi hilo nitajibu kwa maandishi sina hakika sasa hivi wako wangapi lakini tunao na wanatoa huduma hizo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kuongezea ni kwamba tunao wafadhili wetu hawa wa WHO wao huwa wanakuja hapa mara kwa mara

kuangalia hali ya maabara yetu kuhusu suala la vifaa pamoja na wafanyakazi wetu kwa jumla. Kwa hivyo, mpaka sasa hivi tulichofanya ni kwamba tumetoa orodha ya vifaa na wafanyakazi tunaowahitajia tumeshawapa na wameshatuahidi kwamba watafanya kila namna waweze kutusaidia ili vifaa pamoja na wafanyakazi hao waweze kupatikana.

**Nam. 91**

**Umiliki wa Mali za Shirika la Umeme Zanzibar**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu -** Aliuliza:-

Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) linamiliki mali kadhaa zilizopo *TANESCO* Tanzania Bara kama vile:- Laini (*Line*) ya Ubungo hadi Rasi Kiromoni (132KV), Kituo cha Rasi Kiromoni, na Mnara wa Mawasiliano Kimara. Lakini Shirika halina Hatimiliki za laini hizo. Inasemekana kuwa *ZECO* inakosa hati za kumiliki laini hiyo kwa sababu *TANESCO* inadai kuwa ni mali yake.

(a) Je, Mhe. Waziri ni nini hatma ya miundo mbinu hiyo kwa *ZECO*?

(b) Madai hayo ya *TANESCO* kumiliki miundo mbinu iliyolipiwa na SMZ yana msingi gani wa kisheria?

(c) Kama ipo sheria inayowapa haki ya *TANESCO* ni nini msingi wa uhalali wa Sheria hiyo inayomilikisha mali kwa taasisi ambayo haikuitolea gharama za kuianzisha?

(d) Kwa kuwa *TANESCO* inadai kuwa laini hiyo ni mali yao kwa nini matengenezo yake yalipiwe na *ZECO* kwa mujibu kifungu namba 5 cha Makubaliano ya Ununuzi wa Umeme (*PPA*) ambacho kinaeleza kuwa kinaeleza kuwa *ZECO* italipia gharama zote za matengenezo ya laini kuanzia Ubungo hadi Rasi Kiromoni pamoja na matengenezo ya Kituo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 91 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika kufuatilia hatma ya miundombinu hiyo *ZECO* na *TANESCO* zimekubaliana kumteua mshauri (c*onsultant*) kwa ajili ya kuangalia uhalali wa umiliki wa *ZECO* katika miundombinu hiyo;

Makubaliano haya yamo katika mkataba wa mauziano umeme (*PPA*) baina ya *ZECO* na *TANESCO* uliotiwa saini tarehe 22/04/2010;

(b) Mhe. Spika, madai hayo ya *TANESCO* kumiliki miundombinu ya *ZECO* hayana msingi ya kisheria, bali *TANESCO* inatumia kanuni zake *"General Practice"* ambazo zipo kinyume na kanuni za kitaifa juu ya uhalali wa umiliki wa miundombinu, ambazo hata hazikuzingatia mkataba wa awali wa ununuzi wa umeme baina ya *TANESCO* na *ZECO;*

(c) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika kifungu (b) ni wazi kuwa hakuna msingi wa uhalali wa kisheria. Hili limedhihirika katika majadiliano mbali mbali aliyofanyika baina ya mashirika ya *TANESCO* na *ZECO* wakati wa kujadili mkataba wa ununuzi wa umeme (*PPA*), kwa laini ya pili ya megawati 100 unaogharamiwa na *MCC*. *TANESCO* wameendelea kudai umiliki wa miundombinu hiyo kwa kuhofia kutozwa gharama na *ZECO* kuitumia laini hiyo baina Ubungo hadi Kutuo cha Tegeta tokea ilipohamishwa mita ya *ZECO* hapo Ubungo; na

(d) Mhe. Spika, ni kweli kwamba makubaliano ya ununuzi ya umeme kifungu cha 5 yameeleza wazi kuwa ZECO italipia gharama zote za matengenezo ya laini kuanzia Ubungo hadi Ras Kiromoni pamoja na matengenezo ya kituo. Mhe. Spika, sababu kubwa inayoifanya *TANESCO* kuendelea kudai laini hiyo ni mali yao ilikuwa inahofia kutozwa fidia na *ZECO* kwa kuitumia laini hiyo kutoka Ubungo hadi Tegeta fidia ambayo ni kubwa kuliko gharama za matengenezo waliyoyafanya katika laini hiyo. Pia gharama zinazoitoza mara mbili *ZECO* kwa kuwa *TANESCO* wanasema miundombinu ni yao hivyo haitozingatia kuwa miundombinu hiyo kuwa ni ya *ZECO*.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba laini ya umeme inayotoka Dar es Salaam kuja huku Unguja bado ni ya *TANESCO*. Mhe. Spika, ni kwamba kituo cha Ras Kiromoni kinaharibika sana kwa chumvi kwa sababu kiko karibu na bahari na tulisikia kwamba kituo hicho kitarejeshwa nyuma eneo limeshapatikana.

Je, kazi hiyo imefanywa na kama imefanywa gharama ya kuondosha kituo hicho cha zamani kwenda pahala pengine nani anagharamia *ZECO* ama *TANESCO*?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, ni kweli kituo kile cha Ras Kiromoni kiko karibu kabisa na bahari na mara nyingi unajua maji ya chumvi yanapoleta athari katika vifaa vya aina hii. Mhe. Spika, wazo la kukiondosha kituo hicho kukisogeza nyuma lipo lakini lina gharama kubwa mno na hadi hivi sasa kazi hiyo haijafanyika isipokuwa kinachofanyika hivi sasa ni kuhakikisha kila baada ya muda mfupi kunafanyika usafi kuhakikisha ile chumvi haileti athari ambazo zitakifanya kile kituo kiharibike.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wizara imekiri hapa kutokana na maelezo ya Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna matatizo katika hatimiliki na uelewano wa kisheria katika laini ilioko Tanzania Bara. Lakini hii ni laini ambayo ilifanywa nyuma sana. Mhe. Spika, mimi namuuliza Mhe. Naibu Waziri ni masahihisho gani yaliyofanywa kwa laini hii iliyoungwa juzi iliyokuja Pemba.

Je, utata huu umeondoshwa au bado upo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, hii laini ambayo imetoka kule majani mapana hadi pale pwani ni kwamba laini hii kwa sasa hivi inamilikiwa na *TANESCO*.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu nina suala dogo sana lakini lina umuhimu wake.

Mhe. Spika, tunaamini kwamba suala la umeme unaotoka Tanzania Bara kuja hapa ni kitu muhimu sana na kinataka kusimamiwa vizuri sana, na katika jibu lake Mhe. Naibu Waziri ametwambia kwamba ametafutwa mshauri kwa ajili ya kuweka mambo sawa baina ya *ZECO* na *TANESCO*. Je, kutokana na ushauri huo uliopatikana ni mafanikio gani yamepatikana ili kundoa tatizo hili?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, nimesema tumetafuta mshauri ili tuzungumzie suala hili, shughuli hiyo inaendelea. Lakini nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi na Wajumbe wako wa Baraza hili kwamba *TANESCO* na *ZECO* kwa sasa hivi hatuna *good tuff* kwa hiyo sisi tutaendelea kujitetea kwamba tunao uhalali pamoja na yote hayo lakini sisi tutaendelea kujitetea na nina hakika kwamba tutashinda.

**Nam. 79**

**Ujenzi wa *Jetty* Mwambao wa Bahari**

**Mhe. Ali Denge Makame -** Aliuliza:-

Ujenzi wa *Jetty* unaofanywa na wawekezaji katika sekta ya utalii umekuwa ukileta migogoro baina ya wawekezaji na wananchi na hivi karibuni Ujenzi wa *Jetty* unaofanyika Nungwi Unguja umetatiza maelewano baina ya Mamlaka inayoshughulikia uwekezaji na ile inayosimamia mazingira ya bahari – Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini.

(a) Serikali ina sera gani juu ya ujenzi wa *jetty* za aina hiyo.
(b) Je, kuna utafiti gani ulifanyika ili kubaini ujenzi salama wa jetty katika maeneo ya mwambao na nini matokeo ya utafiti huo.
(c) Je, huo ujenzi unaofanyika Nungwi unakasoro gani zinazoweza kuleta madhara kimazingira.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 79 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Sera ya Serikali juu ya ujenzi wa aina yoyote inaelekeza mazingatio juu ya utunzaji wa mazingira, na hayo yamewekewa masharti katika sheria Nam. 2/79 ya kusimamia mazingira endelevu ya bahari na nchi kavu. Hivyo katika kusimamia ujenzi kwa miradi ya uwekezaji linayoidhinishwa na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi maelekezo ya Idara ya Mazingira yanayozingatiwa na mpaka sasa hakuna taarifa ya tatizo la maelewano baina ya taasisi hizo mbili. Maelewano yenye dalili ya utata yanajitokeza baina ya Idara ya Mazingira na Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Idara hizo ambazo zote ziko chini ya Wizara ya Kilimo ndizo zinazopaswa kushirikiana na kutoa maelekezo kwa pamoja.

Tofauti ya maelekezo ya idara hizo, wakati mwingine, hupelekea utata wa maelewano. Hata hivyo, kwa masuala ya mazingira ya baharini na nchi kavu sheria ya mazingira lazima izingatiwe.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa ya kufanyika kwa utafiti wa ujenzi salama wa jetty. Wakati wa ujenzi huo Kamati ya Wataalamu inayojumuisha wahandisi wa ujenzi wa *jetty*, hushirikishwa ili kuhakikisha ujenzi huo ni salama kwa maisha ya watu. Aidha, Idara ya Mazingira ndio inayotoa ruhusa ya ujenzi wa jetty hizo, baada ya kuridhika kuwa usalama wa mazingira umezingatiwa; na

(c) Mhe. Spika, wasimamizi wa ujenzi huo kama nilivyoeleza awali, hawajaeleza kasoro za kimazingira zenye athari katika ujenzi wa Gati ya Nungwi. Aidha, usimamizi uunahusisha ukaguzi wa kila mara na endapo itabainika kuwepo kwa kasoro wakati ujenzi unaendelea, hatua za kukinga kasoro hizo huwa zinachukuliwa na kuelekezwa na Idara ya Mazingira.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amezungumza suala la ujenzi wa jetty hii kwamba wamekaa pamoja na Idara ya Mazingira. Mhe. Spika, ni kwamba sasa kuna matatizo ambayo yamejitokeza kwa waongozaji meli kwamba wanapata usumbufu. Mhe. Spika, mara nyingi jetty na mnara uliokuwepo Nungwi muangaza wao wa taa wanapoonesha wenye meli huwa wanababaika kujua kwamba ni mnara au ni jetty. Kwa hivyo, kulingana na usumbufu huo meli ambazo zinapita katika bahari hii na kuingia hapa huwa zinapata usumbufu huo.

a) Je, Mhe. Waziri kama litatokea la kutokea ataiambia nini serikali au wanaongoza meli wanaopita katika njia hizo?

b) Mhe. Spika, kwa wana vijiji wa Tumbatu hadi Nungwi pindipo meli zinazopita katika maeneo yale zimepotoza muelekeo kuingia katika biashara zao za mwani amewahamasisha nini kujikinga kama yakitokezea hayo?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, nilisema ujenzi wa jetty unasimamiwa na kamati maalum iliyoundwa, kamati hii inahusisha wahandisi wa ujenzi wa jetty, Idara ya Ardhi, Idara ya Mazingira, *ZIPA*, Idara ya Majenzi na Bandari wenyewe. Kwa hivyo, wakati wa ujengaji wa jetty hizi tahadhari zote huwa zinachukuliwa kwa sababu wataalamu wa maeneo yote wanakuwemo katika hiyo kamati.

Mhe. Spika, sitaki kuamini kwamba kweli jetty inaweza ikaingiana na mnara na ikapoteza mwelekeo wa meli kwa sababu urefu wa jetty na urefu wa mnara ni tofauti. Mhe. Spika, ni kwamba muongozaji wa meli anakuwa anakuwa anaangalia taa ya mnara na haangalii mataa ya jetty. Kwa hivyo, niseme kwamba tahadhari zote huwa zinachukuliwa.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri katika ujenzi wa jetty zinajengwa kuanzia ufukweni mpaka kwenye maji ya bahari, lakini uwezekaji unatakiwa uwe kama mita 30 kuanzia kwenye ufukwe.

a) Je, ujenzi huu wa *jetty* unafuata sheria gani mpaka ukawa ufanywe kuanzia ufukweni kuendea kwenye maji ya bahari?

b) Wananchi panapojengwa jetty huzuia kupita au kuvua je, hiyo ni katika miongoni mwa sheria au wawekezaji wanajichukulia hatua mikononi mwao?

c) Wananchi wanapata faida gani baada ya eneo lao la bahari kujengwa jetty?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna sheria inayosema wawekezaji wanatakiwa kujenga mita 30 kutoka ufukweni kwenda juu. Mhe. Spika, suala la *jetty* halimo kwenye sheria ya uwekezaji, lakini kuna kanuni zinazoruhusu ujenzi wa *jetty* na ruhusa imetolewa na Idara ya Mazingira na yeyote anayeruhusiwa kujenga *jetty* kuelekea pwani inakuwa ni mradi mwengine na unalipiwa malipo yake tofauti.

Mhe. Spika, pia kama tulivyomsikia Waziri wa Fedha wakati anazungumzia bajeti ya mwaka huu kwamba serikali sasa itatoza kodi maalum kwa ajili ya *jetty.*

Mhe. Spika, ni kwamba wananchi hawazuiliwi kusogea katika maeneo ya *jetty*, lakini kwa muundo wa *jetty* ulivyo wananchi hawawezi kufanya kazi zao katika eneo hili. Kwa hivyo, sio kwamba wanazuiliwa lakini wenyewe hawezi kazi zao kutokana na muundo na mjengo wa hiyo jetty yenyewe.

Mhe. Spika, faida inayopatikana moja kwa moja kwa wananchi baadhi yao ambao wana elimu kutoka katika eneo lile wanaweza wakawa wanafanya kazi za ujenzi au kuhudumia ndani ya *jetty* na faida nyengine ni kwa serikali yao kupata mapato kutokana na ujenzi wa jetty.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake baada ya hapo naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama nafahamu vizuri kwamba wakati wa kujibu alisema kwamba hakuna utata baina ya Idara ya Mazingira na ujenzi wa *jetty*. Mhe. Spika, kwa ninavyofahamu mimi kwamba mazingira ni suala la kitaifa na mataifa yanajitahidi sana kuleta miradi Afrika ili kuondoa uharibifu wa mazingira na moja katika miradi hiyo ni *MACEMP* kwamba mazingira yanahifadhiwa yasiharibike. Hivyo, Mhe. Spika, kuruhusu kujengwa *jetty* maana yake si unamkomoa Waziri wa Kilimo kwamba watakapokuja wakaguzi wa jumuiya hizo wamuadhirishe.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba *jetty* ni mradi mmoja wapo kama alivyosema Waziri wa Fedha na Uchumi lakini ni mradi ambao unakataliwa na

Wazanzibari wenyewe, hivyo hakuna vianzio vyengine tukafutilia mbali miradi ya *jetty* kwa sababu inawakera sana wale walioko katika mazingira ya pwani.

Mhe. Spika, hakuna suala la kumkomoa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira au Sekta ya Kilimo. Kwa sababu kama nilivyosema ujenzi wa *jet* unasimamiwa na kamati na Idara ya Mazingira ndio inayotoa masharti ya ujengaji wa *jet* hiyo. Idara ya Mazingira imo ndani ya Wizara ya Kilimo, Mradi wa *MACEMP* umo ndani ya Wizara ya Kilimo. Kama nilivyosema mwanzo tahadhari zote huwa zinachukuliwa za kimazingira.

Mhe. Spika, sina ushahidi wa wananchi kukataa *jet* zinazojengwa mahotelini. Kilichojitokeza ni kwamba, hasa kwa *jet* ya Nungwi, ni kwamba kulikuwa na mvutano wa makundi, kundi la wavuvi na kundi la Kamati ya Maendeleo pale katika Kijiji cha Nungwi. Kwa hivyo, kilichojitokeza ugomvi haukuja kwa sababu ya *jet*, ugomvi ulikuja kwa sababu ya pahala, wavuvi wanasema ni dago lao, Kamati ya Maendeleo wametoa ruhusa pajengwe. Lakini si kuikataa *jet* yenyewe kama *jet* kujengwa pale. Ahsante.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 – Afisi ya Waziri Kiongozi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na tunakusudia tumalize michango kwa Afisi ya Waziri Kiongozi asubuhi hii na jioni moja kwa moja tumwite Mhe. Waziri Kiongozi kufanya majumuisho. Sasa wajumbe ambao bado hawajachangia ni wengi, hawapungui 20. Kwa hivyo, itabidi tukasimu muda kwa kupunguza kidogo ili wachangiaji wengi wapate nafasi. Niwaombe basi tuchangie kwa muda wa dakika 20, 20 ili tupate wajumbe wengi zaidi.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazrui:** *Bismillahi Rahmani Rahim*. Kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo siku ya Ijumaa tukawa hai, salama, wazima na wenye furaha kama hivi tulivyo.

Pili, nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa siku hii ya leo. Ahsante sana.

Aidha, namshukuru Mhe. Waziri Kiongozi na nampongeza sana kwa hotuba yake aliyoitoa na kwa kweli imezingatia mambo yote yaliyokuwa muhimu ya sisi kuweza kuchangia katika bajeti hii.

Mhe. Waziri Kiongozi umahiri wake wa kuongoza wizara hii kwa muda wa miaka kumi, umeonesha dhahiri kwamba Mhe. Rais hakukuteuwa kuwa Waziri Kiongozi kwa kubahatisha, ila alitumia vigezo halisi na kwamba kazi hiyo ameitimiza kwa juhudi kubwa na matumaini makubwa kabisa. Anastahili sifa kwamba ni kiongozi wa kwanza ambaye alichukua wadhifa huu akiwa na umri mdogo kabisa na vile vile kuwa kiongozi wa kwanza aliyechukua muda mrefu kwa muda wa miaka kumi kuwa katika afisi hiyo.

Tunakuombea kila la kheri na tunakupongeza sana kwa utendaji wako wa kazi kwa muda wa miaka kumi iliyopita. Lakini basi, Mhe. Waziri Kiongozi utakumbuka ulipoanza kazi katika Baraza hili hali ya hewa ilivyokuwa na sasa hivi *Alhamdulillah* hali ya hewa ilivyo.

Mhe. Spika, hali ya hewa sasa hivi ni nzuri kwa hivyo, maisha tunaangalia hatima inakuwajue. Kwa hivyo, hatima inaonesha *Alhamdulillah* nzuri. Matumaini yetu kwamba hatima hii itaendelea kuwa nzuri mpaka pale utakapomalizika muda wa miaka kumi kama yeye Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vile vile Kiongozi Mkuu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda kunukuu ukurasa wa 5 na 6 ambao Mhe. Waziri Kiongozi ametia katika hotuba yake.

Ukarasa wa 6 *Item No. 8* inasema,

> "Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010, nchi yetu inatarajia kufanya Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2010. Narudia kutoa wito kwamba vyama vya siasa, wanachama na wananchi wote wadumishe umoja na amani wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi ili nchi yetu iendelee kuwa ni nchi ya amani. Nawaomba sana viongozi wa vyama vya siasa vitakavyoshiriki katika uchaguzi huo, vishirikiane na Tume ya Uchaguzi ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki".

Mhe. Spika, hii ndio nukuu yangu, nilipozungumza kwamba ukurasa wa sita Mhe. Waziri Kiongozi ametueleza hayo.

Ukienda ukurasa wa 33 na 34, nitanukuu 34 kifungu cha 47.

"Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 tume ilitekeleza majukumu yafuatayo: kuendeleza daftari la kudumu la wapiga kura kwa kuandikisha wapiga kura

408,267 na angalia kiambatanisho Nam. 6" Hapa ndipo nitakapoanza kuchangia Mhe. Spika, kwenye suala la Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi imefanya kazi yake ambayo imepewa kikatiba na imepewa mamlaka hayo ya kuweza kutayarisha daftari la kupiga kura kwa ajili ya kujitayarisha na uchaguzi wa mwaka 2010. Vile vile kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Waziri Kiongozi katika hotuba yake kutakuwa na kura ya maoni mwaka huu wa 2010. Azma ni kwamba kila Mzanzibari ambaye anastahiki kupiga kura anapata fursa hiyo bila ya kunyanyaswa na kunyimwa haki yake.

Mhe. Spika, haki ya Mzanzibari imo katika katiba, katika sheria na vile vile anayemnyima haki yake Mzanzibari kupiga kura basi pia ana hatia na adhabu yake imo katika sheria. Sasa basi, tunasema kwamba uandikishaji umefanywa na tume *Alhamdulillah* mpaka sasa hivi umemalizika. Sasa hivi watu wote wanaangalia majina yao ili kuona kwamba yamo au hayamo na kupinga wale ambao wana matatizo.

Lakini uandikishaji huu Mhe. Spika, uko *very questionable*. Kwa sbaabu hiyo ndio nikaona nitoe indhari mapema ili yale malengo ambayo Mhe. Waziri Kiongozi ameyaeleza katika hotuba yake yatimie.

Mhe. Spika, mwaka 1995 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilisajili wapiga kura 348,934. Katika sensa iliyofanywa mwaka 2002 Wazanzibari *population* yao ilikuwa ni 984,625. kwa tegemeo la ukuaji wa asilimia 3 kila mwaka. Tunatarajia sasa hivi mwaka 2010 tuna Wazanzibari 1,257,000 na ushei wa madhumuni ya sensa hio hio iliona kwamba ifikapo mwaka 2010 kutakuwa na watu hao na kwa takwimu inajulikana wazi kwamba, katika nchi asilimia 48 ya population huwa ni watu ambao wameshafikia umri wa miaka 18.

Kwa hivyo, ukichukua *population* ambayo imekisiwa na sensa ya mwaka 20020 utagundua kuwa Wazanzibari ambao walikuwa wapewe *ZEN ID* walikuwa ni 603,367. Wazanzibari ambao wasajiliwe kwa ajili ya kupiga kura wawe 603,367, hatuangalii hali halisi ilivyokwenda.

Kwa mujibu wa ripoti ya mtoa vitambulisho waliyopewa *ZEN ID* ni watu 550,415, hapa inaonekana nakisi ya watu 52,952. Walioandikishwa katika kupiga kura ni watu 408,536 utaona hapa pana nakisi ya 141,879. hapo tayari utaona kwamba una masuala mengi ya kujiuliza kutokana na hizi data ambao tulizipata kutoka *ZEN ID* na kutoka kwa *ZEC*.

Niache hapo nije katika uchaguzi wa mwaka 1995. Uchaguzi wa mwaka 1995 waliojiandikisha ni 348,934 ambapo sasa hivi wameandikishwa ni 406,536.

Kwa hivyo, hapo tayari utakuta ukiangalia mwaka 1995 mpaka leo mwaka 2010 waliozidi katika buku hili ni watu 59 elfu tu. Hili linashangaza sana, kwa wale watafiti wa *data.* Watu wa takwimu wanapata hofu kubwa sana kuhusu daftari letu. Ningemuomba Mhe. Waziri Kiongozi atufafanulie masuala haya ili aweke wazi wananchi wote na wale wahakiki wa data waweze kuondokewa na wasi wasi wao.

Uchaguzi wa mwaka 2005 Mhe. Spika, waliojiandikisha walikuwa ni 507,225. Kwa hivyo, uchaguzi wa mwaka huu waliojiandikisha mpaka sasa hivi ni 408,536 utakuta hapa pana nakisi ya watu 94,689. Hali hiyo inazidi zaidi na zaidi kutia shaka juu ya suala la daftari letu ambalo tunakwenda kupigia kura na ambalo Mhe. Waziri Kiongozi anatoa kila aina ya indhari kuona uchaguzi huu utakuwa huru na wa haki. Lakini moyo wa uchaguzi huu ni daftari letu.

Tuangalie kwa mfano, tuchukue Jimbo la Donge. Jimbo hilo walioandikishwa mwaka 1995 ni watu 11,634, waliopiga kura ni 11,390. Sasa kwa mujibu wa sensa watu kama elfu kumi wanastahiki kupewa *ZEN ID* na wanastahiki kuandikishwa kupiga kura.

Tuache ya sensa. Kwa mujibu wa ripoti ya mtoa *ZEN ID* anasema kwamba, ametoa *ZEN ID* 12,831 katika Jimbo la Donge, lakini basi jimbo hilo hilo walioandikishwa mwaka huu ni 7,958. Nakisi kubwa iko baina ya mwaka 1995, naamini kuma Donge hakujatokea magwa, hakujatokea kolera, hakujatokea msukosuko wa kufa watu wote elfu 3 au 4 kwa mpigo. Na naamini kwamba watu wa Donge hawajasimama kuzaa, wanazaa na watoto wanakua kwa hivyo, idadi inaonesha kwamba kuna watu 2,256 wenye *ZEN ID* hawajaandikishwa katika daftari hilo.

La kushangaza Mhe. Spika, ni tofauti baina ya mwaka 1995 na mwaka 2010 karibu watu elfu 5 hawakuandikishwa katika daftari hili. Mambo haya lazima yachambuliwe, yaelezwe, ili wananchi na wadadisi wa mambo watokane na shaka ya daftari letu ambalo tunataka kupigia kura mbili muhimu, kura ya maoni na kura ya kuchagua serikali kama itakuwa ya Umoja wa Kitaifa Inshaallah ili isiwe na utata wala *contradiction* au *controversies.*

Majimbo yote yana matatizo lakini tuchukue Jimbo la Uzini. Jimbo hili mwaka 2005 walioandikishwa kupiga kura ni watu 14,214, waliokisiwa mwaka 2010 watakuwa 15,723, waliojitokeza kuandikishwa ni 8,756. Kwa hivyo, kuna nakisi ya 4,345.

Koani mwaka 2005 walioandikishwa ni watu 15,639, wakatarajiwa mwaka huu wataandikishwa watu 17,437, badala yake wameandikishwa watu 12,082 kuna nakisi ya watu 3,557.

Mjimkongwe mwaka 2005 waliandikishwa watu 13,858, wakatarajiwa mwaka huu wataandikishwa watu 15,125, waliojitokeza mwaka 2010 wameandikishwa watu 7,409 tu, watu 6,449 hawapo. Siamini kwamba pametokea vifo vya watu wote hao au watu hawa hawazai au hawakui.

Kikwajuni mwaka 2005 walioandikishwa watu 11,918, na mwaka huu walitarajiwa watu 13,050, lakini waliojiandikisha mwaka huu ni 7,802, kwa hivyo, kuna nakisi ya watu 4,116.

Mhe. Spika, majimbo yote ningeorodhesha wangeona ipo nakisi kubwa, lakini nimechukua yale majimbo ambayo nimeona yako *notorious* kabisa. Kwa hivyo, tatizo Mhe. Spika, lipo na ningeomba Mhe. Waziri Kiongozi alishughulikie kwa udhati wa moyo wake na kwa nia yake njema naamini kwamba mambo haya ataweza kuyaweka sawa.

Mhe. Spika, jengine katika sheria ya uchaguzi watu wote watakaosajiliwa katika buku hili wawe na kadi ya *ZEN ID.* La kusikitisha kuna watu wengi wamekwenda katika vituo vya kujiandikisha wamepanga mistari mirefu, wamekaa siku mbili mpaka tatu katika mistari hiyo kutaka waandikishwe, wakiwa na haki kamili ya kuandikishwa na *ID* zao mikononi. Lakini kwa bahati mbaya hawakuandikishwa na ni wengi wafikao elfu 20.

Nikitoa mfano nina majina ya watu 155 ambao wamekwenda katika Shehia ya Mombasa, katika shehia hiyo sheha pale ni mwanamke akapiga matakuro yake watu 155 hawakuandikishwa ambao wana *ZEN ID* mikononi mwao. Wakarejeshwa wakanyimwa haki yao, kwa kuwa sheha wa shehia ile amekataa na tume haikuwa na hata la kusema wakaondoka watu wale bila ya kuandikishwa.

Ukiangalia ikiwa Shehia moja tu ya Mombasa bibi sheha kakataa watu 155 ambao wana haki kamili ya kuandikishwa. Je, shehia zote za Unguja na Pemba watu wangapi hawakuandikishwa kwa misingi kama hiyo? Mhe. Spika, naomba sana tuliangalie suala hili na tupatiwe ufumbuzi.

Katika daftari hili kuna vijana tele wadogo wadogo ambao hawajafikia umri wa miaka 18 kama, wameandikishwa, wamepewa *ZEN ID.* Hawa ni wengi ni *school boys and school girls,* hii ni aibu ya kujifedhehesha. Tunataka tufanye mambo kwa uadilifu.

Mhe. Spika, kuna watu ambao si raia wa Tanzania ni raia wa Msumbiji ambao wanapiga kura katika nchi yao na ushahidi ni huu hapa. Huyu ni mtu wa Msumbiji hii ni kadi yake anayepiga kura kwa ajili ya kumchagua Rais wa

Msumbiji na sasa hivi anataka kutuchagulia Rais wa Zanzibar. Huyu pia kaandikishwa na si peke yake ni wengi.

Mhe. Spika, kuna watu ambao wameandikishwa katika Jimbo la Tumbatu hao hao wakatoka wakenda katika Jimbo la Donge. Majina tunayo na watapingwa katika daftari hili hili tuone tume itachukua hatua gani ya kuwaondoa katika jimbo moja na wakawabakisha katika jimbo moja. Majina tunayo na tumeshaya-*mark* tunangojea tume itachukua hatua gani kuwafuta katika jimbo moja. Huo ni mfano wa jimbo moja lakini hata Bumbwini hivyo hivyo.

Kwa hivyo, ningependa kauli ya Mhe. Waziri Kiongozi itekelezwe kivitendo na sio kimaneno. Mhe. Spika, Tume yetu ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria yake inatakiwa tume hiyo iwe *independent* isiingiliwe na mtu yeyote wala taasisi yoyote. Yaliyojitokeza hapa kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar haiku *independent*, inategemea sana sana na programu ya *ZEN ID*. Yaani tume yetu imeshindwa kufanya kazi, haifanyi kazi yoyote isipokuwa programu yake ya kompyuta itoke *ZEN ID* iingie katika *ZEC*. Hii ni *weakness* kubwa sana inayonyima uhuru wa tume hii na kuonekana tume hii haiko huru, tume hii iko *under control* ya Idara ya Vitambulisho.

Kwa kweli hii ni kwenda kinyume na sheria ya kuanzishwa kwa *ZEC*. *ZEC* ni kitu peke yake kijitegemee na bila ya kuingiliwa, lakini *ZEC* imeshindwa inafanya kazi chini ya usimamizi na kuchukua *data* na kila *information* inatoka kwenye *ZEN ID*. Kwa hivyo, ikiwa *ZEN ID* wanakosea na wao wanakosea, sasa imekuwa *data garbage in, garbage out.* Hakuna *any differences* baina ya *ZEN ID* na *ZEC*. Hili ni kosa, ni tatizo nahisi litatuliwe.

Mhe. Spika, ningeomba masuala haya ya tume yawekwe sawa, tume iwe *independent* isiingiliwe kabisa na Idara ya Vitambulisho. Kuingiliana katika kiprogramu na mambo mengine inaonesha *ZEC* haina meno wala haiwezi kufanya kazi zake peke yake bila ya kusaidiwa na Idara ya Vitambulisho.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza masuala ya tume ningeomba Mhe. Waziri Kiongozi alishughulikie suala hili ili hatima yake ya miaka 10 akiwa kiongozi mahiri kabisa, aliyefanya kazi nzuri, akaja akafelishwa na Tume ya Uchaguzi ambayo imepewa madaraka ya kutoa matokeo mazuri ambayo yataandaa Zanzibar mpya ambayo haina utata.

Nikiendelea mbele niingie katika ukurasa wa 31 ambao Mhe. Waziri Kiongozi katika bajeti yake ya mwaka jana alisema katika ukurasa wa 31 sehemu ya tano, kutakuwa na kusimamia na ujenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi, Mbweni.

Mhe. Spika, Baraza lilioko Mbweni maelezo tumeyapata na tumeridhika. Lakini nina wasi wasi kwamba katika bajeti yake hii je, hili jengo ametia gharama za kutosha za kuweza kulienzi jengo lile? Jengo lile sio kama jengo hili tulilonalo sasa, matumizi yake ni mara kumi zaidi ya jengo hili hapa, ya umeme, kama ni jenereta mafuta, kama ni bustani, *whatever*.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri Kiongozi namkumbusha kwamba jengo lile gharama zake ni kubwa zaidi na kwa bajeti yake ilikuwa izidi kuliko bajeti ya mwaka jana. Kwa sababu mambo ya kule ni makubwa zaidi, gharama ni kubwa. Hili namuomba Mhe. Waziri Kiongozi alitie katika mantiki yake.

Jengine ukurasa huo huo alisema mwaka jana kwamba kusimamia ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Mhe. Spika. Ujenzi huu bahati mbaya na mwaka huu umekuja tena vile vile kwamba kutakuwa na kusimamia ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Spika. Hatujajua katika bajeti ya mwaka jana kulifanyika nini katika ujenzi wa nyumba hiyo, nyumba hiyo imeshaanza kujengwa, imefikia wapi.

Kwa sababu heshima ya Baraza hili ni kwamba tuone Mhe. Spika, anapata makaazi yenye heshima ya kuwa Spika, Mhe. Spika, anapata kila aina ya *service* ambayo anastahiki kupata na moja wapo ni nyumba. Sasa naona hapa hatujapata maelezo ya kutosha kwamba nyumba hii imejengwa au itajengwa au vipi.

Jengine Mhe. Spika, hata Mkuu wetu wa Upinzani mpaka leo imeshindikana kupatiwa gari. Mhe. Waziri Kiongozi hakueleza hapa katika hotuba yake, ni kitu gani kinachopelekea serikali yetu kushindwa kumpatia Mkuu wa Upinzani usafiri na kuonesha hali halisi ya kwamba nchi hii ni nchi ya utawala wa vyama vingi. Sheria hii tunaiheshimu na heshima yake iko wapi.

Mhe. Spika, nikiendelea nakwenda katika ukurasa wa 53 kuhusu suala la shughuli za watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, suala hili ni suala muhimu sana, limezungumzwa sana. mimi nataka kutilia mkazo tu kwamba, suala hili naona bado kabisa halijapewa umuhimu wake. Shilingi 225 milioni ni pesa kidogo sana kabisa kwa ahadi hii ya katika shughulki zao watu wenye ulemavu. Kwa sababu kwa muda mrefu watu hawa walikuwa hawakufanyiwa *service* wanazozitaka.

Hata hivyo, bado asilimia 30 tu ya makadirio ndio iliyotumika, nahisi hatukuwatendea haki na kwa kweli katika mwaka unaokuja bajeti hiyo imepunguzwa. Mimi nilitarajia bajeti hii itaongezwa lakini imepunguzwa, kutoka shilingi 225 milioni mpaka kufikia shilingi 211 milioni. Nasema kwamba, jamani tusifanye masihara, hawa wenzetu walemavu ndio

tunatarajiwa sisi tuwaangalie, wengi waangalie haki za wachache, tukianza kuwa wengi tukawadhulumu wachache basi nchi yetu itakuwa haipati hata baraka. Tuhakikishe kwamba hawa wachache tunawahudumia na kwa kuwa ulemavu si jambo la mchezo, mtu yeyote, wakati wowote anaweza akawa mlemavu.

Mhe. Spika, siku moja nilijiwa na Umoja wa Ugonjwa wa Akili, walikuja nyumbani wakanambia tumekufuata bwana tunataka wewe uwe mshikafedha wetu. Nikasema he, niwe mshikafedha wenu! Mimi sitaki. Wakasema unakataa? Nikawambia ninakataa sitaki kuwa mshikafedha wenu. Sisi tuna umoja huu tunataka wewe uwe mshikafedha wetu. Nikawaambia aa, nendeni zenu sitaki. Nikaona hawa bwana wagonjwa wa akili, mimi niwe mshikafedha wao, fedha ikipotea si watakuja kunila bwana, nikasema sitaki.

Sasa wanaondoka pale nikafikiri, nikasema mimi nawakatalia hawa kesho nikija nikiwa mwendawazimu Mwenyezi Mungu aninusuru, ndugu yangu, mtu wangu, mimi nitawaambia nini wale watu. Nikawaida njoni, hebu nambieni tena mnasemaje? Wakasema tunataka uwe mshikafedha wetu sisi katika jumuia yetu. Nikawaambia nimekubali sawa. Wakanambia basi njoo kwenye kikao chetu nikaenda tukakutana, wakanichagua nikawa mshikafedha wao, nikawa *member* na mimi wa umoja ule.

Kwa sababu gani? Nilifikiria mustakabala, leo mzima nina akili timamu kesho sijijui nitakuwa vipi, leo nawakatalia wale nitakwenda kuwafanya nini? Na yale niliyoyakataa yalinifika. Nimekwenda kule napima lile jengo lao kutafuta misaada kutoka *DANIDA* nafanya makisio ya jengo lile, nikakuta jamaa pale nilikuwa nina ndevu nyingi hivi, wakanivamia wale. Aa Maalim Seif Sharifu, wakanivamia, wakanibana kisawasawa sifurukuti, maana yake kutaka kunitoa choo hasa, nikawambia wale ma-*nurse* nyinyi mnaona hali hii, wakasema fanya hivyo hivyo tu wewe usitumie nguvu, ukitumia nguvu watakumaliza. *(Kicheko)*

Kwa hivyo, nimejikubalisha mimi kwenda kuwa mshikafedha wa umoja ule na kwa kweli yale niliyofikiria yatanifika yalinifika kweli, lakini inabidi uvumilie. Kwa sababu wewe ni binadamu hujijui lini utakwenda katika matatizo kama yale.

Hivyo, nasema kwamba Mhe. Waziri Kiongozi tuhakikishe kwamba walemavu tunawapatia kila aina ya msaada. Tuwasaidie sana jamani na tusiwatie katika semina tu basi aah, tuwapatie fedha za kufanyia ujasiriamali.

Mimi nimekwenda kule Spain njiani kuna vibanda vibanda, vizuri tu vya *round* vimewekwa, upande huu na upande huu katika mji wote ule kati kati baina ya njia na njia kando kando vimewekwa vibanda vile. Vibanda hivi kila anayeuza

unamkuta mlemavu, nikaambiwa ndio, walemavu wote hapa ndipo wanapouza magazeti, kuuza vitu vidogo vidogo, mtu mwengine yeyote haruhusiwi kuuza katika maeneo haya isipokuwa hawa tu wanasaidiwa ili wapate kuwezesha maisha yao.

Walemavu wana watoto, wana familia, majukumu, uwezo wao ni mdogo. Kwa hivyo, hapa Spain walemavu wanapewa elimu kwa wingi, yaani walemavu wengi wana *PhD, degree*, kwa hivyo, wanaangaliwa kwamba kila mlemavu awe na elimu ya juu kabisa. Vile vile aliyekuwa hana elimu anapatiwa ujasiriamali, anapewa *entrepreneur*.

Mhe. Spika, namshauri Mhe. Waziri Kiongozi kwamba walemavu wote wenye uwezo wa kusoma wasomeshwe wawe na elimu ya juu ili waweze kumudu maisha yao.

La pili walemavu wote ambao hawana uwezo wa kuparamia juu wapewe utaalamu pamoja na pesa ya mbegu ili waweze kuanzisha miradi yao wawe entrepreneur wazuri kabisa.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nampongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi kuhusu suala la *TASAF* ambayo imeonesha mafanikio makubwa sana *Alhamdulillahi*. Ingawa watu wananung'unika kwamba kuna kuchelewa sana kupita miradi kwa sababu ile njia ya kupitisha miradi inakuwa ndefu sana. Kwa hivyo, naamini kwamba katika awamu ya pili hii watafanya ile *analysis* kuona kwa nini inachelewa ili ule urasimu upungue wananchi wapate mambo haya kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, mafanikio yanapatikana lakini inachukua muda mrefu na kwa hali hiyo yanakuwa yanaleta maudhi kidogo. Kwa hivyo, naamini katika awamu inayofuata idara yake itaangalia namna gani ya kuweza kufupisha masuala ya kupoteza muda kwa sababu muda ni pesa na hawa wamo katika miradi.

Mhe. Spika, jengine ningemshauri Mhe. Waziri Kiongozi kweli kaingia katika mambo mengi kupanda miti, mambo ya miradi ya kukarabati, miradi ya mikoko, kuku wa mayai. Lakini nahisi kwamba vile vile ipo haja ya kuingia katika suala la ujasiriamali. Ningemuomba Mhe. Waziri Kiongozi aanzishe kwa makusudi hasa awaoneshe Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji mfano kwamba tuanzishe kitengo cha *manufacturing* cha kuanza viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Spika, kiwanda cha kutengeneza vifungo vya shati, makoti na nguo hakifiki dola elfu moja, kiwanda cha kufanya *office pin* hakifiki dola elfu moja. Lakini sisi hapa Unguja vifungo tunaagizia, *office pin* tunaagizia, bahasha ya

barua kiwanda chake hakifiki dola elfu moja lakini tunaagizia. Ile *clip* ya ofisini mashine yake ya kufanyia *clips* haifiki dola elfu moja tunaagizia.

Hivi ni viwanda vidogo vidogo ambavyo tunaweza kuwapa watu wetu wakawa wajasiriamali wakaweza kuanza hiyo sekta ya manufacturing na ikaweza kuondosha yale mambo madogo madogo ya kuagizia. Tunaagiza mpaka pini, *toothpick*, vifungo haiwezekani.

Mhe. Spika, baada ya hayo nikushukuru sana na kumuombea kila la kheri Mhe. Waziri Kiongozi kwamba mambo haya atayazingatia na atayafanyia kazi ili hatima yake iwe njema. Mhe. Spika, jina lake Mhe. Waziri Kiongozi ni Shamsi, kwa Kiarabu shamsi ni jua, ukiambiwa *anta shamsi* maana yake ni mtu wa manufaa, maana yake jua lina manufaa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri Kiongozi jina lako liende sambamba na vitendo vyako. *(Makofi)*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru na wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii leo asubuhi kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, naomba nafasi ya pekee na mimi nisiwe mwizi wa fadhila kwa wenzangu wote kila anayesimama hutoa dua kubwa sana kwa Mhe. Waziri Kiongozi. Kwa hivyo, naomba na mimi nitoe dua yangu na sisi ni masharifu wa Tunduni itapanda.

Mhe. Spika, nimeangalia kitabu hiki chote na kila anayesimama anasema uzuri na ubaya wake ndani. Lakini mimi nasema katika kuongoza mimi siku zote huwa najiuliza, hivi kweli mimi nifike umri wa miaka mia ndio nitaweza kuongoza, kumbe kuongoza hakutaki umri mkubwa. Tukiangalia mimi na Mhe. Waziri Kiongozi basi mkubwa mimi lakini ametuongoza vizuri sana. Ni haki yake kabisa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri ili aendelee kutuongoza. Ukweli uko wazi Mhe. Spika, lazima tuseme na wala tusifiche. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nina ushahidi kwa Mhe. Waziri Kiongozi kutokana na utekelezaji wake. Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi ukimwambia, ukipiga kelele tu kwenye vyombo vya habari, wananchi akiwaona tu kuna tatizo moja basi siku ya pili kishaingia bila ya taarifa. Hiyo ndio sifa moja ya kiongozi.
Mhe. Spika, sifa ya pili kuna miradi mingi tuliyomkusanyia humu ndani sijamsikia kufanya ubadhirifu hata mmoja pamoja na watendaji. Hii ndio sifa Mhe. Spika, kwa nini tusimpe.

Mhe. Spika, nikiingia katika kitabu ukurasa wa 9 nizungumzie mambo ya mfumko wa bei. Mhe. Spika, namuomba hasa Mhe. Waziri Kiongozi hebu akae aendeleze yale ambayo tunayomsifu. Hili suala la mfumko wa bei akae kwa

kina kabisa aangalie ni tatizo gani ambalo linasababisha kupanda kwa bei. Kila siku tunasikia pembe linapanda, unga unapanda, mafuta yanapanda na mambo chungu nzima.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi alikalie suala hili aende nalo na lile jina lake kama alivyofafanua Mhe. Mwakilishi aliyekaa sasa hivi. Kwa sababu hali ni ngumu kila usiku ukacha, mapembe haya yanakausha watu sauti.

Mhe. Spika, wenzetu Bara hawataki hata kuliona pembe, wanakula michele mizuri tu. Kwa nini sisi huku Zanzibar Mhe. Spika, tuwe tunakula lile lile pembe tu. Hebu aunde tume kwa makusudi aangalie kuna kasoro gani. Kama kuna ushuru mkubwa basi wapunguziwe hawa watuletee angalau mchele mzuri, kuliko leo anapunguziwa ushuru halafu wanatuletea lile lile pembe halitusaidii kitu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili suala aliangalie kwa kina kabisa kwa mujibu wa taratibu na sheria zinazoendana na wakati huu tunaokwenda nao.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 10 uimarishaji masuala ya miundo mbinu. Mhe. Spika, hapa kuna sentensi kidogo tu inanitia wasi wasi na sidhani kama lugha hii Mhe. Waziri Kiongozi anaweza kuitamka, niseme labda watendaji au kompyuta imerusha. Lakini hii lugha naomba kidogo nisaidiwe. Naomba kunukuu.

> "Mhe. Spika, serikali yenu inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu mijini na vijijini".

Mhe. Spika, inasema serikali yenu sasa hapa mimi kidogo kinanipa mashaka Kiswahili hiki. Kama angekuwepo Mhe. Moh'd Ali Salim (Mulla) angenisaidia. Nani mwenye serikali hapa anayezungumzwa? Mhe. Spika, sentensi hii sijui ina mantiki gani hii "serikali yenu", anazungumza Mhe. Waziri katika kitabu hiki cha hotuba serikali ni yenu, sasa nani ni nani. Mhe. Spika, ningeomba ufafanuzi kwa sababu sisi wengine kidogo tuna hii falsafa za Kiswahili kule kwetu Jimbo la Kitope. Sasa ningeomba anisaidie hii lugha ili nikae sawa.

Mhe. Spika, lakini tukija katika miundo mbinu amesimamia vizuri hata kule katika sehemu yangu ya Jimbo la Kitope kuna barabara nzuri kabisa sasa hivi. Niseme Alhamdulillahi tunashukuru masuala ya barabara imesimamiwa na fedha zilizoletwa zimetekeleza kama vile wajibu unavyotakiwa. Hivi ndio tunavyotaka, viongozi aina kama hawa ndio tunaowataka ili waweze kutuongoza.

Mhe. Spika, naingia ukurasa wa 12 suala la sekta ya afya. Mhe. Spika, mimi hapa siku zote nitasema na nitaendelea kusema. Wananchi wa Jimbo la Kitope

kila watakaponiletea suala la afya lazima nitalisema. Mhe. Waziri Kiongozi wasikudanganye, mimi sasa hivi naitwa dokta, usifikirie kuwa dokta ni *specialist* hapana, naitwa dokta kwa sababu zile huduma wale wananchi ambao tunawapelekea kule hospitali basi tumegeuzwa jina tunaitwa dokta.

Mimi napenda ndio dokta, kwani dokta lazima usome. Kuna dokta wa kutibu na wengineo, ukiiamini nafsi yako tayari umeshakuwa dokta. Mhe. Spika, inawezekana nikakwambia mjiti huu wewe utakutibu wala sikusoma, umekinai na umekula utapona kichwa, si dokta mimi, lazima niwe dokta.

Mhe. Spika, suala la afya leo hapa wamekuzwa Dk. Marijani lakini tuangalie fedha yake inalingana, hili tulitazame. Tumemsifu vizuri amerudi *fresh* juzi lakini je, tutamuenzi? Maslahi yake yatakuwa mazuri? Hebu tuliangalieni hili suala kwa sababu tunao wengi hawa lakini na wengi Mhe. Spika, wameshakimbia tusifichane. Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi kama hajui aniulize.

Mhe. Spika, kuna jamaa mmoja alikuwa KMKM kabakia na mwaka mmoja tu *specialist* wa masuala ya nusu kaputi yuko wapi sasa hivi. Kabakisha mwaka mmoja anaambiwa subiri kuna kiinua mgongo chako milioni 10, akasema hapa nakwenda zangu kunako pesa. Hujui hilo Mhe. Waziri Kiongozi, tukikaa hapa tunasema tu, linatuuma bwana kwa sababu kila siku tutakuwa tunahamia kwenda Bara kutibiwa tu. Pesa chungu nzima kule wengine hawana jamaa, wengine wanao jamaa.

Mhe. Spika, suala hili la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ndio tiketi yake Mhe. Waziri Kiongozi, hakika namwambia wala simfichi. Wananchi walio wengi wanaathirika katika hii Wizara ya Afya, ukilisimamia vizuri masharifu wa Mchangani *Allahu maamina* Mwenyezi Mungu atakubariki. Hili sikufichi nakwambia ukweli. Aaa kuingia Ikulu ataingia kwa nini asiingie.

Mhe. Spika, kusema ukweli suala la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii bado tunalitelekeza, wizara hii jamani hatuitazami, ni wizara muhimu sana hii. Leo mnabishana habari ya maabara, mimi juzi nimekwenda maabara nimewapeleka watu waliokuwa wanataka kufanyiwa uchunguzi wa kukatwa mabusha na ngiri hizo ndio fani zangu. Kwa nini niseme uongo, kama wamo wengine humu ndani wenye mabusha nitawasaidia. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, tumekwenda kule tumelipa kwa mujibu wa sheria ni kweli kwa sababu kila kipimo kina fedha yake. Lakini pale panapotolewa unapoanzia sio ndani kunakofanyiwa uchunguzi haparidhishi. Ukweli tuuseme hata mabenchi hamna, maana yake mabenchi yenyewe hayatoshelezi. Kwa sababu

sasa hivi ukienda utakuta wengine wamesimama, wengine wamekaa kitako, hebu tutafute sehemu iliyokuwa pana.

Lakini tukija hapa tunagombania *AC*, sijui wana nini. Mhe. Spika, nimeizungumzia hapa leo Mhe. Waziri sijui ataniambia nini, hata *AC* kule *ICU* hamna kuna mapanga boi, atanikatalia na wakati saa zote nakwenda kule.

Mhe. Spika, ukweli tunataka hili jina liendane na vitendo vyake. Hatupigi kelele tu hivi hivi tunaona yale mambo jamani. Leo utakuta ma-*orderly* au manesi ni kidogo sana wanafanya kazi kubwa sana mshahara wao mdogo. *Wallahi* inasikitisha kweli. Hapo nyuma walikuwa wakiingia zamu ya usiku ile *night shift* sijui, wanaingia kwa wiki moja hana motisha ya aina yoyote kutakuwa na uangalifu hapo.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri Kiongozi hili suala tiketi yake Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Waziri alikamate hili, linatupa matatizo, hebu twendeni na ile nembo yenyewe ya jina ya rufaa. Tunao uwezo wapo ma-*specialist* wazuri lakini hatuwawezi, hatuwathamini, hatuwafikirii. Leo daktari mzima hana gari hata vespa humpi.

Mhe. Spika, juzi moja kulitokea *emergency wallahi* nililia machozi, mtoto mdogo kapondwa na gari la ng'ombe anatoka Kinuni. Mimi nipo, anaitwa daktari anasema niko njiani, lakini je, angekuwa na usafiri wake angewahi kumuokoa yule mtoto, haikuchukua muda yule mtoto kafa, nimo ndani ya chumba cha *ICU* yule anakufa. Lakini yule daktari kaja kajitahidi, alipofika pale kajaribu na yeye kamuomba Mwenyezi Mungu lakini Mwenyezi Mungu kamwambia huyu wangu tu namchukua. Mhe. Spika, mtoto mdogo wa miaka kumi na moja.

Mhe. Spika, mimi niliuliza vipi daktari, akasema nimekuja na vespa, maana yake vespa yenyewe hakuitilia maanani kama ni yake. Hata hivi vigari vya *escudo* wanashindwa kukopeshwa ambavyo ni vya bei rahisi kabisa. Sasa hebu tuangalie mazingira, ndio maana nikasema tunao ma-*specialist* ni wazuri sana lakini wanaondoka *bye bye*. Hili tukilisema mnatuona sisi wawakilishi tunasema kama utani, sio utani jamani sote tuliangalie.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niisifu sana huduma ya maji ni nzuri inaendelea, lakini kuna mradi wa AKRA humu haukutiwa na wanatusaidia katika majimbo matatu. Lakini pamoja na hayo bado naisifu serikali kutokana na jitihada zake za kutuletea maji safi zimo katika mbio mbio, hiyo kusahau ndio mambo ya binadamu yalivyo.

Lakini ukurasa wa 19 Mhe. Spika, suala la kilimo kila siku nikiangalia Kibokwa, Bumbwisudi umwagiliaji maji. Mhe. Spika, tuna mabonde mazuri sana yenye rutba nzuri katika Jimbo la Kitope Kirombero, Pangeni na Upenja. Lakini nashangaa sana Mhe. Spika, kuwa kila siku tunaonesha maeneo yale yale. Namuomba Mhe. Waziri Kiongozi asikubali hilo, kila siku utakuwa unaoneshwa picha ile ile tu. Bajeti ngapi nimeshahudhuria mimi hapa nakuta yale yale Kibokwa, Bumbwisudi, Mwera, mengine yameachwa solemba. Kusiwe na mfumo wa bei? Utakuwepo.

Mhe. Spika, kuna masuala ya Muungano ambayo anashughulikia Mhe. Waziri Kiongozi, lakini kuna mambo makubwa sana. Sasa hivi askari wetu tusiwaachie wakawa wananung'unika, askari ni watu wa kuenziwa, ndio maana nikasema ni sawa sawa na sekta hii ya afya. Kuna tatizo la askari wetu hapa niseme wote lakini nazungumzia Zanzibar hawa polisi. Wananung'unika wanasema wanakatwa fedha ya shilingi elfu tano ya kifo, lakini fedha hii wanashangaa haitiwi kwenye *pay in slip* yao ya mshahara na hilo wanafanyiwa kama ni lazima. Kwa sababu akienda kule anakuta shilingi elfu tano imeshakatwa. Wamejaribiwa kushauriwa wamekataa Mhe. Spika, hebu na hili wasaidiwe.

Mhe. Spika, unajua Mwenyezi Mungu anampangia mtu umri anaweza kufika miaka 20 na zaidi hajafa yeye anaendelea kukatwa tu, sasa ile siku anayokufa analipwa shilingi milioni moja wakati huku nyuma ameshachangia milioni 10, hizi nyengine zitakwenda wapi. Mhe. Spika, suala hili wameomba na wao kupitia sisi viongozi wao kwenye Jimbo langu la Kitope polisi wangu wanalalamika hii fedha waangaliwe ina ulazima gani.

Mhe. Spika, halafu isitoshe zaidi la kusikitisha anaambiwa mtoto anayefika miaka 20 wako mwenyewe uliyemzaa yule hahusiki kwenye fedha ile haitamsaidia. Maana yake leo mtua amefiwa na mwanawe ana miaka 20 ukienda kusema kule hapewi kitu kwa maana hiyo anatazamwa huyu mtoto mdogo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi alione suala hili alifuatilie ndio roho zenyewe hizi.

Mhe. Spika, la mwisho la kunisikitisha humu nimeona mambo mengi unaambiwa sijui kuna ukarabati wa nyumba, makaazi ya Spika imetajwa. Lakini Mhe. Spika, gari ya Mhe. Waziri Kiongozi ni mbovu, benzi ile Mhe. Spika, naendesha mimi sasa hivi hebu nifikirie, yeye Waziri Kiongozi, mimi Mwakilishi tuwe sawa sawa. Gari inavuja *hydraulic*, nimekwenda pale kujisaidia nilishtuka nilisema kajichinja mtu hapa, kumbe naambiwa gari ya Waziri Kiongozi. Loh! salale.

Mhe. Spika, twende na wakati bwana, haiwezekani Mhe. Waziri Kiongozi kutumia gari ile imeshapitwa wakati. Maana yake kuna benzi hata ikifika akipata Mhe. Mshimba wewe tena haifai, twende na *model* nyengine bwana. Mhe. Spika, gari ya Mhe. Waziri Kiongozi mbovu, Dk. Mwinyihaji Makame amtafutie gari *immediately* tusije tukaadhirika, inavuja *hydraulic* aibu.

Mhe. Spika, mwisho nasema kuhusu Baraza letu la Wawakilishi pamoja na kamati zako nao waongezwe fedha hawa wafanyakazi wa Baraza hili. Mhe. Spika, tuwaangalie nao kwa vizuri kabisa. Mhe. Spika na Katibu tuwatazame wafanyakazi wetu wa Barazani wanastahiki wasaidiwe na wao angalau mtu aende na wakati na lile Baraza lenyewe, sio sisi wawakilishi tukimbizie tupate mafao tu. Tuwaangalie hawa wafanyakazi wetu waende na wakati, wavae vizuri, mtu si kama anashindwa kuvaa vizuri lakini uwezo wa fedha yenyewe anayopata ni ndogo. Mhe. Spika, hili lako tuwaangalie hawa wafanyakazi mafao yao ili waende na wakati, mshahara wanaopata mdogo tuwasaidie wafanyiwe marekebisho.

Mhe. Spika, nakushukuru sana, kwa kila la kheri namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie Mhe. Waziri Kiongozi, wenzetu wamesema awe Makamo, afike daraja la Rais bwana sio Makamo. Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono mia juu ya mia pamoja na Jimbo langu la Kitope. *(Makofi)*

**Bihindi Hamad Khamis:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi asubuhi hii ya leo. Pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema na salama.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na watendaji wake wote. Pia nisisahau kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuweza kufuatilia miradi ya maendeleo ya *TASAF* pamoja na miradi mbali mbali ya serikali. Mhe. Spika, pia niwapongeze watendaji wakuu wa *TASAF* Pemba pamoja na waratibu wake. Mhe. Spika, nilikuwa na mchango mkubwa lakini kwa sababu muda ni mdogo nitajitahidi kuchangia machache na wenzangu nao wapate nafasi.

Mhe. Spika, niende kwenye kilimo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi kwenye bajeti iliyopita alilitaja bonde la Makwararani kama litakuwa ni mojawapo litakalolimwa kilimo cha umwagiliaji maji. Lakini nakumbuka kwenye historia yangu kuanzia mwaka 1984 mpaka mwaka 1989 bonde lile lilikuwa linalimwa kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi atawaeleza nini wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na wanaoishi kwenye Jimbo la Mgogoni ili wapate maelezo mazuri wajenge matumaini kwenye eneo hili.

Mhe. Spika, niende kwenye Idara ya Maafa. Mhe. Spika, juzi tu Mhe. Subeit Khamis Faki wa Jimbo la Micheweni alimuuliza Mhe. Waziri swali la kuhusu maafa yaliyotokea Micheweni. Ni kweli maafa yalitokea siku ya Jumapili tarehe 6 mwezi huu. Kwa kweli sisi viongozi wa siasa linapotokea tukio kama lile la maafa huwa tuko karibu sana kwenye maeneo yale na hasa kwa sababu mimi mwenyewe binafsi naishi kwenye Jimbo la Micheweni nilitoka nikenda hospitali kuangalia ile hali.

Lakini Mhe. Spika, juzi tu nilishangaa kusikia kwamba Mhe. Waziri ile taarifa hajaipata. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri idara yake hii iwe pamoja na wananchi, iwe pamoja na Ofisi ya Wilaya na Majimbo ili linapotokea janga hili taarifa zifike kwa wepesi.

Mhe. Spika, niende kwenye majiko ya kusanifu kwa sababu kwenye hotuba ya Waziri Kiongozi alieleza nishati ya kutumia majiko sanifu. Mhe. Spika, kwa sababu mimi naishi kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba Jimbo la Micheweni na huwa ninatembelea majimbo mbali mbali, kwa kweli siku moja nilitembelea Jimbo la Wingwi nitawakuta kina mama wamejikusanya wanatengeneza majiko sanifu. Sasa sijui kama ilikuwa ni mradi wa *TASAF* au ni sehemu ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, kama ni mradi wa Afisi ya Waziri Kiongozi kupitia *TASAF*, basi namuomba Mhe. Waziri anieleze ili nikiulizwa maswali nipate kuwafahamisha vizuri kina mama wale.

Mhe. Spika, niende kwenye studio jamii. Mhe. Spika, maafa yanapotokea wakati tuna *studio* yetu jamii Micheweni ilikuwa taarifa zile zitoke kwenye maeneo yale ya Micheweni.

Mhe. Spika, nizungumzie mazingira. Mhe. Spika, juzi tu hapa tulikuwa na bajeti ya serikali kwa kila anayesimama huwa anaizungumzia Micheweni. Kweli eneo lile la Micheweni lililotengwa kwa ajili ya maeneo huru basi maeneo mengine ni ya wananchi. Mhe. Spika, naomba tuwafahamishe vizuri watu wa Micheweni wapate taaluma zaidi ya kuhifadhi mazingira ili wajue kama mazingira ni hatua moja wapo ya maendeleo.

Mhe. Spika, pia hapo hapo wakati mazingira ni eneo ambalo ni muhimu kwa kujiletea maendeleo yetu binafsi, pia ielekeze Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji lile eneo kama hawajataka kulitumia. Basi wananchi wa Micheweni wapande miti ili kurudisha hali ile ile iliyokuwepo zamani.

Mhe. Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri Kiongozi kwa kufuatilia miradi yote ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kwenye kilimo, afya na

maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Mhe. Spika, pia namuombea Mhe. Waziri Kiongozi aendeleze majukumu yake mpaka pale Mwenyezi Mungu atakapomuhitaji. Namuombea dua njema mimi na wanawake wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kila analoliomba Mwenyezi Mungu amuelekezee alipate na amjaalie aingie kwenye madaraka ambayo yana maslahi na yeye. Amin. Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunijaalia na mimi asubuhi ya leo kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nataka nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri Kiongozi kwa hotuba yake nzuri na pia nimtake basi kwa michango ambayo mingi imeshatangulia kama kawaida yake awe mfuatiliaji mzuri.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Haji Omar Kheir alivyowasilisha hotuba yake pamoja na Waziri Kivuli wa wizara hii. Kwa kweli hotuba zao zote ni nzuri zenye mantiki nzito ambayo inahitaji kufanyiwa kazi na sote tuliomo humu pamoja na wote walioko nje ambao wanatusikiliza.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze mchango wangu kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, mwanzo kabisa nikupongeze wewe kwa kukiongoza chombo hiki katika kipindi chote hiki kwa vizuri kabisa. Bila ya utata au bila ya kufanya kigugumizi hapana ambaye atapinga jinsi gani Baraza la Wawakilishi limepiga hatua katika utendaji wake wa kazi ambao wewe ndie unayetuongoza. Wale ambao wametangulia waliosema wana *experience* ya miaka 15, miaka 10 na zaidi pamoja na watendaji wa Baraza watakuwa ni mashahidi wa hili hususan katika kipindi hiki cha vyama vingi vya siasa. Mhe. Spika, tumepiga hatua nzuri nakupongeza sana.

Mhe. Spika, pia nipongeze suala zima la hatua ambazo zinachukuliwa kuhusiana na kuona kwamba chombo chetu sasa tutaweza kupata jengo zuri na la mfano katika Afrika ya Mashariki. Lakini pia ujenzi ambao mimi siku niliyoona nilipofikia jengo la Mhe. Spika, basi hatua iliyopigwa ni ya haraka na ya kupigiwa mfano. Kwa hiyo, tunapongeza sana shughuli za Baraza zinavyokwenda.

Lakini Mhe. Spika, pia niungane na wenzangu katika kumuomba sana Mhe. Waziri Kiongozi ingawa hili si geni wala si jipya tumeshalisema sana kwamba chombo hiki kipate heshima yake inayostahili katika suala zima la matumizi.

Suala hili ambalo wenzangu wengi wameshatangulia kulisema lakini kwa umuhimu wake sina budi kulirudia la kwenda tukipiga magoti kwa kweli linakidhalilisha chombo chetu. Hasa ukiona kwamba wale ambao tunawaendea kwa ajili ya shughuli hizo sidhani kama wanastahiki sisi kwenda kuwasjudia.

Kwa hivyo, ni muhimu na ni vyema Baraza letu sasa tunaelekea ukingoni kuelekea kwenye uchaguzi mkuu. Lakini mara tu litakapoanza Baraza jipya basi na utaratibu uwe mpya kwamba chombo hiki kiwe na mfuko wake kutoka Hazina moja kwa moja, kikisimamiwa na Katibu wetu wa Baraza chini ya uongozi wako Mhe. Spika, ili tuweze kujipangia mambo yetu kadiri ya vile ambavyo tunayapanga wenyewe. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelalamika na wengine wewe mwenyewe umesema Mhe. Spika, wametaka kukurejeshea *passport* zao. Lakini hii inatokana na moja ya sababu ya hili suala la kwamba hatuwezi, bado hatuna fursa au uhuru wa kuweza kujipangia mambo yetu.

Katika mambo muhimu Mhe. Spika, ni suala zima la kuwatoa wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kwenda katika nchi mbali mbali, ili kuweza kuwaona wenzetu wamepiga hatua kwa kiasi gani. Ushahidi umeonekana hapa wazi kwamba wale ambao wametoka nje kama Mhe. Fatma Fereji na kamati yake na wengine ambao wamekwenda sehemu mbali mbali, basi wamekuwa na mchango mzuri wa kuonesha tofauti au wenzetu wanafanya nini na sisi tunafanya nini? Kwa kweli inatupeleka kupiga hatua za kimaendeleo.

Kwa hivyo, ili tuweze kuwa na nafasi nzuri ya kuona kwamba tunaweza tukawatoa wajumbe wetu katika mafunzo ndani na nje ya nchi kwenda kuona mambo mbali mbali kuhusiana na utekelezaji wa shughuli zao, basi ni vyema Baraza la Wawakilishi liachiwe lifanye mambo yake wenyewe kupitia mfuko ambao Mhe. Waziri wangu kivuli hapa ameelezea kwamba huo ni mfuko unaoitwa *The House of Representatives Fund.*

Nikitoka hapo, katika suala hili hili la Baraza la Wawakilishi, nilitaka na mimi nizungumzie kidogo tu suala zima la kuwa na mfuko wa maendeleo ya jimbo. Lakini pia nitilie mkazo suala zima ambalo Mhe. Ali Haji Ali jana alilizungumza, kwamba ili na hii mifuko iweze kufanyakazi zake vizuri, basi kuwe na mamlaka huku chini, hizi zinazoitwa serikali za mikoa ziweze kufanya kazi zake kama ni wasaidizi wa serikali kuu, badala ya kuwa serikali kuu kila kitu inafanya yenyewe na huku labda kuna wasimamizi tu kama Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya. Kwa hivyo, ziwepo hizi serikali ili wakishirikiana na wabunge na wawakilishi wao kwa kupitia mifuko hii, basi maendeleo yanaweza yakapatikana kwa haraka kwa mujibu wa hali na mazingira ya maeneo husika.

Mhe. Spika, katika suala hili nimalizie kwa kugusa kile kipengele ambacho Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji jana alikisema kwa ukali kidogo, suala la kwamba chombo hiki labda kuna watu wametaka kukaa kukishughulikia na akahoji kuna uhalali gani wa hilo.

Mhe. Spika, mimi pia niliona *concern* yake alivyozungumza. Lakini kwa upande wangu mimi nikafikiri kitu chengine kwamba labda kilichokusudiwa pale ilikuwa ni kuli-*access* Baraza. Sasa ikiwa hivyo ndivyo, basi nadhani vipo vyombo *independent* vinavyofanya kazi hizi. Wapo watu kama *REDET*, kuna wengine wanaitwa *cinovete* tunaona wanatoa taarifa zao mbali mbali baada ya utafiti wa kuchunguza mwenendo wa kitu fulani. Kwa mfano juzi tumesikia wakitoa, ingawa walikuwa wakitofautiana katika kusema kwamba Mhe. Rais kafikia asilimia hii au hivi katika utendaji wake labda wa kutekeleza ilani za uchaguzi na kadhalika.

Kwa hivyo, sio vibaya kama kunaweza kukatokea kitu kama hicho, lakini viwe ni vyombo huru vinavyoweza kukaa na vika-*access* na pia vitatupa changamoto katika chombo hiki kuweza kuona wapi labda tunakosea? Wapi turekebishe na wapi tuendelee kufanya vizuri zaidi?

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka nizungumze kidogo kuhusu suala la mazingira kama lilivyoguswa katika kitabu cha Mhe. Waziri Kiongozi kwenye ukurasa wa 23 kifungu cha 31.0 na kusema kwamba uharibifu wa mazingira unachangiwa zaidi na ukatwaji wa miti. Inakadiriwa kama hekta 1,000 huwa zinaangamizwa kila mwaka.

Mhe. Spika, maoni yangu hapa pamoja na kusoma ripoti mbali mbali za wataalamu au watafiti wanatuambia kwamba ongezeko kubwa la watu katika eneo pia linasababisha uharibifu wa mazingira. Kwa sababu kwa vyovyote watu wale watahitaji kukaa na kufanya shughuli mbali mbali. Kwa maana hiyo, kunatokezea haya mambo kama yalivyoelezwa hapa ya uangamizaji wa misitu. Kwa sababu sisi ni wtu wa visiwa na visiwa vyetu ni vidogo, bila shaka na ardhi nayo itahitaji kuonekana umuhimu wake wa kuangaliwa, lakini pia kulinda maisha yetu kwa kupitia uharibifu huu.

Mhe. Spika, tunashuhudia sehemu mbali mbali au ukitazama wataalamu wanavyotuambia, ilizungumzwa hapa asubuhi katika kujibu maswali hapa kwamba inasaidia katika kutupa hali ya hewa nzuri ndani ya nchi. Sasa tunapoipunguza ndio joto linazidi, kina cha bahari kinaongezeka na kadhalika.
Mhe. Spika, ushauri huu nilishawahi kuutoa muda mrefu huko nyuma na leo nitapenda niurejee kwa sababu hali inazidi kuwa mbaya uingiaji holela wa watu ndani ya visiwa hivi Mhe. Spika, kila mtu ni shahidi. Unapozungumzia habari

ya Mji Mkongwe ulivyojazana wafanyabiashara hawana mpango, bila shaka na makazi yao ni hivyo hivyo. Lakini na maeneo mengine tofauti.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani umefika wakati tuone haja ya kwamba uingiaji wa watu ndani ya visiwa vyetu uwe na utaratibu maalum, isiwe kila mwenye nauli yake ya boti au hata kama kasaidiwa boti za mizigo zile Shs. 2,000 anaingia anakuja zake hapa. Huu Mhe. Spika, hautufikishi mbali. Ikiwa tuna malengo ya kisiasa sasa hivi tunaelekea katika kuona tunajenga Zanzibar mpya, siasa yetu ni Zanzibar kwanza. Kwa hivyo tuone basi kama Zanzibar nayo uingiaji wa watu ndani ya nchi yetu kama kwengine kunavyofanywa. Hata katika kitabu ambacho nimekipokea asubuhi hii kunazungumziwa suala zima la SADEC kunaona kwamba kuna *universal*, ili kuona uingiaji katika maeneo hayo unakua *controlled*. Kwa maana hiyo hata ndani ya visiwa vyetu hili suala ni muhimu na ni vyema Mhe. Waziri Kiongozi akalikalia hili na kuona ufumbuzi wake unakuaje.

Mhe. Spika, nikiwacha eneo hilo sasa nataka niingie katika Idara hii ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ambayo moja kwa moja nitakwenda katika ukurasa wa 45, kifungu cha 61.4

Kifungu cha 61.4

> "Kuratibu kikao kimoja cha Mawaziri wa Muungano na Zanzibar kilichofanyika tarehe 03/05/2010 hapa Zanzibar".

Mhe. Spika, hapa ninapata wasi wasi kidogo kwamba mwaka mzima huu, hatujui Bara kumefanyika vikao vingapi, lakini hapa Zanzibar kimefanyika kikao kimoja tu. Kwanza naona kwamba labda haya mambo hayapewe umuhimu unaostahili, ukilinganisha na kero ambazo tunazo za Muungano zinazohitaji kuzungumzwa katika vikao hivi. Mimi nilidhani kila mwezi kungekuwa na kikao na katika kila kikao angalau japo kero moja ingekuwa inatatuliwa, lakini mpaka leo hii tuna kikao kimoja ambacho kinaonekana katika kitabu hiki. Pia kupitia taarifa mbali mbali za hotuba ikiwemo na hotuba tuliyomaliza ya serikali, tunaambiwa kuna mambo sita, ambayo kwa mimi muono wangu pengine moja au mawili na labda hayajatimia katika kule kutekelezwa kwake au kuwa kero hiyo imetatuliwa. Kwa kweli naona suala hili halijapewa uzito unaostahili wa kuona kuwa hizi kero zinaondoka.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 62, kwenye ukurasa wa 46 imeelezwa hapa wataalamu wa wizara na Afisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanatafuta mbinu ya kutekeleza agizo la kuwapatia Wazanzibari mgao wa ajira katika maeneo ambayo ni ya Muungano. Hili mimi linanishangaza sana, linanishangaza kwa sababu nashindwa kuwaelewa wenzetu hawa wa upande wa pili . Hivi mpaka leo wanadhani kuwa sisi bado ni watu wa kufikiriwa,

wakae wafanye mipango. Hivi walisahau kwamba ule mwaka 1964 tuliungana tukiwa nchi kamili sisi, wao nchi Tanganyika na sisi nchi Zanzibar, kwa nini wanasahau hicho. Kwa kweli hapa naona ni mambo ya kuchezesha na kupoteza muda tu.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 4 kinachosema kwamba naomba kunukuu;

Kifungu cha 62.0

> "Wizara za Fedha ya Muungano na Zanzibar zimetakiwa ziangalie kwa pamoja nyaraka za kuthibitisha kuwepo hisa za Zanzibar Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Taarifa ya suala hili ipelekwe kwa Makamo wa Rais, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi tarehe 24/06/2010".

Mhe. Spika, maana mpaka leo hawana uhakika, wanaona labda ni uvumi. Sasa watafute hizo nyaraka wathibitishe na mimi naona zipo kwa hivyo hiyo ithibati itapatikana tu. Kwa hivyo, sasa nataka kujua baada ya kwisha kuthibitika kama na kipengele cha pili huku nilivyokiacha, kinachozungumzia habari ya asilimia 4.5. Wakishathibitisha kwamba asilimia ya Zanzibar kutokana na hizo hisa ambazo ziko pale, pamoja na mchango wa Zanzibar katika kuanzishwa kwa BOT.

Je, watatulipa na fidia kuanzia ule mwaka 1965 ambapo walikuwa hawatupi chochote, na kuanzia huu mwaka 2006 au mwaka 2009 ambapo tumeanza kupewa hii asilimia 4.5 kipindi hiki chote ambacho tumeanza kupewa hiyo asilimia 4. 5 tofauti baina ya hiyo hisa kamili itakayopatikana itakuwa vipi na hili tuambiwe litachukua muda gani? Kwa sababu ni masuala ambayo yameshapita muda mrefu na ni jambo ambalo linajulikana, lakini watu hawajakua tu na ule umakini wa kulipa umuhimu hili suala na kulikalia kitako kuona jinsi ya kulifanya hili suala.

Suala jengine Mhe. Spika, katika hiki kipengele cha 5 ambacho kinasema,

Kifungu cha 5

> "Waziri Kiongozi ameshamwandikia Waziri Mkuu kuhusu mapendekezo ya Zanzibar juu ya kuondolewa kwa suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano. Waziri Mkuu analifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Sasa najiuliza hivi Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar mkubwa ni nani? Kwa sababu wenzangu wameshanukuu hapa hotuba ya Mhe. Rais ya katika sherehe za Januari 12 mwaka huu kwamba hili suala limeshamaliza wala sio suala tena la kutafuta, sisi tunasubiri utaratibu tuchimbe tu, sasa ikiwa tena watu wameanza kukaa anasubiriwa Waziri Mkuu atowe yeye mapendekezo yake. Najiuliza hivi yeye na huyu Rais mkubwa yupi, kwamba huyu apinge kauli za huyu?

Pia Mhe. Spika, hapa hapa najiuliza au ndio maana ya kumuondosha Rais wa Zanzibar asiwe Makamu ili kwa mujibu wa *protocol* yao awe Rais wa Zanzibar ni waziri tu asiye na wizara maalum, kwa maana hiyo yeye amsubiri Waziri Mkuu anavyopenda yeye na anavyotaka yeye. Kwa kweli Mhe. Spika, hatukuitendea haki nchi yetu. Wala kipengele hiki nisingependa hata kuwemo humu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi, kwa sababu naona kama kwamba imekuwa kauli ya Mhe. Rais sasa haina maana na tunasubiri kauli ya Waziri Mkuu wa serikali ya pili huko kutoka Tanganyika atusemee yeye kwa maslahi yetu sisi.

Mhe. Spika, mfano nyumbani kwako unataka kupika lakini unasubiri jirani akuambie upike au usipike, sioni kama hii ni haki Mhe. Spika. Kwa nguvu zangu zote kipengele hiki mimi naona kama sijakiona, nichukulie kuwa sijakiona. Kwa sababu bado najua kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar yeye ndiye Rais wa Zanzibar na yeye ndiye angestahiki kuwa kauli yake ni ya mwisho.

Mhe. Spika, lakini ukiachilia mbali kauli ya Mhe. Rais, chombo hiki sijui kama yuko mtu mwengine ambaye atatoka mbali ya Zanzibar aseme kwamba maamuzi yetu sio. Haya ni maamuzi ambayo tumeshapitisha katika Baraza na Baraza la Mapinduzi limeshapitisha maamuzi yake na ndio maana Mhe. Rais alitoa kauli ile. Kwa hivyo, katika hili Mhe. Spika, nilikuwa napenda sana wenzetu waheshimu. Sidhani kama hili lilihitaji kuingizwa katika mazungumzo ya kero, kwa sababu kero hii tulishaiondowa wenyewe.

Mhe. Spika, bado naendelea kushauri kwamba kila kero ambayo tunaona kwamba tunaweza wenyewe kuiondosha, ninadhani zote tunaweza basi tufanye hivyo. Sasa ikiwa kero hizi zitahamia upande wa pili basi itakuwa vizuri, kwa nini sisi tu ndio tuwe tuna kero. Mimi sijasikia upande wa pili kama wao wana kero. Sasa wao watakapokuwa na kero na sisi tuna kero, labda tutapata ufumbuzi mzuri na kuona kwamba kuna umuhimu wa kukaa kutatua. Vyenginevyo itakapokuwa sisi tu ndio tunaokusanya kero na wenzetu wanapata vitu vyao vyote, hawana shida na kila kitu ni chao, nadhani hata siku moja hawatayapa umuhimu masuala haya ambayo sisi tunadhani ni kero.

Mhe. Spika, katika masuala haya hata Mhe. Waziri Kivuli katika hotuba yake kwenye kipengele hiki cha Idara ya Uratibu ameeleza mambo mengi hapa ambayo ameona na mimi naona ni hivyo hivyo naunga mkono kwamba bado Wazanzibari hatujapata nafasi ya kueleza au kutetea mambo yetu hata katika hizi jumuiya ambazo zinaundwa, iwe ni SADEC au Afrika ya Mashariki na nyenginezo. Siku zote tunasemewa, siku zote matokeo yake yanakuwa na matatizo kwetu sisi na kutuongezea masuala ya kero. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, kwa uwezo ambao tunao kwa kupitia katiba yetu na kwa uwezo ambao Rais wa nchi hii anao, basi ni vyema masuala ambayo tunayatolea fat-wwa yakaheshimiwa kama sisi tunavyoheshimu wengine.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba nimalizie kwa kutilia mkazo tu masuala haya ya Idara ya Maafa upande wa walemavu.

**Mhe. Spika:** Kwa dakika mbili.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** *Inshaallah*. Mhe. Spika, kwa kuwa maafa yanatokea sana na sote ni mashahidi na hasa katika hali hizi ambazo kuna mtafaruku wa hali ya hewa katika dunia, basi ni vyema hata hii Idara ya Maafa kwa mfano, iingiziwe fedha kiasi kwamba linapotokezea tatizo liweze angalau kwa asilimia 50 liweze kutatuliwa kwa pale pale. Kwa sababu ukiangalia kitabu hiki hata ile fedha inayoombwa basi inaingizwa kwa asilimia 30 ndivyo ilivyoandikwa hapa na kwa upande na kwa upande wa walemavu vile vile wameingiziwa kiasi hicho hicho na mara hii inaonekana imepungua zaidi. Kwa hivyo, itakuwa hata hiyo asilimia 30 haifikii. Sasa niendelee kusema kama walivyosema wenzangu kwamba sisi sote hapa ni walemavu watarajiwa, kwa sababu wakati mwengine unaweza ukajikwaa tu au kiatu tu kikakuendea hivi basi ikawa ndio sababu hiyo ikawa tena na wewe ndio umekosa mguu.

Kwa hivyo, haya ni masuala ambayo kwa kweli Mhe. Waziri Kiongozi tunataka uyape umuhimu wa hali ya juu kwa sababu hatuwatengezei tu wao, lakini tunajitengenezea sote kwa sababu kila mmoja hajamaliza kuumbwa.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kuheshimu muda wako naomba nimalizie hapa. Ahsante sana.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nitakuomba radhi sitosimama, nitachangia hapa hapa.

**Mhe. Spika:** Unaruhusika.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataallah* mwenye kutuwezesha na kutufikisha hapa na

tukawa tuko salama na Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atujaalie shughuli hizi zimalize salama.

Pia nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, mimi nitakuwa katika ukurasa wa 53 na nitamalizia katika ukurasa wa 55 katika Idara ya Shughuli za Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, Idara ya Shughuli za Watu wenye Ulemavu, halafu kuna Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Nafikiri Jumuiya hizi sasa zimekua nyingi sana. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri Kiongozi kwa kazi zake nzuri na ninampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Aman Abeid Karume.

Mhe. Spika, kwa sababu walemavu siku nyingi sana huko nyuma tulikuwa hatujitambui tuko wapi? Serikali ya Awamu ya Sita naipongeza sana kwa kuweza kutuhamasisha na kuweza kufikia hapa tulipofika. Pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru marehemu aliyekuwa afisa wetu hapa marehemu Maalim Khalfan Hemed Khalfan, Mhe. Spika, huyu aliweza kuwatetea walemavu kwa hali na mali jinsi na yeye alivyokuwa ni mlemavu na alitutoa katika mwahala mwingi sana.

Kwa sababu Mhe. Spika, tulikuwa walemavu hatujui twende wapi wala hasa tulikuwa hatujitambui kwa kweli. Lakini naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kupitia kwa marehemu Maalim Khalfan, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie roho yake aiweke katika malazi ya watu wema peponi amin.

Mhe. Spika, shughuli za Watu wenye Ulemavu na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Jumuiya tulizonazo ni nne na watu wenye ulemavu ni watu maskini wa umaskini sana. Usiangalie mjini, angalia vijijini tunakotoka na walemavu wanazidi siku hadi siku Mhe. Spika. Tuna UWZ hawa ni walemavu wa viungo, kuna ZANAB hawa ni walemavu wa macho, kuna ZPDD hawa ni walemavu wa akili na kuna wenzetu Jumuiya ya juzi tu imeundwa ya maalbino na nyenginezo.

Mhe. Spika, watu hawa ni maskini sana na wanataka tegemezi sana kwa kupitia katika Idara yao ya Waziri Kiongozi kwa hali na mali ili kuwatetea. Linalonisikitisha sana Mhe. Spika, watu wenye ulemavu kama ni watu wa kutelekezwa au kama labda watu tunawalazimisha watusaidie hata hatujui tuko wapi? Maana serikali inavyotoa uwazi wa watu wenye ulemavu, lakini bado kabisa haijafikia hapo.

Mhe. Spika, hivi viofisi vyetu tunavyofanyia kazi, basi leo utaomba haya kesho unahamishwa utawekwa pahala pengine nafikiri ni sehemu ya watu

wakihifadhia makaa. Yeye haingii lakini atakwenda kukuweka wewe. Mhe. Spika, pengine na choo kiko hapo hapo. Hili ni jambo jamani linatusikitisha.

Mhe. Spika, mimi nilikwenda Mkoani wakaniambia niwaombee jengo lililokuwa la ZSTC wakati huo halijauzwa nafikiri na nilipigania kwa juhudi zote angalau tugaiwe hilo jengo na nikawaambia matengenezo yote nitatoa mimi, saruji, rangi na kila kitu, lakini ilishindikana. Majengo ya serikali yamo. Kwa hivyo, kupitia kwa Mhe. Waziri Kiongozi basi atusimamie na sisi tupate humu katika majengo ya serikali kule Pemba, ili tupate mwahala mwa kufanyia kazi zetu. Sio tena tujikusanye vibarazani, tutaonekana ni watu wa maajabu na serikali wao ndio waliotaka kutukwamua katika umaskini, ili watuweke kwenye hali ya kawaida na tujione ni watu wazuri kama wenzetu.

Mhe. Spika, ikiwa hilo haliwezekani kwanini basi tukishapewa mwahala tuhamishwe wakati nyumba ni ya serikali mtu hajaijenga yeye? Anakuambia hapa hama nenda kakae kwengine, tutakua vipi sisi?

Mhe. Spika, juzi walemavu wangu waliopo Wete, kiofisi tulichonacho basi watu 50 hatuingii na walemavu nikikupa idadi yake hiki kikundi kimoja tu basi ni watu wengi sana. Basi hiyo juzi watu walihamishwa kwa masikitiko sana kijichumba walichowekwa, mimi sijaingia wala siwezi kuingia, maana mguu hivi ulivyo nikienda kuuzidisha halafu daktari aje aninyanyuwe na kwenda kuniunga tena. Hatuna nafasi Mhe. Spika.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri Kiongozi chini ya idara hii na sisi wakati ndio tulipo, basi majumba ya serikali atutengee pahala kwa kufanya shughuli zetu. Kuanzia Wete, Mkoani, Chake Chake na Wilaya ya Micheweni sehemu zote hizo walemavu wameenea. Kama si hivyo, basi kiwanja tunacho serikali itusaidie ili tuweze kujenga, hatuna mfadhili, tumeomba mpaka tumechoka, *data* zimekwenda zikirudishwa lakini hatujapata kujengewa. Kwa hivyo, tunaomba serikali iweze kutuweka, imejenga majumba ya maofisi mbali mbali tele, ndio washindwe na sisi kutujengea ili wakatuweka pahala tukahifadhika. Chini ya Waziri Kiongozi naomba suala hili aweze kulitizama kwa kina jinsi watu wenye ulemavu wanavyopata shida.

Mhe. Spika, mafunzo yaliyotoka katika kamati hii ya taifa nayo haitende haki vile vile. Kwa sababu kamati hii ni kamati imeundwa ya watu wenye ulemavu wote. Basi angalau wakifanya zile shughuli zao watualike. Mimi kama Mwakilishi wao watakaloliamua huko basi vigongo vinanifika mimi, lakini sialikwi hata siku moja wala sijui kinachoendelea huko. Nakuja kuambiwa tu kuna jambo hili na jambo hili wewe tuchangie hiki.

Sasa Mhe. Spika, kama na mimi nimlemavu wa viungo, ni mlemavu wa mambo yote. Kwa sababu Mwenyezi Mungu asikujaalie ukasema leo kidole kimekaa hivi kichwa kitakaa sawa. Hujajijua mbele yako, maradhi kwa kila leo yanatuingia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi aweze kuwatizama walemavu kwa jicho la huruma na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa uwezo, kama alivyoweza kutushughulikia huku mwanzo. Kwa hii miaka mitano tu niliyokaa basi mafunzo mengi sana mimi nimeyapata, mafunzo ya UKIMWI na mambo mengineyo ya watu wenye ulemavu kwa kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi na watu wengine.

Mhe. Spika, huyu Waziri Kiongozi ni mtu wa mfano, kwa sababu na yeye amejiwekea kuwa hizi Jumuiya za watu wenye ulemavu, hayuko aliyekuwa haijamgusa humu ndani. Kama sio mwanao basi ni ndugu yako, kama si ndugu yako mkeo, kama sio mkeo basi ni mama yako. Kwa hivyo, sote humu ndani ni walemavu, wewe unatembea lakini ulemavu unao basi ni mlemavu. Kwa hivyo, naomba walemavu watizamwe kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, halafu katika hawa wawili waliokwenda kusoma kwa hizi shughuli za watu wenye ulemavu. Mhe. Waziri hawa hawatoshi kwa sababu walemavu kwa Unguja na Pemba ni sawa sawa na hawa waliokuwa sio walemavu ni mchanganyiko. Kwa hivyo, tuzidishiwe mori wa kuweza kupelekwa kwenye mafunzo na kuweza kuwashajihisha wenzetu na kuwahamasisha.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa kwenye kamati ya taifa tulikuwa tukiwahamasisha walemavu na tulikuwa tukiwahamasisha kwa nguvu na ari, wala tulikuwa hata usafiri hatuna. Mimi siku moja nimekaa tu nyumbani kwangu, kidogo akaletwa dereva ameambiwa mchukuwe Bi Raya aende Makangale. Haya walemavu nitawakuta wapi. Nikaambiwa ukifika wameshakusanywa kwa Sheha. Hata mume wangu alikuwa hayupo basi nikawacha salamu tu kwa watoto, basi nikatoka na kwenda mzigoni, kutwa huko mpaka saa 12 tunawatafuta walemavu. Tulipokwenda huko Makangale tuliwakuta walemavu wa kila aina, kuna watoto wengi sana walemavu wa akili.

Mhe. Spika, tulipofika na kuwahoji wakasema wao hata hiyo hospitali hawazijui, hata mjini hawakujui, hawajui mahali popote, tunawashajiisha ili watoto wale wapelekwe hospitali.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri Kiongozi, humu mashamba ndimo watu walimokuwa na shida sana na kudhia, hawajui jinsi ya kupata haki zao, hawajui wao waende wapi na katika kuhamasisha ni uzito. Kwa sababu kwa kwenda siku moja basi siku ya pili huwezi kuwapata.

Halafu Mhe. Spika, ulemavu kwa hakika unayumba sasa hivi. Tokea afariki Maalim Khalfan sikufichi Mhe. Spika, ulemavu unayumba na hizi Jumuiya huwenda zikavunjika kwa sababu hazina wale watu wa kuweza kusimamia waliokuwa madhubuti katika Jumuiya hizi. Hivi sasa nikikuambia watu kila wanapokaa wanaambiwa hameni, hata ile afisi yetu ya Chake Chake ile basi pale watu wameshaambiwa wahame na vitu vyao vyote wavihamishe.

Mhe. Spika, juzi tulikwenda kufanya kikao wakaniambia Mhe. Bi Raya tunahama tutahamia wapi, kodi ya nyumba ile pale kwa mwaka sijui ni milioni moja na zaidi basi hawana. Kwa hivyo, imebidi mwenye nyumba akawaambia wahame kabisa. Halafu mule ndani muna vitu chungu nzima vilivyokuwa tukivifanyia kazi. Sasa ikiwa watahama na kwenda kuomba chumba pahali, vile vitu watakwenda kuviweka vipi na watawezaje kufanya kazi zao, itakuwa ni mtihani Mhe. Spika.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atutizame kwa jicho la huruma. Majumba ya serikali yapo, kwa hiyo tuweze kupewa na sisi ili tupate afisi tujisikie. Ikiwa si hivyo, basi tuweze kupiganiwa angalau kiwanja tunacho basi tuanziwe msingi na tusaidiwe kidogo kidogo ili tupate pakukaa Mhe. Spika.

Jengine ni kuhusu ajira kwa walemavu. Mhe. Waziri Kiongozi tunaomba kule kwetu sisi kwa mazingira yetu basi watu watakapoajiriwa na mlemavu akijitokeza aonekane. Japokuwa kasoma sana na vyeti atakwenda navyo, lakini watu wakichukuliwa anaambiwa njoo kesho, njoo keshokutwa hapati ajira. Tunaomba kwa kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi, angalau utuangalie na sisi na iweze kutoa ajira kwa Unguja na Pemba angalau hawa walemavu wawili mmoja atoke Unguja na mmoja atoke Pemba, ili na wao wajisikie.

Mhe. Spika, sasa hivi watu wanashajihishwa kusoma na watoto wamesoma na wamepata. Kwa hivyo, tunaomba watu watakapoajiriwa na walemavu wasisahauliwe wakawekwa nyuma kwa wale wenye elimu zao Mhe. Spika, ili na wao wajikwamuwe, wale ni watu wanategemewa, ikiwa ni mwanamke kaolewa anazaa na ikiwa ni mwanamme ameoa anazaa wanataka kuhudumia familia zao.

Jengine Mhe. Spika, ni elimu naomba nigusie kidogo, kwa sababu watoto wale taahira tulitaka ule mchanganyiko Mhe. Waziri, lakini ule mchanganyiko kwa hakika kila ninapotembelea maskulini ni mgumu, kwa sababu hawa watoto taahira, yaani wale walemavu wa akili Mhe. Spika, watu hata hawajui wafahamiane nao vipi.

Skuli tuliyonayo ya kusomesha watoto hawa wenye matatizo ya akili ni sehemu moja tu ambayo ni Michakaeni, yaani watu hawa uwezo kuwatoa watoto

mashamba na kuwapeleka Michakaeni. Nafikiri ni vyema angalau tupatiwe usafiri wa *min-bus* kwa ajili ya kuwachukua hawa watoto kwenda na kurudi, kwa sababu wazee wao hawawezi kuwapeleka na kuwarudisha.

Kwa kweli humu tunamowachanganya hawafaidiki, yaani hawapati chochote, kwani mimi ninakwenda na watu kuniambia sisi hatuelewani nao na wala hatujui chochote maana hujui hata umueleze vipi.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri katika kupitia wizara yake haya ayaone.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi, wanawake wenzangu, Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu pamoja na wanawake wa Pemba wa Kusini na Kaskazini tunaiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa asilimia mia *(Makofi).*

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa uchache wa muda basi nitajaribu kwenda haraka na kukata baadhi ya mambo.

Kwanza naomba niunge na wenzangu waliompongeza Mhe. Waziri Kiongozi, kwa utendaji wake katika kipindi hiki cha miaka kumi.

Baada ya pongezi hizo naomba moja kwa moja nianze na Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, Baraza letu ni moja kati ya mihimili mikuu mitatu ya dola, ambapo imeelekwa kwamba Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama. Kati ya hayo, niungane na wale wenzangu wote Waheshimiwa Wawakilishi walioona haja na umuhimu mkubwa kwa wakati tulionao hivi sasa, kwa serikali kukubali na kuridhia kuanzisha Mfuko wa Baraza na wenzangu wameeleza kwa urefu.

Mhe. Spika, hili halikutokana na kikao hiki tu, tangu kipindi cha nyuma tulikuwa tukilizungumza hili, lakini nashindwa kuelewa jinsi serikali inavyolipiga chenga suala hili.

Nadhani Mhe. Waziri Kiongozi wakati atakapokuja kufanya majumuisho ya hotuba yake, kwa sababu kila mwakilishi anayesimama hapa hutaka suala hili lianzishwe. Kwa hivyo, labda tupate muongozo wako Mhe. Spika sisi Wawakilishi tufanye nini, ili serikali itekeleze suala hili. Kwa sababu Baraza hili ndilo lenye mamlaka na wajibu wa serikali ni kufuata maamuzi yanayotokana na Baraza. Sasa ikiwa wawakilishi sote tumeshasema hivyo hatujui tuzungumze lugha gani zaidi ambapo serikali itapaswa kutii suala hili.

Kwa hivyo, kama kuna muongozo Mhe. Spika baadaye utueleze wawakilishi, ili tuufuate kwa sababu upo umuhimu mkubwa kutekelezwa hususan katika kipindi hiki na hicho tunachoelekea baadaye.

Mhe. Spika, nikiendelea na Baraza la Wawakilishi kuna ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete. Kwa kweli ule ni ukumbi ambao ulikuwa ukitumika mpaka miaka ya karibuni, lakini sijasikia lolote lililozungumziwa kuhusu kuimarisha ukumbi ule.

Je, Baraza au serikali imekubali ule ukumbi kumalizia vile vile, kama sivyo basi tuiulize serikali kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi, mpango wa serikali uko vipi katika kuimarisha ukumbi ule. Kwa sababu Zanzibar ni visiwa viwili Unguja na Pemba pamoja na kwamba tayari imeshakubalika kuwa mikutano mingi au yote takriban ifanyike hapa. Lakini katika kukiendeleza Kisiwa cha Pemba upo umuhimu mkubwa kwa ukumbi ule kuuendeleza kwa maslahi ya Baraza pamoja na nchi yetu kwa jumla.

Mwisho kuhusiana na Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, wakati mwengine huwa napata tabu sana kuifahamu itifaki ya nafasi ya Spika katika shughuli za kitaifa.

Kwa mfano, viongozi Rais kwa Serikali, Spika kwa Baraza la Wawakilishi na Jaji Mkuu kwa Mahakama. Lakini haipendezi katika shughuli za kitaifa ambazo Mhe. Spika unakiwakilisha chombo hiki unachohudhuria katika kutaja itifaki ya uongozi Mhe. Spika takriban wewe kutajwa pamoja na Wakuu wa Mikoa au Masheha, hainipendezi vizuri kwa kweli *(Makofi)*.

Kwa sababu kwa kufanya hivyo ni sawa na kulidhalilidha Baraza hili, ambacho ndicho chombo kikubwa cha wananchi. Kwa hivyo, nadhani wakati wa majumuisho Mhe. Waziri Kiongozi atakapokuja naomba anitajie nafasi ya itifaki ya Mhe. Spika kwenye shughuli za kitaifa iko vipi. Kwani unapotajwa wewe Mhe. Spika ndio kutajwa sisi wawakilishi.

Mhe. Spika, suala la pili kuhusu Tume ya Uchaguzi, kwa kweli wenzangu wameshaeleza kwa kirefu na wala sitaki kurejea. Lakini hivi sasa upo uandikishaji wa watu wambao waliokosa sifa za kuandikishwa katika Uchaguzi wa Zanzibar. Kwa hivyo, kama walivyoeleza wenzangu takriban wale ambao waliokoseshwa sifa ndio wale Wazanzibari halisi, yaani tunawashuhudia kwenye majimbo yetu.

Kwa mfano, jana amekoseshwa sifa hiyo na leo anaambiwa anao uwezo wa kuchagua viongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wenzangu wameeleza kwa urefu. Lakini napenda kusisitiza kwamba sheria hizi tulizonazo na hususan Sheria ya Uchaguzi kwa kweli imeshapitwa na wakati.

Kutokana na kilio hiki ambacho wawakilishi tumekuwa tukizungumza pamoja na mageuzi haya tuliyonayo ya kisiasa katika nchi yetu, basi kuna umuhimu mkubwa serikali kulifikiria suala hili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi baada ya kusikia kelele hizi pamoja na vilio vingi, nini msimamo wa serikali katika kuzirekebisha sheria hizi ambazo zinaonekana dhahiri ni sheria za kibaguzi za wananchi katika nchi yao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atuelezee msimamo wa serikali, namna ambavyo inaweza kuzifanyia marekebisho sheria hizi ambazo za kuwabagua Wazanzibari katika nchi yao *(Makofi)*.

Mhe. Spika, suala la tatu ni kuhusu Idara ya Uratibu. Kwa kweli tumekuwa kipindi chote tukizungumzia Kero za Muungano zinaathiri nchi yetu kisiasa na kiuchumi.

Nadhani nimuulize Mhe. Waziri Kiongozi kupitia kwako Mhe. Spika na atakapokuja kufanya majumuisho anieleze, kwamba serikali imeweka muda gani au ina mkakati gani wa kuhakikisha kero zilizomo kwenye kapu haziongezeki. Vile vile hizo zilizomo kwenye kapu ni muda gani umewekwa na serikali lini kero hizo zitakuwa zimeshapatiwa ufumbuzi. Kwa sababu kuendelea kila siku miaka nenda rudi na kuambiwa kero inatatuliwa nusu au robo kero, lakini zikawa zinaendelea hili halifurahishi *(Makofi)*.

Kwa hivyo, tunataka serikali ituambie lini au ni muda gani maalum uliowekwa na serikali, kwamba ikifika kipindi hicho kero zote za Muungano zilizopo zitakuwa zimeshapatiwa ufumbuzi, ili tuone kwamba tunaendelea kuwa kwenye muungano ambao wenye ridhaa pamoja na amani kwa pande zote mbili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia ni tatizo la wataalamu. Kwa kweli tumekuwa tukisisitiza Maendeleo katika Sekta ya Elimu, lakini tunalo tatizo jengine ambalo sidhani sijui kama hatujaliona au vipi, kwamba wataalamu wetu kukimbia nje ya nchi. Kwa uzito wa suala hili Mhe. Spika, serikali inapaswa sasa kulitangaza suala la kutoroka kwa wataalamu kwamba ni janga la kitaifa *(Makofi)*.

Kwa sababu serikali inakuwa ikitumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kusomeshea watu, sasa watu wanaosomeshwa wingi kati yao kwa kweli hawarudi katika nchi. Hali hii yote ni kutokana na kwamba serikali haijajenga

mazingira mazuri ya kuhakikisha kuwa wataalamu hao wanabakia ndani ya nchi *(Makofi)*.

Naomba kumuuliza Mhe. Waziri Kiongozi kupitia kwako Mhe. Spika, je serikali inazo takwimu kamili juu ya suala hili, yaani ni watu wengi, kwa sababu wako wengi wataalamu ambao wako nje ya nchi aliondoka miaka ya 1960 na kuendelea 1970 pamoja na mingine. Lakini katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita anazo takwimu zozote zinazoonesha ni watu wangapi waliopelekwa masomoni na wameshindwa kurudi katika nchi *(Makofi)*.

Kwa hivyo, naomba hilo anijibu wakati atakapokuja sambamba na kunielezea mipango ya serikali iliyonayo ya kuhakikisha kwamba wataalamu wetu tunawatunza katika nchi. Kwa sababu Mhe. Spika hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa amekwenda masomoni na halafu hataki kurudi katika nchi yake kwa ajili ya kufanyakazi, lakini tatizo mazingira yaliopo yanawalazimisha watu kukimbia.

Sasa je, serikali imeshaliona hili na kama imeshaliona, hivi haioni kwamba wakati umefika wa kuandaa mazingira maalum ya kuhakikisha kuwa tunawabakisha nchini wataalamu wetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mwenzangu amezungumza hivi kweli kumuekea mtaalamu au kuna mpango wa kuhakikisha kuwa wataalamu wetu wanapata vyombo vya usafiri.

Kwa mfano, tulipokwenda Malaysia Mhe. Spika, hili hatutosita kulieleza, kwa sababu kule serikali imeandaa mpango maalum vijana wote wanaomaliza pale wanao utaratibu wa kupatiwa nyumba, sasa hili haliwezekani katika nchi yetu. Kwa kweli ninaamini ikiwa wataalamu wetu watapatiwa nyumba, vyombo vya usafiri pamoja na mambo mengine, basi wataalamu wataamua kubakia katika nchi.

Mhe. Spika, kuhusiana na Mfuko wa *Constituency Development Fund (CDF)* naunga mkono kama walivyounga mkono wenzangu kuhusu mfuko huu. Kwa sababu Mfuko huu utakuwa ni ukombozi wa majimbo yetu pamoja na maendeleo katika nchi yetu.

Lakini tatizo kubwa lililojitokeza ni *formula* ambalo mimi ninaloliona mpaka hivi sasa, kwa sababu takriban kazi tunazozifanya wawakilishi na wabunge katika majimbo yetu ni kazi za kuisaidia serikali katika kuleta maendeleo. Kwa hivyo, sote tunahakikisha kwamba penye barabara, maji, umeme sisi wawakilishi tunakuwa tunafanya, kweli lakini uwezo wetu ni mdogo. Kwa

manaa hiyo, ufumbuzi wa *CDF* utasaidia kwa pamoja, yaani wawakilishi na serikali kwa jumla.

Kwa kusema mfuko huu uingiziwe fedha za miradi midogo midogo ya wananchi kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, nadhani itakuwa hatujafanyakazi, yaani kutakuwa na ugomvi huko majimboni.

Mhe. Spika, hivi karibuni Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi alituambia kila jimbo lilitengewa shilingi 10 milioni kwa mwaka. Hivi kweli shilingi 10 milioni kwa mwaka unakwenda kuzipeleka kwenye jimbo kwa *formula* ipi, kwamba kila mwezi nipelekea kiasi gani.

Nadhani hata katika Bajeti ya Serikali tufike pahala tuiangalie na ikiwezekana lile fungu liongezwe kwa ajili ya ule mfuko kuwa mkubwa na hata wenzetu wabunge watakapoingiziwa, basi isije ikatutahayarisha sisi wawakilishi. Kwa sababu inawezekana wabunge kwa mwezi wakaingiziwa shilingi 10 milioni, lakini sisi bajeti yetu kwa mwaka ndio shilingi 10 milioni.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi kupitia kwako Mhe. Spika, alizingatie vizuri, angalau tuweze kwenda vizuri kuhusiana na Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nitoe pongezi kwa Mifuko ya *TASAF*. Kwa kweli imefanyakazi nzuri sana katika majimbo yetu. Kwa hiyo, naomba Mhe. Spika, kwani haipendezi mwakilishi kuzungumza hapa kwamba kuna mradi fulani unafanywa ndani ya jimbo lake ikawa hajui.

Sasa ombi langu ni kwamba chochote kinachofanywa na serikali kwa wananchi, basi kama sikushirikishwa kwa mwakilishi angalau taarifa mwakilishi apewe, ili afahamu nini kinachoendelea ndani ya jimbo lake.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi, na kumshukuru pamoja na kumpongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi katika utendaji wake kwa kipindi cha miaka kumi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, ahsante kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii, halafu nimsifu Mhe. Waziri Kiongozi kama vile alivyosifiwa.

Vile vile niwashukuru watendaji wake Mhe. Waziri Kiongozi wamefanyakazi vizuri. Nilikuwa nimeweka kama *points* nne lakini siwezi kuzigusa kutokana na wakati.

Lakini moja kati ya hizo ambazo nitazizungumza ni kwenye ukurasa wa 19 kifungu 13.0 kuhusu Biashara ya Utalii. Mhe. Spika, biashara hii kwa maelezo yake hayaoneshi kama maelezo haya yametoka hapa, nafikiri yametoka kwenye ukusara ya 9. 12.0 kuhusu Mfumko wa Bei. Kwa sababu hapa imezungumza vizuri na baadaye ikarukia hii Biashara ya Utalii na maelezo ambayo yako huku hayafanani na mazingira yaliyowekwa.

Mhe. Spika, ninachokusudia kuzungumza Biashara ya Utalii kama ilivyozungumzwa ni nzuri tena inayo faida. Hata hivyo, biashara hii hivi sasa inatuharibikia sana kwa sababu karibu wiki mbili mfululizo wananchi wanapiga kelele kutokana na mambo ambayo wananchi wanafanyiwa. Kwa mfano, kuna watu wale ambao *suppliers* wanaopeleka vitu vyao na wale wanaoitwa *PO* na wengine, basi wanakusanya zile fedha zinapofika kama shilingi 200 au 300 ama 400 milioni wanaondoka nazo.

Kwa hivyo, pale haiangalii utalii wenyewe isipokuwa serikali, ijapokuwa kila mtu ameambiwa abebe mzigo wake mwenyewe. Lakini mbebaji mkubwa ni serikali, ambayo inaongozwa na Mhe. Rais na msaidizi wake mkubwa ni Mhe. Waziri Kiongozi. Mhe. Spika, huo sio mchango, isipokuwa ni agizo naomba lifanyiwe kazi.

Jambo jengine ambalo nataka nizungumze ni ukurasa wa 21 kama nitawahi. Ukurasa huu unazungumzia kuhusu uwezeshaji wa wananchi. Kwanza mimi nilikuwa mkali tena mkaidi kutokana na hali hii hasa kwa Mifuko ya JK na AK. Kwa kweli mifuko mizuri na inafanyakazi zake vizuri na tayari wananchi wanafanya shughuli za biashara kutokana na mifuko hii na zinakwenda vizuri.

Jambo la msingi linalohitajika kwamba sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuelewe kwamba mifuko ile ni mizunguko. Sasa kama ni mzunguko fedha tayari zimeshagaiwa na kinachosubiriwa hivi sasa marejesho, ili wengine wapate fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

Kutokana na hali hiyo, sisi kama wawakilishi tuwe mabalozi wakubwa wa kusimamia urejeshwaji wa mifuko yenyewe, kwa ajili ya kupewa watu wengine na kuweza kuendesha shughuli zao *(Makofi)*.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lisilisahau ni Tume ya Uchaguzi. Tume hii imeundwa kwa mujibu wa sheria kama ilivyozungumza hapa. Lakini nimeanza

kuwa na wasi wasi mkubwa sana, kwa sababu tume hii jana iliguswa kwa kulaumiwa na wala si jambo zuri.

Kwa kweli tunaamini kwamba tume hii imeundwa na wajumbe wake wametoka pande zote mbili na sote tunawaamini, yaani CUF wametoa wajumbe ambao wanaowaamini na CCM vile vile. Mhe. Spika, mpaka hivi sasa tume hii inakwenda vizuri sana, maana katika mambo makubwa kwenye uchaguzi ni kusimamia daftari, kila mtu anasifu kwamba daftari limepita katika majimbo la limefanya vizuri sana *(Makofi).*

Sasa tukiilaumu tume bado tunaondoa imani ya tume kwetu sisi na wala haipendezi. Kwa sababu tume iko huru na inatakiwa isimamie haki na uadilifu, ambapo inafanya hivyo.

Lakini tume imeongezewa mzigo ghafla, kwa sababu mpaka yanatengenezwa mambo ya daftari na mengine bado hayajaja mapendekezo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, sasa ilipokuja hapo ndipo tume ilipotwikwa mzigo. Kwa hivyo, kosa litakalofanywa na tume itakuwa si la tume, isipokuwa la serikali, kwa sababu tume haikuwa na muda wa kufanya chochote zaidi ya kuyatarisha *ballot* ya kusema ndio au hapa ninavyofahamu mimi.

Kwa sababu mimi kama CCM ambaye ni kiongozi wa jimbo mpaka leo sijapata mafunzo kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, yaani ijaiona semana wala kongamano. Kwa hivyo, tume haipaswi kulaumiwa isipokuwa tuilaumu serikali, kwamba imekubali kufanya maamuzi ya kupitisha sheria hii kwa muda mdogo. Kwa maana hiyo, lazima hapa naona uwepo ule uvumilivu wa kisiasa, kama si hivyo basi tunaweza kuharibikiwa sana *(Makofi).*

Mhe. Spika, nathubutu kusema hili jambo kwa sasa ni jipya tena ni gumu tofauti na tunavyoliona. Kwa hivyo, tunahitaji tuwe makini sana kwa mwaka huu, kuona kwamba mwaka huu ni kama zoezi tu, lakini mchezo mwaka 2015. Lakini tukianza leo kuilaumu tume, basi tunaweza kuisababishia ione kama haina mtetezi katika Baraza hili.

Kwa hivyo, napenda sana tuone kuwa jambo hili ni jipya tena ni gumu na muda mdogo. Maana yake kwenye yale mapendekezo ya zile *draft* za mwanzo tuliona tuchague wakati gani unaweza kuwa mzuri kwa kupiga Kura ya Maoni. Mapendekezo ya mwanzo mengine yalisema kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010, wengine walisema ndani ya uchaguzi wa mwaka 2010 na wengine walisema baada ya uchaguzi wa mwaka 2010.

Lakini kwa busara za Mhe. Rais kama alivyoachiwa imeonekana ifanywe kabla. Sasa nadhani itizame siku ambazo tume imezipata kutayarisha jambo.

Kwa hivyo, lazima tuvumiliane na zile kasoro ndogo ndogo tusiziingize na wala kuzisema sana, kwani tunaweza kutibuwa hali ya hewa ya kisiasa, maana Mhe. Hija Hassan Hija inazungumzwa tume pamoja na CCM niko kimya *(Makofi)*.

Kwa kweli bado tunataka ile nia yetu ya kuwa tunakwenda na jambo hili kwa utulivu iwe ipo. Sasa tukianza kuiletea hoja tume na kuilaumu bila ya kuilaumu serikali ni jambo ambalo halipendezi. Kwa sababu muda iliopata Tume ya Uchaguzi ni mdogo mno na sijui kama watakuwa na nafasi ya kufanya semina, mikutano pamoja na makongamano, maana hili si jambo rahisi sana kama tunavyoliona, kwani kila mtu anao mvuto wake katika hili.

Mhe. Spika, usinitizame sana ukafikiri kama nalipinga, isipokuwa nalikubali sana na wala wenzangu wasiwe na wasi wasi na mimi, yaani CCM. Vile vile ningependa sana wale ambao wanaotoa michango yao msiwasifu wala msiwaponde. Maana kuwasifu kwao inawezekana mnawaponda maeneo mengine na kuwaponda kwao mkawa mnawasifu kwa maeneo mengine *(Kicheko/Makofi)*.

Nadhani ni vyema kila mtu atoe mchango wake aone kwamba anatoa mchango wake kwa ajili ya kuisaidia tume na tuweze kufika kule ambako tunakusudia.
Mhe. Spika, naangalia sana dakika zako, ili nisiweze kuzipotena kwani ninayo mengi. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

**Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak:** Mhe. Spika, ahsante kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, ninatajaribu kuzungumza na kwa yale ambayo tayari yameshazungumzwa sitoyarejea tena kutokana na muda wako. Naomba nianzie kwenye ukurasa wa 31 kuhusu Baraza la Wawakilishi. Kuna sehemu inayozungumzia kuwapatia wafanyakazi 16 wa Baraza la Wawakishi wamepatiwa mafunzo. Lakini nilipoangalia kwenye kiambatanisho N0. 5 kwa kweli sikufurahi, kwa sababu tunalalamika wanawake hatutendewi haki.

Kwa hivyo, baada ya kuona hapa yaani jinsi ya ratiba iliyowekwa imeeleza tu, Shahada wa Falsala, Udaktari wa Sheria Chuo Kikuu, Shahada ya Pili ya Sera ya Maendeleo Chuo Kikuu, lakini sikufahamu katika mafunzo haya wamo wanawake waliopatiwa mafunzo haya, jambo ambalo siku zote tunasema kwamba wanawake nao wapewe kipaumbele.

Kwa maana hiyo, kwenye maandishi haya sikujua miongoni mwa hao waliopatiwa mafunzo wao wanawake. Mhe. Spika, anataka kujua miongoni mwa hawa wafanyakazi 16 wamo wanawake walioshirikishwa kwenye mafunzo haya.

Nikiendelea niende kwenye ukurasa wa 25 sehemu ya Mazingira. Ukurasa huo unaeleza kwamba kuna kifusi na kokoto kando kando ya fukwe unaosababishwa na mmong'onyoko wa ardhi na kupanda kwa kina cha maji. Mhe. Spika, tafiti nyingi zimeonesha kwamba kupanda kwa kina cha maji ni kupanda miti.

Lakini kuna suala moja ambalo napenda kumueleza Mhe. Waziri Kiongozi, ambapo kuna usemi ambao umeenea huko mitaani na sijui kama kweli au vipi. Kwa kweli hivi sasa kumeonekana kuna majani ambayo yanaitwa mlakasa, majani haya yakipandwa pembeni mwa bahari wanasema maji ya bahari hayafiki.

Mhe. Spika, ninaomba suala hili lifanyiwe utatiti na kama taarifa hii wizarani ipo sawa, lakini naomba lifanyiwe utafiti na baada ya kufanyiwa utafiti naomba ichukuliwe hatua muafaka. Kwa sababu hali hii imeshakuwa ya hatari kwamba maji kila siku yanapanda juu na ardhi kuliwa na bahari.

Kwa hivyo, majani haya kwa hapa petu nimesikia yapo Paje na inaonekana watu wa Paje wanayatumia katika kuyapanda kwenda bahari yao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 21 kuhusu suala la Wazalendo waliogundua dawa ya kuulia wadudu wa embe. Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba dawa ya wadudu tayari imeshafanyiwa utafiti na hawa wataalamu wapo.

Sasa ninataka kujua wataalamu hawa katika utoaji wa taaluma ya dawa hii wako pahala gani au wataalamu hawa wanawafuata wakulima kwenye mashamba. Kwa sababu tayari dawa imeshapatikana, mimi nasema imeshapatikana. Kwa kweli siwezi kudharau kwa sababu Mwenyezi Mungu akitaka kitu kuwa basi chochote kinakuwa, pia unapokutwa na shida chochote unaweza kuambiwa ujaribu na pengine kile utakachokijaribu na ndio ikawa mafanikio kwako.

Mhe. Spika, nataka kujua hasa wataalamu hawa wanayo sehemu maalum ambayo wapo, kwa sababu ni wataalamu Wazalendo bila ya shaka tujua wanayo afisi yao maalum au wanawafuata wakulima kwa ajili ya kuwapa taaluma hii. Vile vile taaluma hii waliyoipata wanaendelea kuitoa kwa watu au

wameshagundua na wamekaa tu, kwa sababu inawezekana isiwe kama mtu mtibabu.

Kwa mfano, kuna waganga wengine wakishapata dawa na kujua hii ni dawa basi anakaa nayo mwenyewe mpaka mauti yamemfika hakuna aliyerithi. Kwa hivyo, inabakia kusema babu fulani alikuwa akijua dawa ya maradhi fulani, lakini ndio imeshakwenda.

Kwa maana hiyo, ninachotaka kujua wao hii taaluma waliyoipata juu ya kufanya utafiti wa dawa hii, wanaendelela kuitoa kwa ajili ya kuwafundisha watu au imebakia wanayo wenyewe *(Makofi)*.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu Idara ya Maafa. Kwa sababu juzi liliulizwa swali hapa kuhusiana na Idara ya Maafa kwamba mtu wakati anapopata maafa na kuchelewa kupata msaada. Jibu likaja kwamba inasababishwa na ucheleweshaji wa taarifa.

Nadhani nitoe ushauri kwamba hali inaonesha kuwa hakuna taaluma, pengine kuna mwananchi ambaye hajui hata akikutwa na maafa aanzie au apite wapi. Kwa hivyo, ninaomba taaluma hii itolewe kwa wananchi kwa lengo la kufahamu wakati anapopata maafa apite au aende wapi.

Vile vile itolewe taaluma kupitia shehia ili wajue wakati yanapotokea maafa wajue wapi pa kupeleka taarifa, yaani kwa wahusika, kwa ajili ya kuweza kusaidiwa kwa haraka iwezekanavyo na wala sio umeshapita muda wa miezi 6 ndio anasaidiwa. Kwa kweli hali kama hii itakuwa haipendezi na wala hailete *impact* mazuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema sina mengi na nimalizie suala la mwisho kuhusu Kura ya Maoni. Mhe. Spika, niwaombe wanawake wenzangu kama tunavyojua kwamba Mwenyezi Mungu ametujaalia sisi wanawake ndio tunaokabiliwa na matatizo yote. Kwa mfano, linalotokezea janga au maafa sisi ndio unaoathirika sana.

Kwa hivyo, ninaomba itakapofika wakati wa kupiga Kura ya Maoni, basi wanawake wote ambao tunao uchungu na tumeshajua kwamba matatizo yanatukuta sisi. Kwa maana hiyo, tuamue kura yetu katika mwafaka mzuri, ambao utapelekea nchi yetu katika mustakabali mzuri pamoja na maisha ya kupendeza, kwa ajili ya kuishi sisi na watoto wetu, kwani sisi ndio walezi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tuseme ukweli mimi ninaye babu yangu mmoja alinipa hadithi na mpaka leo yupo Ndijani, alisema kwamba sisi za Mapinduzi mke alikuwa na

mtoto mdogo, basi walipokwenda kujificha yule mtoto analia alimwambia mtupe mtoto tutapata mwengine. Mke alimwambia mume wangu unaniambia vipi, alisema mtupe mtoto tutapata mwengine. Kwa hivyo, mama yule alimwambia mimi mwanangu simtupe nitakufa naye ubavuni *(Makofi)*.

Kwa maana hiyo, tuona wakati wa maafa hata wanaume wanatukimbia wanawake. Kwa hiyo, alimkimbia mkewe na kumuacha kwenye kichaka pamoja na mwanawe, alimwambia kama kufa nitakufa na mwanangu.

Kwa kweli babu yule aliondoka na kumuacha na mwanawe pale, mpaka Mwenyezi Mungu alipomjaalia kupata nafasi na kutoka, huyo mtoto mpaka leo yupo na tayari ameshaoa na kuzaa. Kwa hivyo, hii inatosha kuona kwamba sisi tumechoka na matatizo katika nchi hii.

Mhe. Spika, nakushukuru sana *(Makofi)*.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba radhi kidogo nilipitikiwa kumbe leo ni siku ya Ijumaa, nilimtaja Mhe. Haji Mkema Haji kwamba tunakwenda mpaka saa 7:00 na leo mwisho saa 6:00. Hata hivyo, tutatenga muda kidogo kama dakika 15 jioni, kwa sababu Mhe. Haji Mkema Haji nimekuja, basi uweze kusema machache.

Baadaye tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, ambaye anataka kufafanua baadhi ya mambo katika hotauba hii. Vile vile Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kabla hatujamwita Mhe. Waziri Kiongozi mwenyewe.

*(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika,** nilitaka niwasikie Waheshimiwa wangu hasa wanawake wanaosema kwamba wanawake hawaletwi katika shughuli sijui pana nini hapa leo.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa upendeleo huo nafikiri nitazitumia hizo dakika kikamilifu, kwanza mimi naunga mkono hoja hii ya Hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi. Mimi ni mmoja katika wajumbe wa Kamati ya Katiba na Utawala ambayo tuliipitia, kwa hivyo sina sababu ya kutoiunga mkono, sasa naendelea kuiunga mkono. Lakini nimesimama nina

machache tu ya kuongezea mbali ya ile hotuba ya Mwenyekiti wetu ambayo aliisoma jana.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na Idara ya Uratibu, hizi siku mbili tatu ilikuwa hukuniona hapa lakini ni Idara hii kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi ilitupa mwaliko kwenda kuona kazi za wenzetu wa TASAF kule Mrima. Nashukuru nafasi hiyo tumeitumia vizuri na nina haki ya kusema yale niliyoyaona hapa. Kwanza tulikwenda kujifunza namna gani wenzetu wanavyoibua miradi mfuko ule ni mmoja na una lengo la kupunguza umasikini. Je, shughuli zetu zinafanana, kiufupi nimeona zinafanana na Mkoa niliopata kuutembelea ni Morogoro katika Wilaya ya Ngomero kata ya Turiani na Mzumbe, tumeona miradi kama ile ambayo wananchi wetu wanatekeleza ya kupunguza umasikini ya kijamii pamoja na uzalishaji.

Mhe. Spika, nimejifunza zaidi wenzetu katika miradi hiyo wameenda mbali zaidi wanatumia chini ya mradi huu kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili viweze kuwasaidia ajira na kipato pamoja na kutoa motisha kwa wazalishaji, kama pale Mzumbe tumeona kiwanda cha kusindika matunda hiki kwanza kinatoa ajira, lakini pili wakulima wamepata soko na tatu kitasaidia wakulima kupata motisha kuongeza kwa sababu wanapozalisha wanajua wapi bidhaa yao waweke. Kwa hivyo nililojifunza na ambalo nataka kulileta kwetu kuona TASAF III itapo kuja na ishaala itakuja kwa sababu tumefanya vizuri basin a sisi tuelekee huko katika njia ya kupatia ajira, lakini pia motisha kwa wakulima wetu wazalishe pamoja na kuhakikisha tunajitegemea kwa vifaa ambaavyo tunaweza kuzalisha hapa tutokane na kuagizia kutoka nje.

Mhe. Spika, nina mengi lakini nasema hayo kidogo tu yatosheleze. Lakini pia nashukuru kwa kupata mradi wa TASAF katika jimbo la Koani mradi wa maji wa shehia ya Ubago, Kidimni na Koani mradi huo umekwenda vyema lakini kwa masikitiko makubwa tumekwama kwenye mchango wa SMZ. Fedha zote ambazo zilikuwa zikihitajika na TASAF zimetolewa lakini mchango wa serikali bado haujamalizika kwa hivyo ule mradi haujaweza kutosheleza kukidhi mahitaji ya wananchi kama ilivyokusudiwa.

Lakini pia mradi kama huo tuliupata Bungi matatizo yaliyopo mitambo ipo lakini watuamishi au wafanyakazi wahudumu hawapo kwa hivyo huduma ile haipatikani. Umeme upo, mashine ipo lakini wahudumu wale *pump operator* hawapo kwa hivyo hatupati maji, nimemsikia Mhe. Waziri wa Fedha Dk. Mwinyi kuwa mwaka huu watafungua ajira kwa hivyo ningeomba wale wahudumu wa maji katika jimbo la Koani ili dhiki ya maji tuepukane nayo.

Baada ya hapo niwashukuru watendaji wote wa TASAF namna wanavyotekeleza hasa katika kutunza mahisabu yao na hata wahisani au

wanaosaidia watu wa *World Bank* wameridhika na shughuli zetu na wana nia ya kutuongezea TASAF III na *ishaalla* tutaitumia vizuri itakapofika.

Mhe. Spika, nije Idara ya Mipango ambayo tumetembelea wakati wa Kamati tumeona ujenzi wa nyumba yenye Ofisi kule Pemba nzuri nawapongeza, lakini pia makazi ya Waziri Kiongozi atakapokuwepo Dar es Salaam tumekuta kijumba kizuri sana lakini tangu tumepewa hatujawahi kuitumia, ningeliomba Mhe. Waziri Kiongozi kabla hajamaliza muda wake japo siku moja ile nyumba akalale, mimi nimekwenda na Mhe. Najma Halfani pale tulisema labda tubakie mna fanicha na kila kitu lakini yeye mwenyewe bado hajabahatika. Nyumba safi kabisa na ikikaaa tupu anaweza kukaa shetani kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri Kiongozi nyumba ile akaitumia japo kwa siku moja.

**Mhe. Spika:** Kwa hivyo ukaona ukae wewe na Mhe. Najma Khalfani *(Kicheko).*

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, tulikwenda kama wajumbe wa kamati. Lakini jengine niungane na wajumbe wenzangu katika afisi ya huduma za Waziri Kiongozi hasa kuhusu usafiri, tungeliiomba serikali ikalitizama suala la usafiri haliridhishi, hii gari anayotumia hapa Makao Makuu, Pemba ndio kabisa anaazima, akienda Dodoma anakodi, ukweli haileti heshima kwa kiongozi wetu mkuu kama hivyo, anapokuwa na wageni kama kule Dar es Salaam au kafuatana na mama amkodie TAXI, huu si utaratibu unaofaa. Kwa hivyo naomba kwa hili ni mambo ya ndani tujirekebishe tuweze kumtengenezea mazingira mazuri Mhe. Waziri Kiongozi aliyeko.

Mhe. Spika, sasa hivi huko majimboni kuna kitu kinaitwa CDF na sisi kwa upande wetu wawakilishi tulikililia siku nyingi lakini kimekuja kimya kimya na kienyeji mno kwa sababu CDF haikuja hivi imekuja na sheria iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, utaratibu tuliojiwekea Mhe. Spika, sheria yoyote inayotungwa na Bunge na ambayo itahitaji kutumika Zanzibar ipate iridhiwe sasa sijui kwa sababu ina pesa kwa sababu imekuja na bahasha. Hivi sasa kuna migogoro ya pesa zitumike vipi lakini sisi tutaitumia katika uhalali upi? Kwa sababu sheria ile inataka kufanya kazi hapa Zanzibar na watumishi wa SMZ ndio watakaohusika kudhibiti pesa hizo, yaani Makatibu wa Halmashauri, Maafisa Mipango wa Halmashauri, Madiwani wetu sasa hapa nina suala naomba kumuuliza Mhe. Waziri Kiongozi.

Hizi pesa za CDF chini ya sheria ya Jamhuri ya Muungano itafanya kazi bila ya sisi hapa kuridhia hilo la kwanza, lakini la pili ile sheria bila ya kuridhiwa hapa na sisi tukatoa maoni yetu italeta matatizo baadae, kwa sababu ndani ya mfumo wa CDF kunataka kuibuliwa miradi ya maendeleo katika jimbo na kuna kamati maalum mwenyekiti wake Mbunge lakini Mwakilishi sheria haikumtaja. Sasa

wewe Mwakilishi uko katika jimbo lile uende ukachungulie tu watu wanavyofanya vile kabisa itatuweka katika idhilali na unyonge.

Kwa hivyo hiii sheria kama ingeletwa kwanza na sisi tungetengeneza utaratibu pale palipoandikwa Mbunge basi tukatia na Mwakilishi kwani shughuli zetu huko huko baadhi tunafanya pamoja, sasa madaraka yale anapewa mbunge wewe unaonekana mikono mitupu, tena mjumbe wa kualikwa wanaweza kukualika au wasikualike hiyari yao. Haikumtaja Mwakilishi katika sheria hiyo, mimi ningemuomba Mhe. Waziri sheria hii tufanye utaratibu wetu madhali ya Muungano ije kwenye Baraza turidhie na turekebishe kabla na sisi hizo pesa hatujazitia.

Lakini pia niungane na wajumbe pesa ambazo zinataka kutiwa kwa sababu ya miradi midogo midogo fungu hilo liongezwe, kwa kuanzia mimi nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi zile milioni mia sita tuzianzie tu, kwa kuanzia nimekubali lakini baadae baraza jipya lifanye *supplementary budget* ili kima kile kiongezwe na miradi ya wananchi iweze kutekelezwa ipasavyo.

Mhe. Spika , jambo jengine ni kuhusu vikao vya pamaja taarifa nyingi tunapata Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora katwambia mafanikio, Mhe. Waziri wa Nchi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi katupa mafanikio ya vikao hivyo, Mhe. Waziri Kiongozi anatupa mafanikio hayo. Lakini yale yaliyokubalika sasa hivi yameshakuwa rasmi yameandikwa au yamezungumzwa kwenye kikao pale na tumeondoka tu tumekubaliana halafu baadae kwenye utekelezaji hayapo. Mimi nina wasi wasi yale yote ambayo yamekubaliwa bora yaletwe hapa rasmi tena yatiwe saini na viongozi na kama kuna sheria zilizohusika na mambo yale zirekebishwe hapo mimi ndio nitaamini, laa si hivyo mimi sijakubali kama kumefanyika mabadiliko yoyote au kumefanyika kitu.

Lakini Mhe. Spika, katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri katika ukurasa wa arubaini na saba kifungu cha nne kimeelezea kero ya benk na mpaka sasa hivi kunataka kufanywa kikao cha kutoa nyaraka, jambo hili lina miaka mingi zaidi ya miaka kumi na tano linazungumzwa hizi nyaraka hazijapelekwa sijui zinatoka mbinguni, miaka kumi na tano tunazungumzia habari ya benki sasa ndio tunatafuta siku ya kwenda kupeleka nyaraka hatuko *serious* Mhe. Spika, na pesa ndio roho ya serikali na ndio roho ya wananchi katika kuleta maendeleo na pesa ndio fitna mpaka Mwenyezi Mungu kavitaja vitu vya fitna navyo ni pesa, mtoto na mke vitu hivyo vibaya vina fitna na hapa tunazungumzia pesa kwa hivyo tusiache maneno ya Mwenyezi Mungu kuwa pesa fitna tuna miaka kumi na tano tunagombania benki na nyaraka

hazijapatikana ndio kwanza zinapangiwa terehe hili naona hatuko *serious.* Kwa hivyo hili nasema ni kero kubwa.

Mhe. Spika, niishukuru Tume ya Uchaguzi kazi zake nzuri.

**Mhe. Spika:** Una dakika mbili tu.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Ahsante Mhe. Spika, nashukuru waendelee na moyo huu kwa sababu tumewapa majukumu juu ya majukumu na kura za maoni, nawaomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa kazi nzuri tufanye uchaguzi wetu tutoe maoni yetu kwa salama na amani.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru wewe kunipa muda huu kwa upendeleo lakini nimshukuru Mhe. Waziri juu ya hotuba yake na kwa niaba ya wananchi wa Koani naunga mkono mia juu ya mia. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi. Na mimi niungane na Waheshimiwa walionitangulia kumpongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi , Katibu Mkuu na watendaji wote wa Afisi hii kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya uratibu na kusimamia shughuli zote za Serikali, sio kazi ndogo na ni kazi inayohitaji umakini, ujasiri na wepesi kabisa wa kufanya shughuli hizo.

Kwa kweli tunawashukuru sana na tukiangalia Afisi ya Waziri Kiongozi kila Wizara sisi tunapenda mambo yetu yafanikiwe vizuri basi tunapenda Afisi ya Waziri Kiongozi iingilie kati kwa sababu ya huo uliosema uratibu wa shughuli nzima, barua nikiandika mimi pengine kwa Wizara nyengine haina uzito kama angeandika Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa hivyo uzito wa afisi hii sote tunauona na tunaukubali.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Dimani naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja nimejaribu kusimama na kufanya ufafanuzi kwa masuala mawili matatu tu madogo sana na wala sio makubwa.

Suala la kwanza ni lile alilozungumza Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwenye kitabu chetu cha pili kwenye ukurasa wa sabiini na tatu pale tulipozungumzia mikakati ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2010/2011, naomba niweke wazi tu kwamba sio lengo la serikali wala Wizara ya Fedha kuingilia kazi na mikakati ya kazi zake Baraza la Wawakilishi, kwa hivyo sentensi ile kwa neno

moja tu limekosewa na ile ndio iliyopotosha dhana nzima. Sasa naomba niliweke sawa nene moja tu ukiliweka hilo basi.

Kifungu cha pili mkakati wa pili ni kuweka utaratibu utakaoziwezesha taasisi za Serikali kupokea taarifa na maoni kuhusu utendaji wa kamati za baraza, nafikiri baada ya kamati zile kufanya ziara zao tutaweka utaratibu taasisi za serikali wawe na njia nzuri za kupokea hizo taarifa na maoni, kwa hivyo hili neno moja ndio lililopotosha sio kutoa wakati mwengine kompyuta inaruka. Tunaomba radhi kwa hilo haikuwa lengo letu kama ilivyotafsirika.

Mhe. Spika, jengine nataka nizungumze kidogo hili suala la fungu maalum la Baraza la Wawakilishi, hata sisi hii fikra tunaiunga mkono ni nzuri lakini ninachosema wakati wake hatujawa tayari sisi Wizara ya Fedha nasema hatujawa tayari. Kwa nini hatujawa tayari ? Bado Waheshimiwa wajumbe mapato yetu hayajawiva kiasi cha kumgawia kila mtu chake kwa *percentage* bado mapato yetu tunategemea tunachokikusanya, halafu tunachokigawa hivyo ndivyo tunavyokwenda.

Tunafika pahala tuseme ukweli tunapanga lakini tunachukuru kwanza ni mshahara huu tunautoa mwanzo, sasa tukishatoa mshahara tunaangalia kilichobakia ni kipi sasa kile ndio tunakigawa kwa hivyo inabidi tucheze na maturufu Mhe. Spika, huo ni ukweli kabisa, tucheze na maturufu tuone tuende wapi tunaruhusu kufanya bajeti tunawaomba Mawizara watuletee *program* yao ya kazi ule MTEFU halafu tunakaa *committee* tunagawa, tusingependa twende hivyo lakini ndio hali halisi ilivyo.

Labda tukishachimba mafuta yetu tutakuwa na *reserve* nzuri basi hapo tutagawa vizuri Baraza la Wawakilishi *percentage* yako hii na tutaiheshimu *percentage* ile, Wizara ya Elimu yako hii , Wizara ya Fedha yako hii lakini kwa sasa Mhe. Spika, niseme hatujafikia huko. Lakini basi tusivunjike tama nasema hili wazo tumelichukua na tunakwenda kulifanyia utafiti tuone vipi tunaweza kulifanikisha huko mbele.

Mhe. Spika, kubwa ninalotaka kusema tunajitahidi Wizara ya Fedha na Uchumi huko nyuma Mhe. Spika, wewe shahidi na waheshimiwa wengine wamo wa veterani humu wameshapata vipindi viwili au vitatu, tulivyokuwa huko nyuma na tulivyo hivi leo tunajitahidi na asilimia nilizopata kutoka kwa watu wangu wananambia asilimia tisini na nane ya kasma ya Baraza la Wawakilishi imeshatiliwa fedha mpaka hii leo tumebakisha kidogo sana. Sasa hiyo ni hatua nzuri sana ukilinganisha na huko tulikotoka.

Lakini jengine kama nilivyosema juzi wahehimiwa zile karatasi zetu nazo tayari hayo ni mafanikiyo, nikisema hivyo zamani tulikuwa tunakopeshwa sasa

hayo ni mafanikio lazima tukumbuke tulikotoka huko kama nilivyosema kuna wengine maveterani wanajua hali ilikuwaje. Sasa basi waheshimiwa wanasema nisiende zaidi basi siendi zaidi *(Kicheko).*

Jengine ambalo nataka kuchangia kidogo sana ni suala la wataalam kubaki nchini na mimi naunga mkono sana wazo lililotolewa kwamba tujitahidi tutoe senti nyingi kwa wataalam wetu wabaki nchini, lakini ninalotaka kusema ulimwengu wa leo mdogo na ulimwengu wa ushindani wewe mtaalamu unamsomesha unatia pesa zako na degree yake lakini anafungua *internet* kazi iko wapi? Leo yuko Kenya, kama hayupo Kenya yupo Ulaya sio sisi tu lakini nchi zote zinazoendelea tunaathiriwa na tatizo hili. Kuna wenzetu wa Ghana wanalia wanasema wanafundisha wauguzi basi nusu yao wako Uingereza, nilipata stori moja inayosema madaktari wanaosomesha Malawi basi wale waliopo Malawi hawafiki hata nusu yake kwa wale walioko *Manchester* yaani wote wamejikita wako *Manchester* tu peke yake kila anayekwenda kusoma anamalizia Manchester.

Hivi sasa wanajiuliza wafanye nini lakini cha muhimu tutajitahidi serikali yetu kadri tunavyokwenda mazingira ya wafanyakazi wetu tuyaendeleze na hilo tumelianza baada ya kusikiliza maoni yenu waheshimiwa mengi sana, madaktari wetu sasa hivi sivyo walivyokuwa katika miaka miwili iliyopita leo wazuri sana, wazuri mno lazima tujisifu. Wizara ya Elimu nayo tumewatengeneza vizuri sana nayo kama mlivyoshauri *scheme of service* tunatengeneza kwa kada nyengine, kada za kilimo, kada za ma- *engener* na wengine tunajitahidi lakini kila mmoja na ubavu wake lazima tukubali ubavu wetu mdogo. Lakini sio kwamba tuachilie ili wataalam wetu watutoke kama ninavyosema tutajitahidi kadri inavyoyumkinika hali tuiendeleze na fursa tuitoe ili wataalam wetu waweze kubaki nchini mwetu.

Mhe. Spika, mimi nilisema nitoe ufafanuzi mdogo tu sina zaidi lakini nimalizie tu kama nilivyosema naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana *(Makofi)*

**Mhe. Spika.** Waheshimiwa wajumbe nilipenda sana kwamba kila mmoja kati ya wajumbe walioomba wapate nafasi ya kuchangia lakini muda umetukwaza kidogo, kwa hivyo nawaomba radhi weheshimiwa wafuatao kwamba wao hawatapata nafasi ya kuchangia nao ni Mhe. Hija Hassan Hijja, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Asha Moh'd Hilali, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Abass Juma Mhunzi. Hawa nawaomba watusamehe muda kidogo umetukwaza hawataweza kupata nafasi ya kuchangia.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu zaidi nitakaojikita katika michango ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wameitoa kuchangia bajeti yetu hii, lakini vile vile kama kawaida kuna yale mengine mazito basi Mhe. Waziri Kiongozi atakuja kuyatolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura na sisi tunaunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri Kiongozi hotuba ambayo imeonyesha ni namna gani Serikali yetu inavyoweza kusimamia majukumu zaidi katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Nikiendelea na mimi niwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi ambao wamechangia hotuba hii lakini vile vile na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia naamini na wao ukimya wao watakuwa wameridhika na wengine wamekuwa wakituletea vikarasi ambavyo vimetushauri mambo mbali mbali, nitaomba tu kwamba atakapokuja mwenyewe Mhe. Waziri Kiongozi atawataja Mheshimiwa mmoja mmoja kwa wale ambao waliweza kuchangia hii nafasi, mimi ningeomba niende kwa mchango wa mtu mmoja mmoja.

Mhe. Spika, mimi naanza na hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Utawala Mhe. Haji Omar Kheir kwanza tunamshukuru sana kwa pongezi zake kwa Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na sisi wasaidizi wake pongezi hizo tumezipokea, lakini vile vile na sisi kwa upande wetu kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi tunampongeza sana Mhe. Haji Omar Kheir pamoja na kamati yake nzima kwa ushauri na maelekezo na muongozo kwa muda wote tulipokuwa tukifanya kazi katika kamati.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Utawala alitoa maoni yake mbali mbali na nitaomba nitoe ufafanuzi. Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Utawala alijaribu kuelezea kwamba au alishauri kwamba Tume ya Ukimwi iwe wa *program* maalum ya kuweza kufuatilia uhakiki wa fedha ambazo wanapewa *NGO's* ambazo zinajishughulisha na masuala ya UKIMWI katika kuhakikisha kwamba fedha wanazozipata hasa kutoka kwa wahisani wanazitumia vizuri na mahesabu yake yaweze kuwekewa kumbu kumbu. Hili Tume ya Ukimwi tayari ina *program* kupitia UNDP ambayo sasa hivi wamo katika mchakato wa kuanza hiyo kazi ya uhakiki taasisi zote ambazo NGO's zote ambazo zinashughulikia masuala ya ukimwi na zile ripoti zake ziweze kukaguliwa.

Kwa hivyo hili namuomba sana Mhe. Mwenyekiti katika miaka inayokuja kuanzia bajeti ya mwaka 2010/2011 tunayokwenda nayo *program* hii tunakwenda nayo ukweni ni fedha zinazotolewa na wafadhili kwa NGO's zetu

ili kuhakikisha kwamba tunadhibiti maambukizi ya Ukimwi ili ziweze kutumika vizuri na sisi kwa upande wetu kama serikali ni wajibu wetu kuweza kufuatilia kwa karibu.

Mhe. Spika, nikiendelea katika maoni ya Mhe. Mwenyekiti alieleza kwamba kutokuridhika kwake na ukamilishwaji au *finishing* ya ujezi wetu wa jengo la Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba.

Mhe. Spika, hili suala hata mimi mwenyewe nilikwenda Pemba karibu mara tatu kufatilia ujenzi huu. Kimsingi ujenzi ulianza vizuri, mkandarasi alianza kutumia gharama zake. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa hilo, baada ye na sisi kwa upande wetu serikali kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi tulijitahidi tukaenda sambamba na ule mkataba namna ya kuweza kuingiza fedha.

Mhe. Spika, lakini kama unavyofahamu kazi ukishakumkabidhi mjenzi inakuwa kazi ile bado ipo chini ya usimamizi wake mpaka ile siku anayokukabidhi. Lakini bado tulikuwa tunamfatilia kwa karibu, kwa sababu tunaye mtaalamu wetu mzalendo ambaye ni *consultant* wetu ambaye alikuwa akishauri kwa upande wa serikali. Kila hatua iliyokuwa inakwenda tulikuwa tunajaribu kufatilia na zile kasoro tulizokuwa tunaziona tulikuwa tunajaribu kutoa maelekezo iweze kufanyiwa marekebisho.

Mwenyekiti wa Kamati alipokwenda na kamati yake kipindi hicho maelekezo hayo tuliyokwisha kuyatoa na hata Mhe. Waziri Kiongozi mwenyewe alitaka akajiridhishe na hiyo hatua ambayo iliyofikiwa na alikwenda na akamtaka mjenzi kuhakikisha kwamba hayo maelekezo aliyopewa anayafanyia kazi. Lakini vile vile na yeye alitoa maelekezo mengine ya ziada na sasa hivi tunashukuru kwamba mjenzi yule yumo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mhe. Waziri Kiongozi alimpa mjenzi yule mwezi mmoja, kwa hivyo kuanzia tarehe 4 mwezi huu mpaka tarehe 4 mwezi wa 7 ile kazi au kama agizo la Mhe. Waziri Kiongozi linatakiwa liwe limeshatekelezwa na yule mjenzi. Mjenzi yule amekiri kwamba kwa muda huo ataweza kuifanya hiyo kazi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la huduma ya Afisi ya Waziri Kiongozi, akatutaka tuhakikishe Mhe. Waziri Kiongozi anahamia katika nyumba mpya ya Masaki kabla hatujamaliza muda wetu. Suala hili kwa kweli linahitaji fedha kwa sababu nyumba ile kwa hadhi ya Mhe. Waziri Kiongozi nyumba inastahiki lakini ni lazima ndani tufanye marekebisho hasa katika masuala ya fanicha.

Ukiangalia katika kasma zetu sasa hivi kwa fedha ambazo tulizokuwa tumepangiwa kwa kweli hazitaweza kutosha kuweza kumnunua fanicha

kuweza kuingiza katika jengo lile. Tunategemea baada ya kumalizika Bajeti hii bajeti inayokuja tukijaaliwa tutahakikisha fanicha hizo tunazinunua na kabla Mhe. Waziri Kiongozi hajamaliza muda wake wa kutumikia nafasi ya Waziri Kiongozi basi tutahakikisha analitumia jengo lile. Hili nitakuwa nimelijibu pamoja na yale maoni ya waheshimiwa wengine.

Mhe. Spika, mfuko wa maafa, alielezea kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tuingize fedha pale wahisani wanapongiza fedha. Hili alilizungumzia Mhe. Mwenyekiti walipokuwa kwenye Kamati walielezewa misaada tunayoipata kupitia UNICEF, Idara ya Maafa tunapata baadhi ya misaada kupitia UNICEF. Ile programu haitakiwi mchango wa serikali isipokuwa programu ile Mkurugenzi mwenyewe wa Idara ya Maafa kuangalia yale mahitaji wanakuwa wanawaandikia hawa Washirika wa Maendeleo na huwa wanatusaidia baadhi ya vifaa mfano wametusaidia mahema sasa hivi tunayo, wametusaidia madawa tunayo na mengine tumewapelekea Wizara ya Afya. Kwa hiyo hapa hapakutakiwa mchango wa serikali.

Lakini bado tunaendelea kupokea wito wa waheshimiwa kwamba serikali sasa tujitahidi kuanzisha au kuanzishwa mfuko wa maafa ingawa ndani ya sheria umo lakini bado haujaanza kuingiziwa fedha. Sasa hivi tumo katika maandalizi ya sera ya maafa. Wakati wowote hali ikiruhusu, sasa hivi tayari imeshapelekwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu na baadaye itakwenda serikalini na baadaye italetwa hapa kwa ajili ya kuja kuchangiwa na waheshimiwa. Hapo ule mfuko wa maafa utakuwa tayari umeshatolewa maelezo na ufafanuzi wa kutosha na weheshimiwa watatoa michango yao mingi tutakapoleta hiyo sera, Mfuko wa maafa tukijaaliwa utaanzishwa.

Sheria inasema kwamba uanzishwe mfuko wa maafa au kutakuwa na mfuko wa maafa. Lakini mpaka sasa hivi yanapotokezea maafa babo tunaendelea kutumia mfuko mkuu wa serikali ambapo hata Jumuia ya Kimataifa inavyotaka tusitumie katika mifuko yetu ya serikali zaidi tuwe na mfuko wetu maalum. Yanapotokezea maana na wao ule mchango wao waweze kuingiza kupitia mfuko huo. Mhe. Spika, hilo tunaendelea kulifanyia kazi.

Idara ya watu wenye ulemavu alizungumzia kutokuridhika kwake na fedha wanazotiliwa. Idara hii kama tunavyofahamu ni idara changa ambayo imeanzishwa si muda mrefu sana. vile vile hata wafanyakazi wake bado hawajatosha hasa kwa upande wa Pemba ambako katika Afisi tuna mfanyakazi mmoja tu. Lakini tayari maombi yetu tumeshapeleka Tume ya Uchumishi Serikalini.

Hapa tunamuomba sana Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha ambae pia anashughulikia Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi ambaye tume ya utumishi ipo chini ya afisi yake ajaribu kusikia hichi kilio cha waheshimiwa ambacho pia ni kilio cha Afisi yetu kwamba yale maombi yetu ya kuajiri wafanyakazi wa ziada pale Pemba yaweze kufanyika, ili wenzetu hawa kama waheshimiwa wajumbe walipouliza *cansern* zao kwamba Idara ya watu wenye ulemavu. Vile vile hata hao watu wenye ulemavu wenyewe wanahitaji washuhulikiwe kwa ukaribu hasa kutokana na hali yao ya kimaumbile. Hilo nadhani Mhe. Waziri anashuhulikia utumishi analisikia naamini atalifanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Omar Kheri, baadaye alielezea maoni yake binafsi lakini haya nitaomba nije niyazungumze mwisho kwa sababu ni maoni katika suala zima la kura ya maoni na nini ambacho wanachotakiwa wananchi wetu wajiandae. Hili nitakuja kuliweka katika maelezo ya jumla kwa sababu kila mmoja alilichangia kinamna yake.

Mhe. Spika, mchango wa Mhe. Abubakary Khamis Bakary kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alielezea baada ya wazalendo walivumbua dawa ya wadudu wanaoharibu mazao yetu hasa matunda, akajaribu kutoa na kibwagizo kidogo kuhusu suala la mkungumanga kazi yake nini na karafuu kazi yake nini. Hili suala wenzetu Wizara ya Kilimo wamelisikia vizuri na kwa kweli utafiti unaendelea kufanyika, kwa sababu hii dawa imeanza kuvumbuliwa hivi karibuni kwa hiyo ndio inaanza kufanyiwa kazi na utafiti wa karibu ili kujua athari zake na faida zake. Isijekuwa kama alivyosema Mhe. Abubakar kwamba wadudu wanaanza kulewa halafu wakaanza kukazana. Hili kidogo linaweza likatuletea matatizo.

Mhe. Spika, nikiendelea ameeleza katika masuala mazima ya vikao vyetu hasa vya kikanda. Mara nyingi sisi Zanzibar tunakuwa tunasemea, hatujiwakilishi wenyewe kama Zanzibar. Unajuwa kuna taratibu ambazo tayari tumekwisha kujiwekea na kwa bahati mbaya zimejikita ndani ya Katiba yetu katika mambo yote ambayo sio ya Zanzibar peke yake yanapokuja katika mambo ya mashirikiano ya kikanda basi Zanzibar tunakwenda chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pamoja na hayo Mhe. Spika, katika mikutano yote basi takriban hasa katika mikutano ya Jumuia ya Afrika Mashariki na SADEC mawaziri wa kisekta wanakwenda katika vikao vile na ile michango ya Tanzania basi Zanzibar tunakuwa tumeshakaa na wenzetu kabisa Tanzania Bara yale maoni ya Zanzibar yanakuwa tayari yameshatayarishwa na anapewa yule Waziri wa Jamhuri ya Muungano na anayaelezea kwa pamoja. Kwa hivyo hii hata katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki tunakuwa tunashiriki kwa pamoja.

Mimi nadhani hapa ni jitihada yetu sisi kuhakikisha vinapokuja vikao vile basi tusiweze ku- *delay*. Kwa sababu tukiacha kwenda katika vikao vile kwa kweli matatizo ndiyo yanaanza kujitokeza. Kwa masuala ya Zanzibar kama itakuwa hayupo Waziri wa Zanzibar au kama hawapo watendaji wa Zanzibar kwa kweli hapo itakuwa tatizo. Kimsingi takriban mambo mengi katika vikao vyetu Zanzibar tunashiriki kama Zanzibar ingawa maoni yetu yanakuwa yanazungumzwa na Waziri wa Jamhuri ya Muungano.

Nataka nilizungumzie suala moja la *Univirsal*, suala hili limezungumzwa katika Jumuiya ya Afrika Mshariki, lakini Tanzania ilikataa kwa sababu Zanzibar ilikataa. Hata suala la kutumia hizi ID kwamba sasa iwe ndio kigezo kama *passport.* Suala hili aliyeanza kukataa ni Zanzibar kwa hiyo Tanzania Bara nayo ilikataa kwa sababu Zanzibar ilianza kukataa. Mambo mengi yanayofanyika maamuzi basi sisi tunatoa michango yetu na tunashukuru wenzetu mambo mengi tunakuwa tunakubaliana.

Mhe. Spika, nikiendelea mfuko wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Dokta Mwinyi Haji ameutolea ufafanuzi na waheshimiwa wengi wamejaribu kuchangia. Sasa nataka niongeze maelezo ingawa Mhe. Dokta Mwinyi alisema kwa sasa hivi kutokana na hali yetu ya ukusanyaji wetu wa fedha hauruhusu alisema tusubiri tukianza kuchimba mafuta.

Mhe. Spika, suala la uchimbaji wa mafuta linamtiririko mrefu lakini bado hali ya makusanyo yetu ikiwa mazuri. Kwa sababu mfuko wa Baraza la Wawakilishi kwa kweli ni muhimu. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanatakiwa wafanye kazi zao kwa uhuru na kwa uwazi kabisa wanapohitaji taarifa yoyote kwa wakati wowote waweze kuipata kwa wakati. Hili bado tunaendelea nalo na tunalisimamia tukithibitishiwa na wenzetu. Kwa sababu ni lazima tupate maoni ya wakusanyaji wa fedha, tusijetukaanzisha kitu baadaye tukaja tukashindwa njiani.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu kama alivyosema Mhe. Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha. suala kwa kweli tunalikubali na ni muhimu na tukijaaliwa uwezo wa serikali wakati wowote ukiwa mzuri hili suala tutalishuhulikia. Bado naendelea kuomba kwamba tujitahidini tunapotoa michango yetu tuishauri na serikali kuanzisha au kubuni vianzio vipya vya mapato ili mfuko wetu uwe unatuna ili Baraza la Wawakilishi liwe na fungu lake. Kwa kifupi hata mataifa ndiyo yanavyotaka kwamba vyombo hivi vya Baraza la Wawakilishi ni chombo cha wananchi kwamba kiwe kina uwezo wa kuihoji na kuiambia serikali. Huwezi ukahoji kama huna nyenzo za kuweza kumuhojia mtu.

Mhe. Spika, nikiendelea ameeleza suala la Afisi za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi majimboni, Wenzetu wabunge wameshaanza kujengewa. Mhe. Spika, hili na sisi tupo mbioni lakini bado uwezo wa kifedha nafikiri kama mnavyoona, fungu lebo halijatoleza kuweza kujenga Afisi katika majimbo. Mimi naomba kwa yale majimbo ambayo wabunge wameshaanza kujengewa afisi zao basi ni vizuri wakajaribu kuzitumia.

Madhumuni ya afisi zile kwanza kuhakikisha kwamba wale Waheshimiwa wasiwe wanafuatwa majumbani kwao kwa sababu kila mtu na tabia yake, wengine wanakwenda wanatoa maneno kidogo sio mazuri kwa familia za waheshimiwa. Ndio maana inatakiwa waheshimiwa wawemo katika Afisi ili wananchi waweze kutoa shida zao lakini na ni namna gani waweze kuwambia malalamiko yao waweze kuwasemea katika vyombo vya kutunga sheria.

Hili Baraza la Wawakilishi tumejaribu kwa upande wetu jitihada binafsi ukiacha bajeti ya serikali kuna huu mpango wa kujenga uwezo Waheshimiwa yaani DDTP ambao sasa hivi hawa wahesani wetu wa UNDP fedha ambazo wamezitoa wamekataa zisitumike katika ununuzi wa magari na suala zima la ujenzi wa Afisi za waheshimiwa. Isipokuwa wamekubali kwamba fedha hizi zitumike katika kuwajenga uwezo waheshimiwa na ndiyo hayo mafunzo na semina mbali mbali zinatolewa, tumekwenda Pemba tukakaa wiki nzima na Profesa Shibji tukaweza kuchambuliwa Katiba, tukaweza kujua mgongano wa Katiba ndani ya Katiba zetu mbili Jamuhuri ya Muungano na Katiba ya Zanziba. Kwa kifupi fedha hizi ndiyo hiyo kazi ambayo za kujenga taaluma au kuwajenga uwezo waheshimiwa. Kwa hivyo bado ndio tunaendelea na fedha hizo ndio zimesaidia hata kuna badhi ya waheshimiwa kuwapeleka nje ya nchi yetu kwenda kujionea na kujifunza ni namna gani wenzetu wanafanya ili na sisi tuje tuige.

Mhe. Spika, masuala ya papo kwa papo hili wakati wake bado kwa Zanzibar kwa sababu masuala haya ni masuala ambayo unahitaji upate jawabu la uhakika, jawabu ya uhakika kuitoa hapo kwa hapo si kitu rahisi sana. Hili tumeshaanza kuliona kwa wenzetu lilileta matatizo mpaka hapa mtikisiko ulifika mpaka Baraza lilitikisika ulianza Bungeni kwa yale masuala ya papo kwa papo. Kwa sababu kitu unachoulizwa unatakiwa vizuri ukifanyie utafiti unapokijibu ili ukijibu kwa vizuri. Kwa hiyo masuala ya papo kwa papo kwa hapa kwetu nahisi bado wakati wake wakati ukifika huko mbele tukiona sasa hivi tayari basi tunaweza kukalitekeleza halina matatizo. Demokrasia inapanuka.

Mhe. Spika, ucheleweshaji wa pesa za maafa. Hili alizungumzia hasa kwa lile tukiwa la wananchi wa Kilimahewa na  Kwamtipura ni shehia mbili ilikuwa ni siku ya Disemba 9 kama sijakosea. Ulivuma upepo mkali ukaweza kuezua

mapaa ya nyumba ukaleta mtafaruku mkubwa kwa wananchi. Idara ya Maafa ule wajibu wake kwanza ulianza kuutekeleza. Tulikwenda kwa ghafla tukajaribu kuwaona wale wahanga walioathirika, tukaweka kambi kwenye Skuli ya Kilimahewa, tukatayarisha madawa na huduma nyengine muhimu. Kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri wale wote ambao walipata ile athari walikataa kukaa pale kwenye kambi. Moja katika kazi ya Idara ya maafa kutengeneza shelta hapa kwa pale dharura inapotokezea watu wasihangaike.

Tukiangalia katika nchi mbali mbali duniani yanapotokezea maafa kama yale kitu cha mwanzo ile idara inayoshuhulikia na mambo ya maafa iweke kambi ya kuweza kuwahifadhi wale waliothirika wasiweze kupata tabu. Kwa hiyo kazi ya msingi tumeweza kuifanya. Lakini baadaye serikali ikajaribu kutathmini ile athari iliyotokezea na kwa bahati mbaya kipindi kile kile tulikuwa tuna tatizo la umeme, Mhe. Waziri Kiongozi alikwisha kuomba fedha serikalini kwa ajili ya kupewa kifuta jasho au kile cha kuweza kupunguza yale machungu ya athari iliyojitokeza. Ingawa kutokana na kipindi kile fedha nyingi zilikuwa zinatumika katika masuala ya kuhakikisha umeme unapatikana na huduma nyengine pamoja na maji.

Mhe. Spika, ingawa fedha zilichelewa lakini tunashukuru hali ilivyotulia kidogo fedha zilitolewa. Mwezi uliopita Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi tulimkabidhi fedha zile nay eye tayari emeshazikabidhi kwa wananchi. Nadhani Mhe. Ali Denge alisahau alipokuwa akitoa mchango wake. Lakini naamini atakubaliana namimi kwamba fedha zile tayari wananchi wengi au wanachi wetu wemeshakabidhiwa kwa ajili ya wale walioezukiwa na mapaa kuweza kurejesha katika hali zao za awali.

Mhe. Spika, nikiendelea aliseme kwamba Tume ya Uchaguzi iweze kutoa haki. Mhe. Spika, tunauchukua ushauri wa Mhe. Abubakar, lakini mimi nataka niseme kwamba Tume ya Uchaguzi kwa kweli wanajitahidi sana na lazima tunapaswa tuwapongeze. Lakini lazima tuangalie kwa sababu sualala la Tume ya Uchaguzi nitalizungumza kwa pamoja kwa sababu limezungumzwa katika kuowana.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi kila tunapokuja katika vikao vya Baraza yale yanayozungumzwa ndio tunayoyafanyia kazi. Sisi tukirudi michango ile tunaichukua, tunajaribu kuhojiana, kama kuna matatizo yalifanyika katika Wilaya au Mikoa tunayafanyia kazi. Ndio maana kila siku tunapokuja tunajaribu kuja katika maboresho.

Mhe. Spika, hili nitajaribu kuliunganisha na la Mhe. Mazrui pamoja na baadhi ya Waheshimiwa wengine. Kuna takwimu mbali mbali ambazo wengine wamekuja nazo tokea mwaka 2000, 2005, 2010. Hapa sisi ndio tuliokuwa

tukilalamika upande wa Chama Tawala unawarushia makombora upande wa Upinzani na Upande wa Upinzani unawarushia makombora Chama Tawala kwamba kuna fojari katika uwandikishaji, kuna watu wanajiandikisha mara mbili, kuna wengine sio Wazanzibari. Hii ndio iliyosababisha kwamba hiyo takwimu iliyokuwa kubwa kipindi cha nyuma sasa hivi imekuwa ndogo, katika hili hili zoezi ambalo tunalifanya kitaalamu. Basi pia tayari kuna watu wameshajitokeza wamefanya uandikishaji zaidi ya mara moja.

Pamoja na utaalamu wote ambao tunafanya lakini tulipokuja kwenda tukafanya *review* katika *computer* tayari kuna majina yanakubaliana ukija ukiangalia mtu ndiyo yule kwa yule. Kwa hivyo hata hizi takwimu zinakuwa zinatofautiana. Kwa kuwa uwandikishwaji wa safari hii umekwenda kuhakikisha kwamba kura moja atapiga mtu mmoja tena Mzanzibari mkaazi. Ndio maana hao waliopungua walikuwa aidha alikuwa hana sifa upande mmoja sifa yake imebakia upande wa pili. Kwa kweli Tume ya Uchaguzi wanajitahidi sana katika kazi zao.

Vile vile nataka nilizungumzie suala la takwimu zilizotolewa ambazo nadhani Mhe. Hamadi Masoud nitalijibu kabisa hili suala. Kuna takwimu zilitolewa na Tume ya Uchaguzi katika kipindi kilichopita. Takwimu zile zilikuwa ni sahihi, zile zilikuwa ni takwimu za awali, lakini tume ya uchaguzi inapofanya takwimu zake inapofanya uandikishaji baadaye ndio wanakwenda katika mtandao wanajaribu kuangalia wale waliokuwa wamejiandikisha mara mbili ina maana wanalifuta jina moja wanabakisha jina moja. Sio kama mtu kajiandikisha mara mbili anafutwa moja kwa moja, anakuwa hafutwi.

Ndio maana takwimu ya kipindi kile imebadilika na hii ya kipindi hiki imekuwa tofauti. Lakini takwimu iliyotolewa kwa kipindi kile ilikuwa ni sahihi na takwimu hii iliyotolewa katika kitabu chetu sasa hivi ni sahihi. Pamoja na takwimu ambayo imo katika kitabu chetu sasa hivi tunasema ni sahihi. Tume ya Uchaguzi sasa hivi imo katika zoezi la *display* ya majina. Majina yanabandikwa katika maeneo kama alivyosema Mhe. Mazrui yeye amezungumza kwa upande wake. Lakini vile vile na kwa upande wa huku na wao wanajaribu kuangalia katika *display.*

Kuna watu ambao wanajulikana hawana haki ya kujiandikisha katika. eneo moja watakuwa *rejected* vile vile. Kwa hiyo kama kuna mtu ambaye sio Mzanzibar ameandikishwa atakuwa *rejected*. Kwa hiyo hii takwimu baada ya *display* itakuja kutokea nyengine mpya ambayo itakuwa tofauti na hichi kitabu. Kwa hili Waheshimiwa lisitupe matatizo. Tume ya uchaguzi tunapowataka walete takwimu wanaleta zile takwimu ambazo walizokuwa nazo kwa kipindi kile.

Hii takwimu ambayo imo katika kitabu hiki tusitegemee kwamba ndio itakuwa takwimu sahihi itakayokuja katika uchaguzi Mkuu. Baada ya display kutakuwa kuna pingamizi na kuna muda wa kisheria umewekwa mtu ambaye aliyekuwa ana haki atabakia aliyekuwa hana haki atakuwa *rejected* na atakwenda kujiandikisha katika eneo analohusika. Hili mimi nadhani si wakati mzuri wa kuweza kuwalaumu watu wa Tume ya Uchaguzi kazi tuliyowapa na tuliyowatwika. Tuna kazi mbili tumewapa. Tume ya Uchaguzi wamekwisha kujiandaa kwa zoezi zima la Uchaguzi Mkuu wa Oktoba wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Ame Mati, ametusaidia sana katika kuisaidia Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ilikuwa sisi sasa hivi tunyamaze kimya tusiwambie jambo lolote. Kwa sababu kwanza wamefanya kazi ya ziada ambayo sikutegemea kama wengeliweza kuifanya katika kipindi hiki. Tume ya Uchaguzi kama wengeweza kusema kwamba wengelimwambia Mhe. Rais kwamba kwa sasa hivi hatuwezi tukafanya kura ya maoni basi Mhe. Rais na yeye angekuwa hana uwezo wa kuiambia Tume ya Uchaguzi fanyeni kura ya maoni.

Tume cha Uchaguzi mpaka ikishakamilisha zoezi la uandikishaji ili wananchi wote waweze kupata haki wale wenye haki ndio Rais sasa ndio anaweza kusema kwamba tarehe fulani Tume ya Uchaguzi iitishe kura ya maoni. Lakini pamoja na hayo hili halikuwemo katika programu, lakini kama wa kuilaumu tusiilaumu tume ya uchaguzi Mhe. Mati alisema tuilaumu serikali. lakini serikali nayo pia siyo ya kuilaumu tujilaumu sisi wenyewe kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu serikali imeleta Mswada lakini Mswada ule umeletwa baada ya hoja ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, serikali sisi tunawajibika kwa Baraza la Wawakilishi nadhani Katiba kifungu cha 43(5) kama sikusei tukikiangalia Katiba ya Zanzibar kinatwambia Serikali tunawajibika kwa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo Tume ya Uchaguzi imekuwa *forced* na Baraza la Wawakilishi na imekuwa *forced* na Serikali kupitia Baraza la Wawakilishi. Serikali ingelikataa kwa sababu halikuja mawazo wengine wakasema Tume ya Uchaguzi kwa kuwa imejipanga kufanya uchaguzi Oktoba mwaka 2010 basi hili zoezi kwa nini lisiende pamoja. Lakini sisi wengine miongoni mwetu tukasema aa kura ya maoni iyende mapema. Kwa hivyo Tume ya Uchaguzi imefanya vile tulivyotaka. Mimi nadhani ni lazima tuwape pongezi inayostahiki Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu ameeleza walemavu wangapi wameshasajiliwa. Tayari walemavu wamesajiliwa kupitia katika Wilaya mbali mbali na takwimu tunayo pale. Nitamjulisha Mhe. Abubakar ili baadaye kuweza kujua ni walemavu wangapi. Hiyo kazi tunaifanya lakini kama

tulivyosema kutokana na uhaba wa wafanyakazi tuliokuwa nao. Pia na uhaba wa fedha, nyenzo za kufika katika hayo maeneo. Walemavu ni lazima tuamini kwamba Idara hii ni mpya kwa hivyo walemavu wengi walikuwa wanafichwa majumbani, takwimu zao zilikuwa hazijulikani sahihi. Waliokuwa wanajitokeza ni wale ambao wamesoma kidogo na wale ambao wanaweza kwenda wakajiunga katika ule mwamvuli wao wa jumuia ya watu wenye ulemavu. Lakini bado kuna walemavu wengi hasa watoto wazazi wao walikuwa wanawaficha. Sasa hivi tunaendelea pamoja na takwimu ambazo tulizokuwa nazo sasa hivi lakini bado walemavu wengi hawajitokezi.

Hili tunaliomba sana sisi ni waheshimiwa tunaoishi katika majimbo mbali mbali. Tuwashajihishe masheha wawaorodheshe walemavu katika kila shehia, wapelekwe katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya na pale katika afisi ya Mkuu wa Wilaya tunaye mratibu wetu wa Afisi ya Waziri Kiongozi ili sasa tuweze kuwatambua wapo walemavu wa aina gani na sasa hivi walemavu wamebaguliwa katika maeneo mbali mbali, walemavu wasioona, wasiosikia, walemavu wa ngozi na walemavu wa viungo.

Mhe. Spika, hii nataka niseme kwamba hili jukumu la kuwatambua walemavu tusaidie sana sisi Waheshimiwa kupitia kwa masheha wetu ili sasa tuweze kupata hesabu iliyokuwepo sahihi. Zoezi hili kwa kweli bado linaendelea na kama tulivyosema wameanza na programu yao wameanzisha *data base* yao kwa hivyo baadaye zile kumbukumbu zote watazitia pale kwenye *data base* yao na zile kumbukumbu zitakuwa wakati wowote zinapatikana, lakini hiyo kazi bado inaendelea.

Mhe. Spika, amezungumzia vile vile suala la Idara ya Maafa kupatiwa nyenzo. Hivi sasa hivi Idara ya Maafa tayari kuna programu ambayo inaendelea kuwapatia *radio call* maafisa wote wa idara ya maafa kuanzia Makao Makuu mpaka katika Wilaya zetu ili yale mambo ya ghafla yanapotokezea basi tuwe tunaweza kufika kwa mapema na kuweza kutoa muongozo.

Vile vile Idara ya Maafa haifanyi kazi peke yake inafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi nyingi. Kama tunavyosema Idara ya Maafa moja katika kazi yake ni kutoa taaluma kupitia kwa wenzetu hawa wa zima moto, hata kwenye Mabaraza ya miji namna ya kujenga mitaro, namna ya kujenga nyumba katika mitaa, kuweka njia za kupita gari. Wakati mwengine kuna wananchi wengine wanakuwa hawafati ile miongozo inayotolewa. Kwa hivyo Idara ya Maafa moja katika kazi yake sio kuwa na nyenzo ya kufanya wao wenyewe ile kazi, lakini kwa kushirikiana na taasisi nyengine kama tulivyosema. Hata vikosi vyetu vya aina mbali mbali huwa tunavitumia pale yanapotokezea maafa mfano kama moto, mafuriko na kadhalika.

Mhe. Spika, nikija kwa Mhe. Fatma Fereji yeye alisema uwiyano wa pesa za AK na JK alizungumzia nadhani katika kile kitabu, mle tumeeleza kwamba mfuko wa AK na JK wao wametoa bilioni 1.2. Hizi ni fedha ambazo walizozitoa viongozi wetu. Lakini kama kawaida mfuko ule sio kama zile fedha za AK na JK kwamba ndio peke yake ndio zinazotolewa katika mfuko wa kujitegemea. Fedha zile Benki na wao wanachangia mara tatu ya fedha zile ambazo zilizotolewa. Ndio maana wakaainisha kile kiwango kilichotoka serikalini na kile kiwango ambacho walichoanza kuongezea wao. Wao wameanza kuongezea kama shilingi 800 milioni kitu kama hicho. Kwa hivyo, ina maana zile za ziada ni hizo ambazo benki wana-*top up*. Kwa sababu zile za serikali zinatolewa halafu benki na wao wana-*top up* kwa mujibu wa makubaliano yao na serikali.

Kwa sababu zile za AK na JK inakuwa kama ni dhamana ile, inapokuwa wale wajasiriamali wameshindwa kurejesha zile fedha ina maana inakuwa kama ni *guarantor*. Kwa sababu fedha zaidi inayotoka ni fedha ya benki kwa hivyo, kama hakuna *guarantor* ina maana benki hawawezi wakatoa fedha zao. Kwa hivyo, fedha zile bado ile *figure* ni sahihi na utaratibu wake ni kama hivyo nilivyojaribu kuelezea.

Mhe. Spika, nikiendelea kwa haraka haraka amesema kwa nini wanawake wanapewa pesa ndogo katika Mfuko huo. Mhe. Spika, huu ni utamaduni, sasa labda hapa hasa wawakilishi wanawake wawashajihishe wanawake wenzao katika maeneo yetu. Lakini hata sisi wenye majimbo kura nyingi tunazipata kwa wanawake, tuwashajihishe sasa wakope pesa nyingi.

Ukiangalia katika mikopo wanawake wengi wanakopa pesa kidogo, wanaume wanakopa pesa nyingi. Kwa hivyo, mimi nafikiri suala la uwiano kwa nini wanawake wakawa wanapewa pesa kidogo wanaume wanapewa nyingi, nafikiri tuweze kutoa elimu. Wanawake wengi wanaogopa kudaiwa hili lazima tukubali, lakini wanaume hawaogopi kudaiwa. Kwa hivyo, ndio maana wanaume wanapokopa hawaanzi na shilingi laki tano, anaanza na milioni na kuendelea. Sasa wanawake wengi wanaanza shilingi laki moja kajitahidi mpaka milioni moja. sasa tuwashajihishe ili waweze kukopa pesa nyingi ili waweze kujiendeleza katika miradi yao.

Mhe. Spika, najitahidi haraka haraka. Pia alisema suala la *Blue Bank.* Hili nadhani Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi baadae akija katika bajeti yake au atakuja kunisaidia katika maelezo ya ziada. Lakini kweli kuna taasisi *Blue Bank* na sio peke yake kuna nyengine wanaiita *Easy Finance*. Hiyo ni *Easy Finance* kweli, ukienda leo pesa unachukua kesho. Lakini sasa hicho kigongo chake unaweza ukauza mpaka wajukuu wako, sio watoto tu mpaka wajukuu. Kwa sababu unapewa pesa zile unaweka dhamana kitu chako na wanakwambia kila

baada ya mwezi uwalipe asilimia 20, ile asilimia 20 unayowalipa na ile *capital* iko pale pale.

Sasa hapo inatakiwa elimu kwa wale wakopaji. Kwa sababu unapokwenda kukopa kunakuwa na mkataba wa makubaliano baina ya mkopaji na mkopeshaji. Sasa kuna wengine anaweza kusema mimi hata kama riba asilimia mia moja wewe nipe tu, madhali mtu ana shida yake pale anasema tu, matokeo yake wakati wa kulipa ndio anaanza kumtafuta mjomba nisaidie. Hili nadhani Mhe. Waziri wa Fedha kuna *regulation* za *BoT* zinazozungumzia masuala ya riba.

Mimi ninavyojua katika benki riba hawakutakiwa wazidi asilimia 30, lakini inakwenda *around* kuanzia asilimia 10 – 30 hapo ndio wanacheza cheza, ndio maana kunakuwa na ushindani. Kwa hivyo, ina maana benki ukiwa na riba ndogo wakopaji wengi ndio watakuja kwako. Lakini sasa katika hizi taasisi za kifedha ambazo sio benki, hawa *regulations* zao sijui ziko vipi. Nadhani Mhe. Waziri wa Fedha zaidi aje atusaidie atapokuja kuzungumzia bajeti ya Wizara ya Fedha. Kwa sababu kweli wananchi wetu wanapotaka kukopa wanakuwa hawajui athari zake, matokeo yake wanaanza kuambiwa sasa uza nyumba na vitu vyengine wanaanza kupiga kelele.

Mhe. Spika, kweli sisi kwa upande wetu kama serikali tunatakiwa lazima tuwalinde wananchi wetu, ili kuwaangalia hawa kama hawana *right* ya kuweza kufanya hivyo, kutoza riba hizo, basi tutamsikiliza Waziri wa Fedha akija kuzungumza baadae. Kama hawana *right* hiyo tutazifungia mara moja na waweze kufuata taratibu zinazokubaliwa kisheria.

Mhe. Spika, tatizo la mradi wa maji Mjimkongwe nimezungumza na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi amenambia kwamba, mradi wa maji wa Mjini unaosimamiwa na Japan unakabidhiwa mwisho wa mwezi wa Julai. Mimi ningelimuomba Mhe. Fatma Abdulhabib tustahamili mpaka mwanzoni mwa mwezi wa Agosti. Kwa sababu ina maana hata vile visima vitakuwa tayari vimesharuhusiwa kutumika.

Mradi unajua mikataba na wahisani hawa hata kama kitu unakiona, kama ile tarehe ya kukabidhiwa haijafika huwezi ukakitumia na ukakitumia ina maana akija akikukabidhi kama kuna athari atakwambia mimi siwajibiki utawajibika wewe. Mpaka ukikabidhiwa ndio pale sasa una uhuru.

Tatizo la maji sio Mji Mkongwe peke yake hata ndani ya Jimbo langu la Kwamtipura Mhe. Spika. Tatizo la maji bado ni sugu tena sugu sana. Kwa hivyo, hili mimi najaribu kuwaomba wenzangu wote na Waheshimiwa wa Majimbo yote wajue kwamba hili tatizo ni sugu tustahamili mpaka kuanzia

tarehe 1 Agosti tukishakabidhiwa, tuangalie vile visima ile *floor* yake ya maji itakuwa vipi na wananchi wetu wataweza kufaidika vipi na huduma ya maji.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe pia amezungumza kuhusu suala la takwimu hasa Tume ya UKIMWI, bado tunaambiwa ongezeko letu lipo pale pale katika vitabu. Sasa hili nataka nirejee kwamba, Tume ya Ukimwi ina programu yake, na hawa wanapofanya utafiti wa ongezeko la maambukizi hii *review* inakwenda kila baada ya miaka mitano. Kwa hivyo, hatuwezi tukatoa takwimu nyengine mpaka ifike miaka mitano mingine. Kwa sababu ndio ile programu yetu ilivyo.

Lakini bado katika suala zima kila tunapofanya vikao vyetu, tunapofanya tathmini na hata wataalamu Washirika wa Maendeleo na hizi *NGO's* nyengine bado katika suala tulilojitahidi Zanzibar maambukizo ya UKIMWI hayaongezeki.

Tatizo la maradhi haya ni tatizo la maradhi mengine. Mhe. Spika, malaria tumeyaondoa na tumetoka kwenye asilimia kama sikosei 40 mpaka tumekuwa asilimia 5. Kwa sababu maradhi ya malaria mtu akishapoa anakuwa ndo kapowa, maradhi ya UKIMWI hata kama keshapoa yule anakuwa bado. Kwa sababu mtu mwenye malaria ukimtibu hana, lakini mtu aliyepata virusi vya UKIMWI ukimtibu bado anavyo, umeona tofauti hiyo? Hapa maradhi ya UKIMWI mpaka mtu afe, malaria akishakuwa umemtibu hana vimelea ina maana ile takwimu inapungua.

Sasa ingelikuwa tumeshapata dawa ya tiba ambayo mtu anapokuja kupimwa vile virusi hana, nadhani sasa hivi katika hayo maambukizo tungekuwa tuna zaidi ya asilimia 5 chini. Lakini kwa sababu wagonjwa wengi au watu wengi wanaoishi na virusi ya UKIMWI kwa kweli tunawapa tiba na wanaendelea kuishi vizuri ndio maana ile takwimu unaikuta iko pale pale. Kwa sababu hatutaki wafe, tukitaka ile takwimu ipungue ili tupate sifa itabidi tusiwape dawa wafariki.

Sasa hapo itakuwa tunafanya makosa. Ndio maana takwimu zetu mkawa mnazishangaa, mbona hii 0.6 ipo hapa hapa tu, asilimia moja haizidi, lakini kuna baadhi ya makundi lazima tuzungumze ukweli. Kuna baadhi ya makundi ya vijana wetu maambukizo yao yako makubwa. Kwa mfano, wanaotumia madawa ya kulevya maambukizo yako asilimia kubwa. Sasa hili mimi nadhani tunafanya kazi kubwa na tuwapongeze Tume ya UKIMWI. Kama ingekuwa si kazi yao ingekuwa takwimu yetu imeongezeka sana na watu wengi wangekuwa na virusi.

Mhe. Spika, najua unaangalia saa yako lakini nilikuwa najaribu kujibu mengi ili Mhe. Waziri Kiongozi nimbakishie machache. Kwa sababu yeye zaidi

atajibu yale ya kitaalamu sana, lakini haya mengine nitajitahidi niyajibu mimi mwenyewe.

**Mhe. Spika:** Basi jaribu kwenda haraka umalize kwa muda wa robo saa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi:** He, sawa Mhe. Spika, lakini watanilaumu hawa. Mhe. Spika, tukija Idara ya Watu wenye Ulemavu nafikiri hili nimeshalitolea ufafanuzi.

Mfuko wa Baraza la Wawakilishi nimeshatoa ufafanuzi na Waziri wa Fedha na Uchumi amenisaidia.

Mhe. Spika, nikiendelea Tume ya Uchaguzi kuhusu suala zima la kura ya maoni nimeshalizungumza hilo. Sasa nije kwa Mhe. Ali Suleiman Ali nafikiri yuko jimboni sasa hivi katika mchakato, lakini nadhani ujumbe utamfikia huko huko. Yeye alizungumzia suala zima la mfumko wa bei.

Mhe. Spika, mfumko wa bei unatokana na mambo mengi. Kwanza *inflation* ya vyakula lakini zaidi inatokana na dola inapopanda bei. Vile vile sasa hivi kuhusu suala zima la usafiri na hao ma- *pirates* wametuzidishia balaa jengine. Kwa sababu meli zinazokuja katika nchi zetu za Afrika Mashariki inabidi bima zinakatiwa kubwa kwa hivyo na gharama zinaongezeka sasa mfumko wa bei vile vile unasababisha. Kuna vigezo vingi vya mfumko wa bei.

Lakini pamoja na yote hata Mhe. Makame Mshimba namshukuru alizungumza vizuri kwamba, sasa hivi katika suala zima ili tusiwe tunakula mapembe tu na mapembe kwa kweli ukiangalia ladha yake si nzuri, ingawa si vizuri kuponda kitu tunachotumia, tuendelee kutumia, lakini tujitahidi zaidi sasa tulime na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili atapokuja kusoma katika bajeti yao wataelezea. Kuna karibu hekta 28 elfu hizo ambazo zinastahiki hasa kufanyiwa *irrigation*. Sasa serikali huo ndio mkakati wetu.

Sasa hivi kuna programu nzuri tu ya Wizara ya Kilimo. Walizungumza vizuri baadhi ya waheshimiwa kwamba kuna baadhi ya mabonde, hata Mhe. Bihindi Hamad alizungumzia kwamba kuna mabonde kuna baadhi ya sehemu hayafanyiwi *irrigation* kila siku yanazungumzwa hayo kwa hayo tu. Hii ni *challenge* kwa Wizara ya Kilimo na sisi tutajitahidi kuwasimamia kwamba yale mabonde ambayo kila siku yamo katika programu ya uafdhili sasa hivi tuondoke kule twende na maeneo mengine ili kilimo kiweze kuenea kwa wingi na kupunguza huu mfumko wa bei.

Mhe. Spika, vile vile amezungumza suala la Mfuko wa Maafa nafikiri nimeshalizungumza. Lakini pia Mheshimiwa yeye alitofautiana kidogo na

baadhi ya maoni. Ndio maana nikasema suala hili bora nije nilizungumze kwa pamoja kuhusu suala la kura ya maoni.

Mhe. Spika, suala zima la kura ya maoni mimi nadhani sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kazi yetu tumeshaimaliza. Sisi tumetoa maoni yetu, tumeelezea faida na walioelezea hasara. Kwa hivyo, kazi iliyobakia tumewaachia wananchi wetu. Sasa mimi nadhani wananchi wetu tuwape uhuru na hapa zaidi kama Tume ya Uchaguzi kazi yake kubwa itawaelezea ni namna gani zile sheria za upigaji wa kura unatakiwa aidha kwenye ndio patakuwa vipi na kwenye hapana patakuwa vipi.

Lakini sasa tukisema kwamba tuanze kuhamasisha. Kwa sababu katika uhamasishaji kuna watu wa aina mbili watajitokeza, watakaosema tieni ndio watakuwa na maneno yao tena yatakuwa makali, na watakaosema tieni hapana watakuwa na meneno yao tena yatakuwa makali. Tunaweza tukaichafua hali ya hewa.

Mhe. Spika, sasa hivi hali ya hewa mitaani ni nzuri, wananchi wote wameshafahamu nini kinachotakiwa. Sasa sisi kama wanasiasa, mimi nashukuru chama chetu kilitoa muongozo. Tulitolewa muongozo kila mmoja ende jimboni kwake akawaeleze wananchi faida na hasara ya kitu hiki, kwa sababu hakuna kitu chenye faida peke yake, lazima na hasara itakuwepo, hata kisu.

Mhe. Spika, kisu kina faida sana, lakini kisu hicho hicho ukikitumia vibaya kina hasara. Mimi nadhani tukianza kulishikilia sisi bango, ingawa Mhe. Abubakar Khamis Bakary kamchokoza sana Mhe. Waziri Kiongozi. Lakini mimi naomba sana Mhe. Waziri Kiongozi na leo nasikia keshatangaza nia huko, basi mimi nadhani wananchi wameshafahamu nini kinachotakiwa. Yeye naomba asiingie huko, kwa sababu haya mambo ya utashi na wakati mwengine wanachama wetu unawajua.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kazungumza vizuri alipochaguliwa mshika fedha wa wale watu wenye ulemavu wa akili. Alipokwenda na ndevu walianza kumvamia wakasema Seif Sharifu, sasa kuna wengine wakisikia ile Seif Sharifu tu, yeye kama kafanya vizuri, vibaya yeye hataki. Sasa na wengine nikija nikenda mimi nina sharubu watasema si Amani Karume huyo aa.

Hii nilikuwa natoa mifano tu, nazungumzia kwamba, kwa hali iliyoko mitaani hebu tuwaachie wao wenyewe, tusipate tabu kwa hili limeshakwisha. Tukianza kulitia kuche tutalikoroga na tukilikoroga patakuwa hapatoshi. Tatizo tukianza kulikoroga kwenye kura ya maoni basi na Uchaguzi Mkuu hapatokuja kukalika, ile *spirit* yote ya nia njema ya viongozi wetu itakuwa haikupatikana.

Mimi nadhani hata sisi tunapokwenda kutia kura tukubali chochote kitakachotokea. Kwa sababu mimi nikianza kusema sitaki ikijakuwa nataka, nikija kuanza kutia utashi na wengine tumeshaanza kusema Tume ya Uchaguzi muwe makini katika hili. Tume ya Uchaguzi watahesabu kura ndio ngapi na hapana ngapi *full stop*, hawatoongeza kitu kingine.

Mhe. Spika, hili tu nilikuwa nataka nilitolee ufafanuzi kwa sababu niliona kama kuna vilumbano vimeanza. Sasa mimi sikupendelea kuharibu siasa ya huko nje kama tunavyosema sisi wenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk, Ustadh, Alhaj rafiki yangu yeye alielezea suala zima la mfumko wa bei. Mimi nafikiri mfumko wa bei nimejaribu kuuelezea, lakini bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi watakuja kulizungumzia vizuri zaidi.

Kuliondoa suala la mafuta katika kero za Muungano. Mhe. Spika lazima tukiri, kunapokuwa na mlango wa mbele lazima na wa nyuma uwepo, tukisema tutumie mlango wa mbele halafu tupasue ukuta tutoke kwa kweli nyumba itavurugika. Suala la mafuta Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tumeshafanya maamuzi tayari. Hoja imekuja hapa tumezungumza wee, serikali tumeiambia tumesikia na ndio maana Mhe. Waziri Kiongozi akaandika barua kwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye mtendaji mwenzake, kila kitu kinakwenda na *level* zake. Ameshamuandikia Waziri Mkuu, yeye Waziri Mkuu ndiye kiongozi wa shughuli za Bunge.

Lakini vile vile Waziri Mkuu katika kikao chetu kilichopita cha tarehe 2 Bwawani, tuliliulizia suala hili. Akatoa ufafanuzi kwamba tayari suala lile barua imeshakwenda kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano tayari suala lile ameshamkabidhi Mwanasheria Mkuu.

Nataka nikuthibitishieni kitu kimoja. Mhe. Spika, katika safari ambayo tumempata Mwanasheria Mkuu mzuri ni safari hii. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tunavyomuona anayo nia ya kubwa ya kuhakikisha kwamba haya matatizo yanaondoka. Ni mtu ambaye tunakaa nae vizuri katika vikao, yale ambayo yanatuuma sisi yeye yanamuumiza na kwa kuwa yeye ndiye mshauri wa serikali, naamini atamshauri vizuri Rais wa Jamhuri ya Muungano ili hili suala liondolewe.

Kwa sababu lazima tukitaka tusitake kwa kuwa limo ndani ya katiba na ile Katiba ya Jamhuri ya Muungano, *final* lazima liende Bungeni kwa ridhaa ili liondolewe. Tumeshajaribu kufanya utafiti hata hao Wabunge hawana tatizo na hili. Sasa mimi nadhani tuiachie serikali ifanye kazi yake.

Pamoja na hayo, sisi kwa kuwa tumeshafanya maamuzi sio kama tumekaa kimya tunasubiri tuambiwe nini, aa. Tumeshaanza sasa hivi nafikiri kuna Sera ya Nishati ile tayari, hayo ndio maandalizi yenyewe, kuna wataalamu tayari tumeshaanza programu ya kusomesha. Lakini vile vile hata suala hili tumepata semina mbali mbali. Wamekuja wataalamu wa Norway na sisi mawaziri wametufanyia semina *Zanzibar Beach Resort*. Wametueleza mambo mengi tena mazuri, tahadhari ya namna ya kushughulikia masuala haya ya uchimbaji wa mafuta.

Wametutolea mfano mzuri. Wamesema Norway wanachimba mafuta tena wana mafuta mengi. Lakini Norway hawatumii hata *single cent* katika bajeti yao, zile fedha zote zinazopatikana za faida ya mafuta wanawekeza nje na ndio zile zinazokuja kusaidia wale wanaozaliwa, wastaafu, yaani ile kama ni akiba ya uzeeni. Ndio maana wenzetu wanakuwa na fedha nyingi za kuweza kutusaidia na sisi.

Sasa na sisi tutachimba mafuta ili yakidhi mahitaji yetu. Sisi hatusemi kwamba ile faida tuta-*invest* nje ya nchi aa. Kwa sababu bado *capital* yetu haijatutosheleza. Amezungumza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwamba kapu yetu sasa hivi unaikusanya leo unatumia kesho, cha keshokutwa unasubiri. Sasa mimi nadhani hili tuko makini, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi inaendelea na programu. Siku watakayotwambia *ok* sawa sisi tunaendelea, lakini hata kama hawajatwambia.

Mhe. Spika, kuchimba mafuta Zanzibar tukianza kuchimba hatujavunja Muungano. Kwa sababu tayari ndani ya Katiba kuna mambo ni mambo ya Muungano, lakini kila mmoja anafanya kwa upande wake na wala katiba haijavunjika.

Kwa mfano suala la gesi. Gesi inachimbwa Bara Muungano haujavunjika mpaka leo upo, sasa seuze sisi kuchimba mafuta ndio Muungano utavunjika? Sasa sisi tunaendelea na *process* muda ukifika, ikifika hatua ya kuchimba mafuta tutachimba na katiba itakuwa ipo kama imerekebishwa au haijarekebishwa na Muungano utaendelea kuimarika. Kwa sababu sisi tutakuwa keki yetu, tukianza kuwa hatuombi ombi basi hata manung'uniko madogo madogo yatapungua. Kwa hivyo, waheshimiwa msiwe na hofu Waziri wa Fedha keshasema hapa subirini kidogo tu, tunaanza kutafuta yale mapauro al;iyosema Mhe. Najma Khalfan. Majembe ya kuchimbia mafuta tunatafuta na tuna wataalamu.

Kwa sababu rasilimali hii pia taaluma tuliyopewa msikubali tu wataalamu wakajikita wote kutoka nje, lazima muwe na wataalamu wenu wa ndani mtaibiwa. Tumeambiwa na wahisani mtaibiwa, kabisa, wenzetu sikilizeni Bara kule madini yale yamechimbuka kufanya utafiti sasa hivi kelele, hatutaki mfukuze, nani. Sasa sisi hatutaki twende huko. Wazanzibari tuko makini kweli katika mambo yanayohusu maslahi ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawaomba sana wajumbe wamuamini Waziri Kiongozi, barua ameshaandika kwa Waziri Mkuu, taratibu za serikali haziendi kwa midomo zinakwenda kwa *correspondence*, unapeleka unasubiri jawabu. Mimi naamini jawabu itakuwa nzuri.
Mhe. Spika, najitahidi, nadhani kwa Mhe. Said Ali Mbarouk naomba anistahamilie kwa niliyoyabakisha niendelee kwa wengine.

Mhe. Omar Ali Jadi. Mheshimiwa kwa makofi hayo inaonesha yale mazito hasa waliyokuwa wanayataka wamesharidhika. Sasa kama utaniruhusu Mhe. Spika, basi mimi niombe kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wote ambao wamechangia. Na wale niliokuwa sijawataja tumezingatia michango yao. Lakini hii Mhe. Spika, sio kama jawabu aa, hii michango yao ndio tunayokwenda kuifanyia kazi. Haya tunakwenda kuyafanyia kazi katika mwaka 2011/2012. Bajeti ya mwaka 2011/2012 utakuja kutuoana namna tunavyosimama, tunavyoendeleza mambo waliyoyataka wananchi.

Mhe. Spika, nakushukuru baada ya hayo machache kama nilivyosema, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa majumuisho ya hoja za wajumbe waliochangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Vile vile namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi kwa kutoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya jumla ya Afisi ya Waziri Kiongozi.

Baada ya utangulizi huo, sasa nachukua fursa ya kuwataja Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia hotuba ya Afisi ya Waziri Kiongozi kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir(Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala)

2. Mhe. Abubakar Khamis Bakary (Waziri Kivuli Afisi ya Waziri Kiongozi)
3. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Said Ali Mbarouk
6. Mhe. Omar Ali Jadi
7. Mhe. Ali Denge Makame
8. Mhe. Ali Moh'd Bakari
9. Mhe. Ashura Abeid Faraji
10. Mhe. Hamad Masoud Hamad
11. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
12. Mhe. Ali Haji Ali
13. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
14. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
15. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
16. Mhe. Zakiya Omar Juma
17. Mhe. Raya Suleiman Hamad
18. Mhe. Omar Ali Shehe
19. Mhe. Ame Mati Wadi
20. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
21. Mhe. Haji Mkema Haji
22. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi
23. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji ambaye amechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi ametoa ufafanuzi mzuri kuhusu hoja kadhaa zilizotolewa wakati wa kuchangia hotuba ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Mimi nitatoa maelezo ya jumla katika eneo moja la juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kushughulikia kero za Muungano.

Mhe. Spika, mpaka sasa Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi imezipatia ufumbuzi kero saba za Muungano. Kero hizo zilizopatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo:-

1. Zanzibar imepatiwa mikopo ya misaada ya kibajeti kuanzia mwaka uliopita.
2. Zanzibar imepatiwa fedha zinazotokana na misamaha ya madeni.
3. Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar waliokuwa wakitozwa kodi mara mbili imetatuliwa. Imeamuliwa kuwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha, kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zihesabike kuwa bidhaa hizo tayari zimeshaingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

kufika kwenye soko. Kwa hivyo, kusiwe na haja ya kuzitoza kwa mara nyengine tena kodi.

4. Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetakiwa ziangalie nyaraka ili kuthibitisha kuwepo kwa hisa za Zanzibar katika Benki Kuu ya Tanzania.

Mtakumbuka katika siku za nyuma nyaraka hizi zilikuwa hazipatikani. Pengine jambo hili kama alivyosema Mhe. Haji Mkema Haji lilichukua muda mrefu pengine zaidi ya miaka 15 kwa sababu ya tatizo hilo, lakini sasa nyaraka hizo zimepatikana na ndio maana tumezitaka wizara mbili hizi zinazoshughulikia masuala ya fedha ziangalie ili kutoa taarifa. Kama nilivyoeleza kwenye bajeti yangu, ifikapo tarehe 24 mwezi huu.

5. Kuhusu suala la uvuvi katika ukanda wa uchumi na Bahari Kuu imeamuliwa kuwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ipewe mgao wa fedha zinazotokana na mauzo ya leseni katika uvuvi huo wa Bahari Kuu asilimia 50. Serikali ya Muungano ipewe asilimia 30 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipatiwe asilimia 20.
6. *Zanzibar Maritime Administration* iruhusiwe kutekeleza shughuli zake kulingana na mikataba ya kimataifa. Jambo hilo limeshatekelezwa.
7. Suala la utekelezaji wa Sheria za Haki za Binadamu limepatiwa ufumbuzi. Hivi sasa sheria hii inatumika sehemu zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania Bara na Zanzibar).

Mhe. Spika, yako masuala au kero ambayo bado mpaka sasa hayajapatiwa ufumbuzi, lakini yamejadiliwa katika vikao mbali mbali vya Kamati ya Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu. Masuala hayo ni kama ifuatayo:-

1. Suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta kuondolewa kwenye orodha ya masuala ya Muungano.
2. Ajira kwa Wazanzibari katika Taasisi za Muungano.
3. Mgawanyo wa mapato kati ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tansania na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na
4. Hisa za Zanzibar katika Benki Kuu.

Mhe. Spika, wakati wa mchango wake Mhe. Abubakar Khamis Bakary alisema, ipo miradi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo ilipelekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini haikuelezwa kwenye hotuba yangu ya bajeti.

Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba miradi hiyo haikuelezwa, lakini miradi hiyo ni kama ifuatavyo. Kuna miradi minne ya Zanzibar ambayo

ilipelekwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kutafutiwa ufadhili. Ambayo ni ;

1. Mradi wa Bandari ya Maruhubi,
2. Mradi wa Udhibiti wa mimea na wanyama,
3. Mradi wa eneo huru wa maradhi ya wanyama na
4. Jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Zanzibar.

Hii ndio miradi ambayo imewasilishwa. Lakini kama ambavyo tumekuwa tukieleza katika Baraza lako tukufu kwamba miradi hii sio kama watu wengi tulivyokua tukitarajia kwamba miradi hii ipate ufadhili wa moja kwa moja wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Jumuiya ya Afrika ya Mashariki haina fedha. Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inalolifanya ni kuratibu uandaaji wa miradi maalum kwa ajili ya miradi hii kuombewa fedha kutoka kwa fadhili mbali mbali na washirika wa maendeleo.

Mradi mwengine ni mradi wa ujenzi wa jengo la abiria, ambalo tayari hivi sasa umepatiwa ufadhili kutoka kwenye Benki ya EXIM kutoka China.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma na Mhe. Hamad Masoud Hamad waliuliza mpaka sasa vimefanyika vikao vingapi. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa mwaka uliopita wa 2009/2010, vilifanyika vikao viwili vya Muungano. Kwanza kikao cha Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kikao chengine ni kikao cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, kilichokuwa chini ya Uwenyekiti wa Makamu wa Rais.

Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika mwaka uliopita, kamati zinazozungumza masuala mbali mbali ya kero za Muungano, zilikutana mara chache sana, lakini hali hiyo imetokea kwa sababu wakati mwengine yapo masuala yanayojadiliwa kuhusiana na kero za Muungano. Masuala ambayo yanahitaji utafiti, masuala ambayo yanahitaji sheria kwa maana hiyo yanakuwa yanachukua muda mrefu kidogo kufanyiwa kazi. Kwa maana hiyo basi inabidi wapewe muda wa kutosha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Ndio maana kamati na wanakamati wanawajibika kusubiri mpaka taarifa hizo na ripoti za utafiti wa masuala mbali mbali zinapokamilika ndipo ratiba ya kuandaa kikao inapotolewa.

Mhe. Spika, vikao hivi kwa kawaida huwa vinagharimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Spika, kama unavyoelewa kwamba upo utaratibu maalum unaotumika katika kubadilisha sheria, kubadilisha katiba inayohusu masuala ya Muungano. Nalisema hili kwa sababu wajumbe wengi wamesema kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar akiwemo Mhe. Zakiya Omar Juma

kwamba alitoa agizo kuwa suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta liondolewe katika orodha ya Muungano. Lakini bado wanashangaa kwamba Waziri Kiongozi kwa kupitia kwenye hotuba yake amesema kwamba amemuandikia Waziri Mkuu barua.

Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Rais alifanya hivyo, alitoa kauli hiyo hadharani na sote tulimsikia. Lakini kwa utaratibu wa kisheria, Rais anapotoa kauli sisi tuliochini yake tunapaswa sasa kuitekeleza kazi hiyo au agizo hilo, lakini kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizopo. Sasa suala la utafutaji na uchimbaji mafuta limeelezwa katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa lipo. Kwa hivyo, utaratibu wake wa kuondoka, kwa kawaida inapotokea haja hiyo na mapendekezo na ushauri wa kuondoa jambo fulani katika orodha ya mambo ya Muungano. Basi Afisi ya Waziri Kiongozi kama ina maoni na mapendekezo inachotakiwa kufanya kwa mujibu wa taratibu, sasa inamuandikia mtendaji mkuu wa shughuli za serikali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ya Waziri Mkuu. Ndio jambo ambalo baada ya Mhe. Rais wa Zanzibar kutoa agizo hilo basi niliifanya kazi hiyo na nikamuandikia Mhe. Waziri Mkuu.

Mhe. Spika, labda nifanye masahihisho kidogo. Mhe. Hamza Hassan Juma wakati alipokuwa akitoa mchango wake hapa, alisema kwamba Waziri Mkuu tayari ameshampelekea suala hii Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yeye akalipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, naomba nifanye masahihisho. Masahihisho yenyewe ni hivi, Waziri Mkuu baada ya kupata mapendekezo na ushauri wa Zanzibar, juu ya kuondolewa suala hili katika orodha ya mambo ya Muungano. Yeye alilipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye tayari ameshatoa maoni yake juu ya namna ya kushughulikia au kuratibu jambo hili. Sasa alilofanya Waziri Mkuu, ameshalipeleka kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo sasa wataangalia kwa pamoja baada ya kufanya ushauri au mashauriano baina ya yeye na Rais wa Zanzibar, halafu tuangalie hatua nyengine itakayofuata, lakini Waziri Mkuu kwa hatua hiyo tayari yeye ameshapokea maoni hayo na Waziri Mkuu ameshawasilisha kwa kiongozi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma aliuliza kwamba ni lini suala la hisa za Zanzibar katika Benki Kuu litapatiwa ufumbuzi. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu hii, tunatarajia kwamba ifikapo tarehe 24 mwezi huu suala hili la kuwepo au kutokuwepo kwa hisa za Zanzibar litathibitika ifikapo tarehe 24 baada ya mawaziri wanaoshughulikia masuala ya fedha kukutana na kutafuta ithibati.

Mhe. Zakiya Omar Juma aliendelea na kusema ulipaji wa fidia utakuwaje. Je, ikithibitika Zanzibar inazo hisa Je, itaendelea kulipwa fidia ya asilimia 4.5 kwa kipindi chote kile ambacho tumekuwa katika mazungumzo au labda hata hiyo miaka ya nyuma, tokea masuala ya mazungumzo haya yalipoanza.

Mhe. Spika, jibu ni kwamba hili nafikiri litakuwa kama ni dai jipya ambalo pengine linahitaji kujengewa hoja na kufanywa mazungumzo mapya. Maana katika mazungumzo ya awali jambo hili halikuwepo. Sasa ni jambo ambalo tutalizingatia na kuangalia mazingira yatakuaje, kama itakuwa busara kufanya hivyo. Maana wakati mwengine mnapokwenda kwenye mjadala mkienda na hoja ngumu za kupingana na mazungumzo au mjadala unakuwa mgumu kidogo. Kwa hivyo wakati mwengine inabidi busara itawale ili kupata kile unachokusudia. Kwa hivyo, tutaangalia mazingira hayo ili tuone itakuwaje.

Mhe. Spika, Mhe. Hamad Masoud Hamad aliuliza ni lini Zanzibar itajiunga na OIC. Ni kweli jambo hili limekuwa likijadiliwa katika mikutano mingi ya Baraza lako tukufu. Kwa bahati nzuri basi wizara inayoshughulikia masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tayari imeshaanza kulishughulikia jambo hili na hivi sasa wako katika hatua ya kufanya utafiti. Taarifa niliyonayo ni kwamba wamebaini. Hivi sasa Jumuiya hii inafanya mapitio na marekebisho ya katiba yao ya sasa, ili kuona kama wataendelea kuwa na wanachama kwa masharti yaliopo sasa au masharti mapya.

Mhe. Spika, Wizara ya Nchi za Nje imenihakikishia kwamba baada ya katiba hiyo kufanyiwa marekebisho na hayo masharti mapya yakajulikanwa, basi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje itaiandikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar rasmi, ili Zanzibar sasa itowe maoni yake inahisije au ina maoni gani kuhusiana na suala hili au suala hili liendeshwe kwa utaratibu gani. Kwa maana hiyo wamenihakikishia kwamba baada ya kumalizika vikao hivi vya bajeti, pengine inawezekana kama taarifa hizo wanazozikusanya zitakuwa zimekamilika, basi wataiandikia Afisi ya Waziri Kiongozi rasmi juu ya jambo hili.

Mhe. Spika, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu aliuliza TANESCO na EURA itaipunguzia Zanzibar bei za umeme lini, ili bei hizi zinazotozwa kwa upande wa Zanzibar ziweze kulingana na bei zinazotozwa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika kikao kilichopita cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, tulilijadili jambo hili na kikao kilitoa maelekezo kwa waziri anayeshughulikia masuala ya nishati katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba alifanyie kazi jambo hili haraka iwezekanavyo na pengine katika kipindi kifupi kijacho. Sasa atuletee mapendelezo au atuletee maoni yake, maana yalikuwepo mawazo kwamba siku za nyuma wakati lilipoanza jambo

hili Afisi ya Waziri Kiongozi ilimuandikia rasmi Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya jambo hili, na jambo hili lilikuwa tayari limeshatolewa uamuzi, kwamba kwa kuwa Tanzania Bara imepandishiwa matumizi ya umeme kwa asilimia 21, basi ingekuwa vile vile ni busara basi na Zanzibar nayo ipandishiwe umeme kwa asilimia ile ile 21 badala ya asilimia inayotozwa sasa ya 168.

Mhe. Spika, lakini kwa bahati mbaya inaonekana yametokea mambo ya kutokufahamiana, ndio maana katika kikao chetu kilichopita cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, tukamtaka waziri basi sasa atupe maelezo kwa nini agizo lile halikutekelezwa na kama kweli aliona kuwa utekelezaji wake una matatizo, basi arudi kwa aliyetoa agizo kwamba jambo hili tulilotakiwa kulitekeleza lina matatizo moja, mbili na tatu. Pengine Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Waziri Mkuu angeweza kutafuta njia nyengine ya busara zaidi ya kulitatua jambo hili.

Kwa hivyo, naomba niwahakikishie wajumbe kwamba baada ya kumaliza vikao hivi au pengine baada ya kipindi cha wiki moja au mbili hivi, nitajaribu kufanya kila linalowezekana kumtafuta waziri anayeshughulika na mambo ya nishati ili tuanze kupata maelezo juu ya hatua zinazochukuliwa juu ya agizo hili.

Mhe. Ali Haji Ali aliniuliza je, sifikirii kwamba wakati sasa umefika kwa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kuna wakati hoja hii ilijadiliwa sana, nafikiri katika mkutano wa bajeti wa mwaka jana. Suala la Rais wa Zanzibar kuendelea kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano lilijadiliwa sana.

Mhe. Spika, sisi kama serikali, maana serikali ya watu inapokea maoni ya wananchi wake, wananchi wa nchi ndio wenye mamlaka kamili juu ya namna wanavyotaka serikali yao iendeshwe. Sasa kama Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wanaona jambo hili ni la busara, Rais wa Zanzibar aendelee kama zamani kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi tuendelee kujenga hoja hiyo na bila shaka serikali yenu ni sikivu italizingatia jambo hilo na kuchukua hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

Suala la pili ni suala la mgombea binafsi. Mhe. Spika, mtakumbuka mwaka jana kulikuwa na kesi, nafikiri ilipelekwa katika mahakama ya rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutaka Tanzania iruhusu sasa mgombea binafsi katika chaguzi zetu. Leo nilikuwa nikisoma magazeti ya leo, na ripoti niliyoipata ni kwamba jana yalitolewa maamuzi na mahakama kuu ya rufaa imelitupilia mbali ombi la kutaka kuwepo kwa mgombea binafsi katika chaguzi

zetu na ikapendekeza ikasema suala hili sasa lirudishwe katika bunge la Jamhuri ya Muungano, kwa sababu mahakama imesema inaona kwamba suala hili la mgombea binafsi ni suala zaidi la kisiasa kuliko la kisheria.

Kwa hivyo, katika nchi ambayo inaheshimu utawala wa sheria basi isingeweza kufanya vinginevyo. Kwa hivyo, mpaka sasa tuendelee kuheshimu uwamuzi huo uliotolewa na Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Ali Haji Ali aliuliza Je, hatuoni kwamba ipo haja ya kuruhusu uraia wa nchi mbili, kwa watu wenye asili ya Tanzania. Umekuwepo mjadala wa jambo hili, kwamba wakati umefika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iruhusu watu wanaotaka kuwa na uraia wa zaidi ya nchi moja. Lakini mimi ningependa nitowe mawazo binafsi, maana suala hili halijaletwa katika serikali rasmi, ni mambo ambayo yamekuwa yakijadiliwa tu katika mikutano mbali mbali na mijadala mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba nitowe maoni binafsi. Wale wanaojenga hoja kwamba jambo hili lina mantiki na jambo hili lina maslahi. Bado hawajalijengea hoja ambazo zinaweza kunifanya na mimi nikakubali kwamba jambo hili lina maslahi na nchi yetu. Maana hoja wanayoitumia ni moja, wanasema wapo watu wenye asili ya Tanzania au Zanzibar wako nje wana uwezo mkubwa sana wa fedha na wako tayari kuekeza hapa nchi. Sasa tukiwaruhusu wakiwa na uraia wa zaidi ya nchi moja watakuwa tayari kuja kuekeza hapa Zanzibar. Sasa suala hili mimi binafsi linanitia wasi wasi, kwa nini linanitia wasi wasi. Najiuliza mtu anayeipenda Zanzibar, ana asili ya Zanzibar au Tanzania, hivi kwa vile hana uraia wa Tanzania ndio iwe kikwazo cha kuekeza hapa.

Mhe. Spika, najiuliza wale wageni ambao wanakuja kuekeza hapa inakuaje. Kwa hivyo, nasema sioni hasa ile mantiki na hoja, inawezekana hoja ipo lakini nafikiri wale wanaotetea jambo hili pengine hawajapata nafasi nzuri zaidi ya kujenga hoja juu ya jambo hili. Kwa hivyo, sisemi kwamba ni jambo baya. Lakini nasema bado wanaolitetea jambo hilo hawajajenga hoja za kuingia kwenye masikio na akili. Kwa hivyo, waendelee kufanya hivyo huwenda wakapata sababu za msingi zaidi kuliko hii wanayoitaja.

Sababu ya pili Mhe. Spika, ambayo inanipa wasi wasi, najiuliza tuchukulie mwananchi A ana uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, halafu ana uraia wa nchi nyengine C. Sasa Jamhuri ya Muungano na ile nchi C zinaingia kwenye ugomvi na kugombana. Je, yule raia mwenye uraia mbili atakuwa upande gani, Mwenyezi Mungu apishilie mbali zikienda kwenye vita, atapendelea upande gani? Sasa hizi ndio hoja ambazo itabidi zitafutiwe majibu, halafu baadae tuzijadili na hatimaye serikali ipate nafasi ya kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba aliniuliza kwa nini nimesema serikali yenu. Hili neno serikali yenu tumelitumia makusudi kwa falsafa ya kutaka kuwafanya wananchi wajione kwamba hii ni serikali yao na waendelee kuiunga mkono. Maana kama ningesema serikali yetu, basi wangedhani pengine ni serikali ya Rais Karume, mimi na hawa mawaziri na pengine Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na walioko nje ya Zanzibar hii sio serikali yao. Lakini ninaposema serikali yenu, maana mamlaka ya kuongoza nchi yako kwa wananchi na nyinyi ndio wawakilishi wa wananchi, kwa kuwa hii nyinyi ni serikali yenu na wale mnaowawakilisha pia ni serikali yao, basi ndio maana nikaona busara kusema serikali yenu, badala ya serikali yetu. Kwa hivyo, ni suala tu la kutafuta mantiki ya kuwafanya wananchi waone kwamba hii ni serikali yao na wala sio serikali ya kikundi fulani cha watu.

Mhe. Mtumwa Mbarak alisema uko mti au majani, mlakasa unakimbiza maji na kwa hiyo tuwatake wataalamu wetu wa mazingira waufanyie utafiti. Tutalipokea shauri hilo na wataalamu wetu bila shaka watalichukua na kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, kaka yangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary, alisema katika hotuba yangu sikusema chochote kuhusiana na kura ya maoni, kuhusu kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa na akasema kuwa angenitarajia sana niseme kwamba ninawataka wananchi wapige kura ya ndio. Pengine kama alivyosema alimnukuu *professor* Ali Denge Makame, pengine compyuta imeruka maneno.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwamba compyuta haijaruka maneno, nilifanya kwa makusudi, niliona busara. Maana wakati mwengine busara inakutuma kwamba yako mambo ambayo ukiyazungumza mara moja, ukiyazungumza mara mbili, ukizungumza mara tatu na unaowaambia ni watu wazima kama wewe na wana akili timamu. Basi kuna hatari ukiendelea kuwaambia tu wakafikiri anatufanya kama watoto. Kwa hivyo, mimi nikasema ninaogopa, nimelizungumza jambo hili na kwa sababu najua nazungumza na watu wazima wenye busara. Katika vikao mbali mbali nimekuwa nikisema kwamba jamani nchi yetu inahitaji umoja na maelewano ni jukumu la kila mwananchi wa Zanzibar anayeitakia mema Zanzibar, kuhakikisha kufanya kila lililo katika uwezo wake kuhakikisha kwamba amani na utulivu unadumu. Kwa sababu bila ya amani basi hatuwezi kuleta maendeleo ya kweli katika nchi.

Kwa hivyo, ushauri wangu, kwa kuwa natakiwa niseme jambo lolote nasema hivi:-Kwamba kwa kuwa wananchi wa Zanzibar ni watu watambuzi sana katika masuala ya siasa, wana maarifa makubwa sana katika maarifa ya siasa. Nawatarajia basi wafanye maamuzi ambayo ndani ya roho zao na kwa kuwa

wanamuamini Mwenyezi Mungu, hivyo wafanya maamuzi ambayo yatasaidia katika kujenga umoja na utulivu. Sina haja ya kulisema jambo hili ni jambo gani, kila mmoja ndani ya roho yake anajua kwamba nikifanya jambo fulani, basi umoja na amani utapatikana. Kwa hivyo, labda niseme jambo hilo.

Baada ya kutoa maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri Kiongozi kwa ufafanuzi huo. Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi, wale wanaoafiki hoja ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Afisi ya Waziri Kiongozi wanyanyuwe mikono juu. Wale wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU 12 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 303,827,000 |
| Kifungu 03 | Afisi Kuu Pemba | 78,173,000 |
| Jumla ya Fungu | | **382,000,000** |

**FUNGU 13 – AFISI YA WAZIRI KIONGOZI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 03 | Afisi Kuu Pemba | 305,552,000 |
| Kifungu 04 | Idara ya Mipango na Sera | |

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri Kiongozi nimeambiwa ametangaza nia. Kwa hivyo, tulikuwa tumeshauriana tukasema tumpatize kabisa huwenda mambo yake yakawa mazuri ikawa hatumpati tena. Mimi Mhe. Mwenyekiti kuna mambo nilikuwa nachangia katika Idara ya Mipango. Kwanza suala la *Parliamentary Fund*, kwa kweli majibu yake hayakunifurahisha vizuri, hilo naliacha kuna wakati nitalipata na nitalieleza vizuri katika idara nyengine.

Lakini hapa nilichosimamia ni suala la walemavu. Nilimuomba Mhe. Waziri Kiongozi suala la walemavu walionyang'anywa afisi pale Wete alifanyie kazi

kidogo, halafu aje anijibu. Nilisema kwamba kuna Afisa Tawala wa Wilaya ya Wete amewafurusha walemavu wasioona katika jengo pale, kwa kweli hali sio nzuri. Najua Mhe. Hamza Hassan labda alitaka kunijibu lakini hakupata nafasi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, nipate maelezo kuhusiana na kadhia hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Saidi Ali Mbarouk, nakiri kwamba kweli nilikuwa nataka nimjibu swali hili, lakini kutokana na muda niliomba radhi kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya hawa wenzetu Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ambao wasioona, Mhe. Mwenyekiti, ile afisi hawajanyang'anywa wala hawajafurushwa. Isipokuwa sasa hivi tumewaazima Tume ya Uchaguzi NEC wana kazi yao kwa dharura, lakini baadae tutawarejeshea wao wenyewe. Wao tumewahamishia tu kutoka jengo lile na kuwahamishia sehemu nyengine pale pale karibu tu ambapo ni Afisi ya Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi. Kwa hivyo, hilo jengo bado ni la serikali, hatujawanyang'anya isipokuwa kutokana na uhaba wa hizo nafasi tumewaondoa mara moja tu, lakini baadae wakishamaliza shughuli zao watarudi tena. Walemavu tunaendelea kuwalea, ahsante.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sidhani kama uamuzi huo ni sahihi. Kuwahamisha wasioona katika afisi tu kwa sababu kuna Tume ya Uchaguzi, mbona katika akili haina mantiki sana, kwa nini wasihamishwe watu wengine wahamishwe wao au kwa sababu hawaoni? Halafu eneo walilowekwa liko vichochoroni haliwezi kufikika kwa hali yao, wale ambao angalau wanafimbo zao ni rahisi kufika. Lakini huko walikopelekwa sio rahisi Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri Kiongozi uamuzi huo waubatilishe, watafute eneo jengine hao NEC wakafanye kazi, lakini wale wagonjwa jamani wasioona na kila mmoja hapa atafikia huko pengine, sio vizuri kwa kweli ningeomba uamuzi huo ubadilishwe Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, hii hoja tuliizungumza sana na watendaji wangu, na tuliifanyia kazi sana na bado naahidi tukishakamilisha kupitisha bajeti yetu, nitakwenda kulishughulikia mimi mwenyewe. Tukijaaliwa tutajitahidi warejee katika lile eneo lao, lakini kwa kuwa Tume ya Uchaguzi NEC tayari wameshaanza shughuli zao, tuatajaribu kuangalia mazingira ya kuwatafutia sehemu nyengine. Bado naendelea kusema kwamba hatujawanyang'anya tuliwahamisha kwa dharura na hili suala tunalichukua na tutalifanyia kazi na tunakuahidi Mheshimiwa Mjumbe kabla kikao cha Baraza hili tutakuja kukujibu, ahsante.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Nimependa hilo jibu lake, na *Inshaallah* namuamini, kwa hivyo tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 04 | Idara ya Mipango na Sera | 549,100,000 |
| Kifungu 09 | Huduma za Waziri Kiongozi | 345,699,000 |
| Kifungu 18 | Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali | |

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii nilisema nataka maelezo kidogo kuhusu kauli ya Rais aliyoitoa Gombani na hii hotuba ya Waziri Kiongozi aliyoiandika ipi mojawapo ni sahihi tuifuate, lakini akati wa kujibiwa masuala haya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi alizidi kunichanganya sasa katika watu hawa watatu au vyombo hivi vitatu, Rais, Waziri Kiongozi na Afisi ya Waziri Kiongozi yupi tumfuate kwa kauli yake iliyokuwa ni thabiti.

Mhe. Rais alitamka kama tayari amefurahishwa ni kauli ya Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kukubali suala la mafuta kutolewa katika orodha za Muungano, lakini suala hili kwa hotuba hii linaanza kutaka kujadiliwa sasa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi anatwambia haya ni mambo mengineyo sasa tusiende hivyo tunataka ufafanuzi zaidi. Kauli ya Rais na kauli ya hii hotuba ipi tuifuate ili wananchi wasichanganyikiwe na la kufanya.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti napenda kutoa maelezo yafutayo, lakini kabla sijatoa maelezo naomba nitoe hadithi pengine Mhe. Omar Ali Jadi akanifahamu kwa wepesi zaidi.

Alikuwepo mfalme mmoja akamwambia mtendaji wake akija mtu yoyote usimpe msaada, sasa siku moja akenda shemegi yake ndugu yake Mkewe akasema hapa nimeambiwa nisitoe chochote hakutoa chochote, yule akenda kwa dada yake jioni ikawa manung'uniko yule mfalme akakosa raha ikawa kazi yake kubembeleza tu mwisho akamwambia kwani imepita nini? Akamwambia aa! si watu hawasaidiani maana ndugu yake hakusaidiwa. Mfalme akaona hii ni kazi akakumbuka kumbe kule kuna mtu alimpa amri kwamba usimsaidie mtu yoyote. Sasa alipokwenda asubuhi akawa anafoka, akamwambia wewe huna akili? Akauliza sina akili vipi? Na umesema nisimpe mtu yoyote. Sasa akamwambia basi huwezi kutumia busara huoni kama yule ni shemegi yangu? Akamwambia si umenambia mtu yoyote akija nisitoe msaada?.

Sasa viongozi wanatoa kauli lakini wanaotekeleza ni lazima wawe na busara wajue kwamba ile kauli ya kiongozi kama anavyoitoa sasa wewe unaitizama unaitekeleza je? Sasa Mhe. Rais wa Zanzibar katoa agizo la haki kabisa, sasa sisi wasaidizi wake kwa sababu hilo jambo ni la kikatiba na sheria, sasa sisi tutumie busara kuangalia tunalitekeleza je? Sio kwamba unalifanya tu kwa sababu umepewa agizo. Sasa utaratibu wa kikatiba kama kama nilivyosema

kuliondoa jambo lolote la kisheria na katiba unafuata taratibu kwanza unawaandikia wanaohusika ili sasa mutayarishe mapendekezo maalum kwa ajili ya kupeleka kwenye Bunge au Baraza la kutunga sheria na kufanya masahihisho au marekebisho kwa mujibu wa jambo hilo linalofanywa.

Kwa hivyo naendelea kusema kwamba sote tunaiheshimu kauli aliyoitoa Rais wetu na kauli yake ndio yenye nguvu, lakini mimi nilichofanya ni kutekeleza agizo lake kwa kutumia hekma na busara.

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Mhe. Mwenyekiti babu yangu alikuwa ni mmalenga sana na akawahi kutunga mashairi mengi sana, kwa hivyo nina imani na viongizi wa kisiasa wamepitia kazi ya umalenga ni watu ambaokuwa ni wasanifu wa lugha. Kwa kauli ya Mhe. Waziri Kiongozi nina imani haki yetu itapatika kama Wazanzibar lakini bado isije kucherewa na sisi tuje kuipata angalau kidogo kwa hayo machache nasema tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 18 | Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali | 340,448,000 |
| Kifungu 20 | Idara ya Maafa | 194,586,000 |
| Kifungu 21 | Shughuli za Watu wenye Ulemavu | |

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Spika, shughuli za watu wenye ulemavu mimi nimechangia lakini bado sijajibiwa, kwa sababu nilichangia kwa kupata sehemu ya kufanyia kazi zetu kwa kuwa kila afisi tunayokaa tunatolewa.

**Mhe. Spika:** Sijui ni ipi kuhusu Ofisi au?

**Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani hoja ya Mhe. Raya Hamad nafikiri inalingana na ya Mhe. Said Ali Mbarouk na nilikwisha kuitolea ufafanuzi kwamba ni kweli kwamba walitolewa katika ile ofisi lakini sio kutolewa kwa kuwa wamefukuzwa au wamenyang'anywa, ila tumewaazima tu Tume ya Uchaguzi kwa sababu wana kazi na walikuwa hawana eneo.

Lakini kutokana na hoja aliyoisisitiza Mhe. Said Ali Mbarouk mimi nimeahidi tukishapitisha bajeti yetu nitakwenda mimi mwenyewe pale na watendaji wangu pamoja na huyo Afisa Tawala aliyewaondosha nimpige masuala kidogo, halafu baadae sasa tuangalie mazingira Tume ya Uchaguzi kuwatafutia sehemu nyengine ili wao waendelee kutumia hiyo nafasi yao, kwa hivyo hili Mhe. Raya nadhani tuamini tukijaaliwa tutalifanyia kazi bila ya matatizo yoyote.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Spika, kwa sababu nilisema kwa kupitia Waziri Kiongozi majumba ya serikali yapo tuweze kupewa angalau sehemu ya

kutulika au kiwanya tunaacho tuweze kufanyiwa marekebisho ya kujengewa tutafute pahala tukae.

**Mhe. Spika:** Hebu tueleze ni suala gani?

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Nilizungumza kwa ajili ya afisi kila tunapokaa tunahamishwa sio Wete tu Afisi zote sisi t unapata shida tukenda na tukenda kuomba jengo hatupati na tukipata tukipewa leo kesho tunaambiwa tuondoke.

**Mhe. Spika:** Sawa sawa kwa upande wa Afisi za Wete tayari majibu ametoa.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi :** Mhe. Mwenyekiti hata hiyo Afisi ya Wete ni Afisi ya serikali ambayo wanaitumia, kwa hivyo kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu na sisi wenyewe tutahakikisha kamba haya maeneo hawanyang'anywi tena. Lakini nataka nizungumzia kitu kimoja kwa sababu jumuiya ya watu wenye ulemavu sasa hivi kuna lile Baraza la watu wenye ulemavu lakini vile vile nataka kuzungumzia kitu kimoja kwa sababu Baraza la watu wenye ulemavu wama afisi zao mbali mbali katika maeneo mbali mbali.

Sasa hivi tunajaribu kuwashajihisha wawe wenyewe waanzishe afisi mpaka katika majimbo mimi mwenyewe mpaka sasa hivi ndani ya Jimbo langu ninayo afisi ya watu wenye ulemavu vile vile na hii haitokani na serikali moja kwa moja, isipokuwa wao wenyewe wanajipanga na sisi viongozi tunajitahidi kuchangia wanapata ile afisi. Lakini kwa haya maeneo ambayo wamo sasa hivi tutakakikisha kwamba hawanyang'anywi tena kwa sababu ni majengo ya serikali sasa labda tutajaribu kuangalia taratibu za kuweza kuwahalalishia ili wakamilike wao wenyewe, kwa sababu kweli kitu kama unakuwa hati au muongozo ulioupata kitaratibu za kisheria ndio kama hivyo mara unaambiwa hama mara hivi.

Kwa hivyo hilo kama tulivyosema nilipokuwa nikitoa mchango wangu kwamba Idara ya Watu wenye Ulemavu hatukuianzisha muda mrefu Mkurugenzi ndio kwanza, kama tulivyosema Pemba tuna upungufu wa watendaji kwa hivyo tukiongeza watendaji haya mambo mengine yataanza kupungua, nadhani Mhe. Raya Suleiman Hamad atuamini tutajitahidi kuwa pamoja nao Ahsante.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Spika, naomba tuendelee.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti nakushukuru niko katika fungu hulo la ishirini na moja shughuli za watu wenye ulematu na ni katika jumla kuu ya fungu dogo hilo, wakati nachangia nilielezea juu ya wasi wasi wangu ya kwamba bajeti ya walemavu iliyopangwa pale kwa mwaka uliopita

2009/2010 ni Shs. 225.7 milioni. Lakini hadi Machi kwa mujibu wa hotuba ambayo tumeipata kwa Mhe. Waziri walikuwa wameingiziwa asilimia thalathini tu ya fedha hizo, siku zote tunasisitiza kwenye baraza hili juu a umakini wa taasisi kubajeti kwa kukaribia yale mahitaji yao na tunajua kwamba kwa kupeleka fungu hili hapa na kama halihitajiki wakati huo tumezikosesha taasisi nyengine matumizi ambayo waliwa na kazi nayo.

Sasa sababu iliyotolewa na Waziri kuhusiana na hili ni kwa nini asilimia thalasini iliyotiwa katika fungu hulo haikuniridhisha kwa sababu tunaambiwa kwamba afisi hiyo ni mpya, Je, makadirio hayakuwa ya kweli na kama sio ya kweli kwa nini tena mwaka huu tunawapa Shs. 211 milioni wakati mahitaji hayo sio halali.

Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Nadhani ukiangalia katika mafungu yetu katika Afisi ya Waziri Kiongozi takriban hayakwenda na kupata asilimia kubwa sana kama vile ambavyo tumehitaji, kwa sababu yale malengo ambayo tumekadiria ndio yaleambayo amazungumza Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi mara nyingi huwa tunapanga lakini tunategemea kile ambacho tunakusanya na fedha hizi tunavyoziomba sivyo vile tunavyozipata tunaweza kuomba *hundred percent,* lakini baadae kinachokuja kinakuwa na kasoro sasa mimi nadhani katika bajeti ya mwaka huu vile vile tulipata muongozo kwamba matumizi ya serikali yatakuwa makubwa zaidi katika harakati za mambo ya uchaguzi na mambo mengine, ndio maana utakuta kuna baadhi ya maeneo vile vile kuna mapungufu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti bado namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kiasi tutakavyopata hizo fedha, tutajitahidi migao yetu iende kwa mujibu wa mahitaji yetu, lakini vile vile tuelewe kwamba fedha tunazozipata tunakwenda kwa mujibu wa *ceiling* tunayopangiwa. Ahsante.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti maelezo kidogo yanakaribia kufahamika lakini bado niitahadharishe serikali kwamba kundi hili la watu wenye ulemavu nalo ni muhimu katika jamii, tusiliondoshee *priority* kwa kweli nimeiangalia bajeti yote ni wao tu ambao wamepataasilimia ndogo sana kwa kipindi hicho cha mwaka huu.

Kwa hivyo naiomba serikali ilizingatie hilo tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 21 Shughuli za Watu wenye Ulemavu | 211,615,000 |
| **Jumla ya Fungu** | **1,000,951,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 16 BARAZA LA WAWAKILISHI**

Kifungu 02 - Utawala Unguja

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi tena nina suala langu kwa Waziri, wakati ninachangia tulizungumzia wengi wa wachangiaji vile vile pamoja na Waziri Kivuli wangu, tulizungumzia suala la kuanzishiwa mfuko wa Baraza la Wawakilishi, kwamba uwe na *fund* yake ili kupunguza matatizo ya fedha kwa mhimili huu mmoja muhimu ambao upo katika nchi yetu.

Lakini maelezo ambayo tumetolewa kwa kweli yanasikitisha sana sasa mimi niombe maelezo katika bajeti hii kuna mifuko imeshaanzishwa na katika kitabu hiki pia kuna mfuko nafikiri wa walemavu au maafa nao unaanzishwa, sasa sijui vipi ile inafanikiwa kuanzishwa? Lakini huu wa baraza ukawa hauanzishwi? Sisi wakati tunazungumzia msaada huo hatukuzungumzia asilimia ya GDP, tulisema tu tuanzishiwe mfuko.
Je, haiwezekani kuanzishwa mfuko huo mpaka tuzingatie asilimia hiyo na kama haiwezekani kwa nini hii mifuko mingine inawezekana kuanzishwa?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Narejea tena kusema hoja kimsingi serikali inaikubali sio imeikataa na hata Dk. Mwinyi ambaye ndio anasimamia masuala ya fedha alieleza hivyo na mimi bado narejea tena, Serikali imakiri hoja hii ni ya msingi lakini kutokana na makusanyo yetu tunakuwa hatuna hakiba hilo ndio tatizo lililokuwepo, kwamba kile ambacho tunakikusanya ndio kile kile ambacho tunakitumia.

Mhe. Waziri wa Fedha kazungumza vizuri hata mshahara ndio kitu ambacho kinapewa *priority* na ndio maana fedha za mshahara zikishatimia tu basi zinatolewa halafu ndio yanaaza kuingia haya masuala ya *other charge* ukiangalia hata huo mfuko wa maafa ambao umezungumza tumeutaja katika sheria lakini mpaka leo tumeshindwa kwa sababu hizo fedha za kuingiza pale pia inakuwa mtihani. Ndio maana serikali ikaamua itumie katika mfuko mkuu wa serikali kwamba inapotokezea bahati mbaya basi tunafukuzia kwenye mfuko mkuu wa serikali.

Kwa hivyo narejea tena hoja yako ni ya msingi Mheshimiwa, lakini bado tunaangalia hii kesi ambayo tunaipata ikiwa inatia tia moyo kidogo tutafanya kwa sababu maamuzi yameshafanyika kwamba Wizara ya fedha tukishaona

hali iko nzuri basi baraza lianzishiwe mfuko wake, sisi tunapenda sana kuhojiwa tunataka mnapotaka kutuhoji basi isiwe tena Mhe. Spika, kasema mimi mfuko wangu kidogo, joho lina aaa! Tunataka Mheshimiwa kajenga hoja tunataka kitu fulani anatia saini katibu fedha zinatumika hivyo ndivyo tunavyotaka. Ahsante sana.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti nakubaliana na maelezo lakini ningeshauri serikali ijifunze zaidi vipi wenzetu wameweza kwa haraka ambao wana hali kama sisi kuanzisha mfuko kama huu kwa sababu utakapoanzisha tutaipunguzia hata serikali ule mzigo, kwa sababu itakuwa wanaweza kujiombea fedha wenyewe. Kwa hivyo naomba serikali ifanye hiyo kazi tuendelee Mhe. Spika.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kuchangia nilizungumzia mambo matatu, moja nashukuru limejibiwa kuhusu suala hili la mfuko.

Lakini la pili nililozungumzia ni suala la CDF sasa kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri ina maana hii CDF itakuwa ndoto kwa Baraza la Wawakilishi kwa sababu mfuko haupatikani. Je, ndio inavyokusudia serikali hivyo?
**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti kama maelezo yangu yatakuwa hayajatosheleza Dk. Mwinyi ataeleza zaidi lakini kimsingi tayari tumeshafanya maamuzi kwamba zile fedha za miradi ya wananchi zimetengwa kama milioni mita tano sasa hizo ndio moja kwa moja sasa hivi ndio tumeanzishia huo mfuko wa CDF wa jimbo.

Kwa hivyo hili nafikiri halina mjadala tayari hapa nafikiri nikae ili Mhe. Waziri atoe maelezo zaidi . Lakini vile vile lazima liangaliwe na utaratibu wa kisheria kwa sababu hata CDF inayoanzisha jimboni ina taratibu zake vile vile ambayo inasimamia matumizi ya fedha na hata tulipokwenda kujifunza Kenya kule tulikuta kuna sheria ambayo inatoa miongozo na kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani hili suala maamuzi yameshafanyika sasa kama kuna taratibu za kisheria nitaomba Dk. Mwinyi atoe maelezo ya ziada ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisis ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti kimsingi hilo suala limeshakubalika hakuna mjadala wowote haturudi nyuma, CDF na sisi tutaianzisha na nashukuru waheshimiwa wajumbe walitushauri kwamba tusifuate mfano mmoja tu tutatafuta *model* mbali mbali ili na sisi tutafute njia yetu ya kutuongoza, nafikiri hilo tumelizingatia na cha kuanzia tukasema hizi fedha za safari hii ndio zitakuwa za msingi kwa kuanzia kwa kila Mwakilishi apate jimbo lake alau mradi mmoja hiyo ndio ya kuanzia.

Lakini tutaharakisha upesi upesi sheria tuilete na tukishapitisha sheria tu tunakwenda mbele Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 02 - Utawala Unguja

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Mwenyekiti mimi nilizungumzia masuala matatu kama nilivyosema mwanzo mawili tayari, lakini la tatu hebu twambieni serikali suala la masuala kwa Waziri Kiongozi linakubalika au halikubaliki.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti Mhe. Abubakari Khamis Bakary ni mwanasheria na mwanasheria siku zote hataki kitu cha kubabaisha babaisha kwa ndio maana tukasema kwa masuala ya papo kwa papo bado tutakuwa hatuwatendei haki wanachi wetu. Kwa sababu Waziri Kiongozi anapoulizwa masuala haulizwi masuala ya Wizara yake tu yeye ni Kiongozi wa mawaziri wote, kwa hivyo kitu anachokitoa kinatakiwa akitowe kilivyo kama Wizara ya kilimo vile.

Sasa mimi nadhani bado tuendelee kusubiri kidogo huu utaratibu wetu wa sasa hivi nafikiri waeheshimiwa wanaridhika unapouliza suala unafanya utafiti, na yeye anajua huyo haya masuala yanapoulizwa tunaambizana tutafute utafiti kwa sote tunajiuliza masuala ya nyongeza kule kule kwanza kabila ya kuja hapa, sasa Waziri Kiongozi akijibu tu yatakuja kumkuta kama yaliyomkuta mwenzetu kule akapata mtikisiko. Sasa mimi naomba kwa hivi sasa kwanza tustahamili lakini baadae tutalizingatia ahsante sana.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti hoja anayoieleza Mhe. Mjumbe ni hoja ya mantiki inaweza kuwa na faida nilikuwa namsikiliza vizuri sana katika mchango wake kasema inamchangamsha Waziri Kiongozi ili aweze kuelewa kila taarifa inayofanyika katika wizara mbali mbali na katika serikali kwa ujumla, kwa maana hiyo inamfanya achangamke aende mbio na awe makini zaidi.

Sasa nasema nia ni nzuri sana lakini katika kila jambo zuri linahitaji maandalizi mazuri ili lilete matarajio yaliyokusudiwa, sasa sisi kama ni serikali tumeona hoja yake ni ya msingi na ina nia nzuri. Lakini pengine tunahitaji muda kwa sababu hata mafunzo Mwenyezi Mungu anatuelekeza kwenye Qurani anasema mnapopata jambo lolote lile ambalo jibu lake hamlijui shauriyaneni. Sasa kwanye baraza mimi kama mtendaji mkuu wa serikali kuna kiongozi mkuu wan chi ni vizuri tukae tushauriane na kuelekezana kama dini yetu

inavyotutaka tufanye, bado ninaendelea kusema lile ni jambo la busara tupate muda kidogo tujadiliane baada ya kushauriana sasa tutatafuta njia namna ya kulitekeleza jambo hili.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Mwenyekiti nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri Kiongozi lakini tukijaaliwa kama tutarudi hapa barazani basi Baraza la mwanzo tutakukumbusha mmeshauriana vipi? Kama hatukurudi basi wengine tutawaambia wamkumbushe. Ahsante *(Kicheko)*

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 6,436,284,000 |
| Kifungu 03 | Afisi Kuu Pemba | 1,509,716,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **7,946,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 30 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 575,160,000 |
| Kifungu 03 | Afisi Kuu Pemba | 119,840,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | | **695,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 12 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 1,408,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **1,408,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU 13 AFISI YA WAZIRI KIONGOZI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 18 | -Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali | 100,000,000 |
| Kifungu 20 | -Idara ya Maafa | 274,725,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **374,725,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 16 BARAZA LA WAWAKILISHI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | -Utawala Unguja | 1,542,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **1,542,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa wajumbe wale wanaoafiki wanyanyue mikono wasioafiki. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja ilamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni kwa kazi nzuri mliyoifanya na kama tulivyokubaliana katika utaratibu kesho Jumamosi lakini shughuli zitakuwa zinaendelea na kesho tutakuwa na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa hivyo tusije tukasahau kwamba siku ya jumamosi itakuwa ni siku ya kazi rasmi kama vile tulivyokwisha kukubaliana.

*(Saa 1.45 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 19/06/2010 Saa 3.00 asubuhi)*